# MWONGOZO WA USHAURI WA KIKUNDI CHA ADVANCE/ KIKUNDI TANGULIZI

Maandiko yametolewa kutoka kwa Biblia Takatifu, Toleo mpya la kimataifa (NIV), haki mliki (c)1973, 1978, 1984,2011 na Biblica, inc yametumiwa kwa ruhusa ya zondervan. Haki zote zimehifadhiwa dunia nzima. www.zondervan.com " NIV" na " New International Version"ni alama za bishara zilizosajiliwa katika ofisi ya Amerika ya alama za biashara na hiki- miliki.

Kimeandikwa na **Ben Jack**

© 2021 The Message Trust

# YALIYOMO


## KARIBU KWENYE ADVANCE 6

## MWONGOZO WA KIKAO 11

KARIBU KWENYE ADVANCE 12

UTAMBULISHO WA MWINJILIST 16

UJUMBE WA MWINJILISTI 20

JUKUMU LA MWINJILISTI 25

NGUVU YA MWINJILISTI 30

KUJITOLEA KWA MWINJILISTI 35

UTII WA MWINJISTI 39

SIFA YA MWINJILISTI 44

FURSA YA MWINJILISTI 50

KUJIZATITI KWA MWINJISTI 55

MSUKUMO WA MWINJILISTI 60

FARAGHA 65

## VIKAO VYA ZIADA NA RASLIMALI 71

KIKAO CHA ZIADA CHA KWANZA UINJILISTI WA MAZUNGUMZO 72

KIKAO CHA ZIADA-UTETEZI WA IMANI 76

KIAMBATISHO MAFUNDISHO YA INJILI 80

KIAMBATISHO SIMULIZI YA INJILI 81

KIAMBATISHO MFANO WA MAZUNGUMZO YA DAKIKA KUMI YA INJILI YA/KWA VIJANA 82

KIAMBATISHO NJIA ZA INJILI 83

KIAMBATISHO MAKALA YA "KITU KIMOJA" 84

USOMAJI ULIOPENDEKEZWA 88

MASWALI YA UWAJIBIKAJI 90

# KARIBU KWENYE KIKUNDI LA ADVANCE/ KIKUNDI TANGULIZI

# MAKUNDI TANGULI/ YA ADVANCE HUKUZA NA KUENDELEZA WITO WA WAINJILISTI KWA KUWAUUNGA MKONO KWA KUJITOLEA KWAO KUTANGAZA INJILI.

Kitabu hiki cha advance kilitokana na jozi/ maoni ya Andy Hawthorne (mesaage Trust Uk) kukusanya wainjilisti wanaohubiri injili kumi na wawili ili kuwaendeleza na kuwaimarisha na kuhimiza wainjilisti wengine wenye uzoefu kufanya vile vile kwa wale ambao wanapa ushauri mwishowe waweze kuanzisha makundi yao wenyewe.

Kupitia mikutano ya kila mwezi, wanachama hupata mafundisho, wanaimarishana kupitia majadialiano na wanashariki kwa wazi kuhusu maisha yao ya kibinafsi na yale ya kiroho. Habari za hivi punde/sasisho kuhusu fursa za kuhubiri injili na kuhimizana kwa matunda ya fursa hizi hutumwa kwa wanachama au kikundi kwa kutumia whatsapp au/ama namna nyingine kama hyo.

Baada ya mwaka mmoja katika kikundi cha Advance kila mwinjiisti hutafuta watu wengine kumi na wawili ambao watawashauri kwa njia hiyo hiyo, Advance huwaona wainjilisti wakiendeleza wainjiisti kusababisha ongezeko kubwa ulimwenguni la idadi ya wakristo ambao bila aibu watashariki injili, iwe kwa jukwaa au kupitia mikutano/kukutana kwa kila siku na marafiki, jamaa, familia au wageni.

Inavyoongezeka duniani kote, Advance ni jibu la moja kwa moja kwa haja ya wasilianiaji wa injili ya yesu walio na shauku na wasio na aibu kuwezeshwa, kuhimizwa na kuungwa mkono.

## KANUNI TANO ZA HARAKATI

Unapoanzisha kikundi chako cha Advance kuna kanuni tano ambazo haziwezi kujadiliwa ambazo ni lazima uzingatie.

### 1. MIKUTANO YA MARA KWA MARA

Mikutano ya kila siku inapaswa kuwekwa kipaumbele na wanachama wa kikundi. Ni muhimu kwamba wakati watu wanajiunga na kikundi,wanajitolea kuhundhuria mikutano. Makundi yanapaswa kuhimizwa kuchukulia kikao hivi takatifu. Wanachama hawapaswi kuruhusu ushirika wa kuzungumza au mikutano mingine “kuwa ya maana Zaidi” hakuna kitu kinachoweza kuwa cha muhimu Zaidi kuliko kuhakikisha kuwa wamejitolea kuandaliwa kwa kazi ambayo mungu amewaita wafanye.

### 2. KUNOA

Kujitolea kusoma/kujifunza biblia ili upate maarifa ya kina ya injili huchukua sehemu muhimu ya wakati wa kikao kila mwezi,na pia inajumuisha fursa za uhakiki mzuri wa uelewa wa mtu na utumiaji wa uinjilisti na injili haswa kupitia majadiliano.

**3. UWAJIBIKAJI**
Kujitathmini kwa uaminifu kuputia dodoso la maoni/hoja juu ya maoni na kushiriki kwa wazi wakati wa mikutano ya kikundi imeundwa kuhakikisha kwamba tunaishi maisha ya uwajibikaji na matakatifu tunapojaribu kuwa waaminifu kwa kuishi na kushiriki injili. Kujiweka wazi na kuwa mwaminifu katika kikundi inaweza kuchukua muda kuikuza laikini inapaswa kuhimizwa kwa/na mfano wa kiongozi wa kikundi.

**4. MAWASILIANO**
Kuhakikisha klla mwana chama ana habari za hivi punde kuhusu fursa za kuhubiri, maombi, hadithi za wokovu kupitia barua pepe au njia ya ujumbe wa maandishi ya kikundi, hukakikisha kwamba makundi yanasaidiana kama jamii ya wainjilisti, na pia mawasiliano ya kila wakati kati ya vikao hujenga uhusiano wa ndani kama familia katika vikundi.

**5. KUZIDISHA**
Kujitolea kuchunguza wazo la kuzidisha kwa nia ya wanachama wa kikundi/washiriki kuanzisha vikundi vyao wenyewe(wakati wanaendelea na kikundi asili) ndani ya miezi kumi na mbili na kumi na nane ya kujiunga na kikundi. Sio wote walio katika kikundi chako wataanzisha vikundi vyao wenyewe lakini kwa kutumia rasilmali hii na kuwa na nia juu yake wengi wanaweza na wataanzisha vikundi vyao, kuhakikisha kuwa kuandaa,kuwezeshwa na kutia moyo wakristo waliojitolea kuhakikisha uinjilisti unaendelea kukua na kuenea kote ulimwenguni.

## JE! NI KWA AJILI YANGU?

Iwe unayo fursa ya kuhubiri injili katika jukwaa or auunapenda kuwafikia wale ambao unakutana nao kila siku, maswali haya matatu yatakusaidia kuamua ikiwa kuanzisha(au kujiunga) na kikundi cha Advance ni kwa ajili yako.....

**IMANI**
Je! una imani kuwa injili haijapoteza nguvu zake na ni njia ya pekee ambayo myu anaweza kujua maisha ya kweli na wokovu?

**UWAZI**
Je! unatamani kuwasilisha injili kwa uwazi kupitia mazungumzo ya kibinafsi au kuhubiri kwenye kujwaa?

**MWALIKO**
Je! unatamani fursa za kupeana mwaliko kupokea tumaini la injili na kuona watu wakiingia katika uhusiano wa milele na yesu?

Ikiwa umejibu "ndiyo" kwa maswali haya, basi tafuta kukusanya wengine ambao wanaeza sema "ndiyo!" na utumie mwongozo huu wa ushauri wa kikundi cha Advance na muanze safari pamoja.

## MWONGOZO WA KIKAO

Mwongozo huu unajumuisha vikao kumi na mbili ambavyo vitakuchukua katika mwaka wako wa kwanza wa safari ya Advance kama kikundi. Ikiwa wewe ni mwinjilisti mzoefu na/au una ujasiri katika kuongoza kitu kama hii unaweza taka kutumia vikao/vipindi hivi kama mahali pa kuanzia, ukiongeza na kurekebisha yaliyomo ili kuweza kutimiza matakwa ya kikundi chako. Ikiwa haya ni mageni kwako jisikie huru kufuata vipindi/vikao neno kwa neno na maagizo-utakuwa na kila kitu unachohitaji kukua kwa pamoja kama kikundi.

Vipindi/vikao hivi kumi na mbili zimebuniwa kutoa uelewa wa injilii, uinjilisti na sifa/tabia ya mwinjilisti, ambayo huanza baada ya kipindi cha utangulizi (kikao cha kwanza).

## SIFA KUU ZA MWINJILISTI

**WAINJILISTI WANAO FUNDISHA BIBLIA WANAJUA BIBLIA KWA UNDANI/KWA KINA (KIKAO CHA PILI, CHA TATU,NA CHA NNE)**
Ni lazima tujue ujumbe ambao tunatangaza kwa undani/kina iwezekanavyo. Kufanya hivi ni lazima tujitoleee kujifunza na kusoma neno la mungu, ili tangazo letu yasitegemee/lisiwe msingi wa maoni yetu na mawazo juu ya injili, bali kwa kile neno la mungu linafundisha.

Maneno ya kuwaagiza ya Yesu Kristo katika Mathayo Ishirini na nane yanatuita tufanye wanafunzi wa mataifa yote, kuwafundisha watu kutii kile Yesu alichoamuru. Tunaitwa sio tu kuwa wainjilisti lakini wainjilisti wanofundisha Biblia, wanaoshiriki ukweli badala ya maoni yao. Vikao hivi vitatu vitazingatia injili na uinjilisti kwa kuangazia kile Biblia inafundisha kuhusu Baba,Mwana na Roho Mtakatifu.

### WAINJILISTI WANAOSALI/OMBA HUTENDA KATIKA/NDANI YA NGUVU YA KIROHO (KIKAO CHA TANO NA KIKAO CHA SITA)

Tunapaswa kujitiisha kwa nguvu za roho mtakatifu kwa kazi ya uinjilisti, kwani sio nguvu zetu bali ni nguvu za mungu huleta wokovu. Kwa hivyo tunajitolea kwa kuishi kwa maombi, kumwomba mungu atupe fursa za kushiriki Imani yetu na kuona maisha yamebadilishwa kama matokeo. vikao hivi vinachunguza maisha ya kiroho ya mwinjilisti na kutoa fursa kuchunguza maisha yetu ya maabudu na athari yake ya moja kwa moja zinazo katika uinjilisti wetu.

### WAINJILISTI WALIOAJIBIKA HUISHI MAISHA MATAKATIFU (KIKAO CHA SABA KIKAO CHA NANE)

Utakatifu ni kiini cha uinjilisti. Kushiki nguvu unayobadilisha kwa njia halisi inammanisha kuishi maisha ya uwajibikaji ambapo maisha na mienendo yetu ya tukiwa kwenye jukwaa ni sawa na maisha na mienendo yetu tusipokuwa kwenye jukwaa, tukishangiliana kwa mafanikiobna kusimama na wengine katika kutofaulu ni muhimu tunapotafuta kukua kama watu watakatifu wakishiriki ujumbe mtakatifu. Vikao hivi huzingatia utakatifu wa mwinjilisti, ikithibitisha hitaji la uwajibikaji na unyenyekevu kama sifa kuu ya wale wanomtumikia mungu.

### WAINJILISTI WALIO JITOLEA: KUWA NA NIA KATIKA KAZI HIYO (KIKAO CHA TISA NA KUMI)

Nia ni ufunguo wa uinjilisti ni lazima tujue na tuchukue fursa za kila siku kushiriki upendo wa mungu, sio kushiriki tu bali kuwaalika wale ambao wanaousikia katika maisha mapya unayotoa, kuwasaidia kuanza safari yao ya uanafunzi. vikao hivi vinachunguza vigezo viwili muhimu ambavyo vinaweza kutofautisha katika kipaji/karama ya uinjilisti.: kuongezeka kwa nafasi ya kushiriki injili kila siku kwa ujasiri na nia ya kuwaalika watu katika ufalme katika kilele cha kila fursa ya injili.

### MWINJILISTI ALIYE NA MSUKUMO: KUCHOCHEA KANISA KUSHUHUDIA(KIKAO CHA KUMI NA MOJA)

Tunaposhikiriki injili na wale wanaoihitaji, ni lazima pia kanisa lichochewe kufanya hivyo pia(kushiriki injili) uinjilisti ni kazi\biashara ya kila mkristo kwa hivyo kuhimiza na kuchochea kanisa kwa kazi ni lazima liwe shinikizo la kila mwinjilisti. Kikao hiki kinachunguza jukumu la mwinjilisti kama mwenye kuhimiza kanisa kuweka ushuhuda wa kristo katikati ya wale ambao ni wafuasi wa yesu.

Mwaka wa Advance unafika tamati na kikao cha kumi na mbili kinachofanya kazi vizuri kama aina ya faragha, kutoa nafasi kwa kikundi kutafakari juu ya yote waliojifunza, yote ambayo yamefanywa ndani yao na kupitia kwako na mungu., nakutazama mbele kwa pamoja kwa ni nini kitakachofuata?

## KUENDESHA KIKUNDI

Himiza kikundi cha karibia watu kumi na wawili (makundi ya jinsia moja ni bora kwa ajili ya awajibikaji) kukutana mara moja kwa mwezi kwa masaa mawili. Wakati huu kiongozi wa kikundi ataongoza kikao pamoja na maombi, majadiliano na uwajibikaji. Mwongozo huu unakupa kila kitu utakachohitaji ili kuongoza na kuendesha kikundi kila kwezi kwa mwaka wake wa kwanza.

### MGAWANJIKO WA VIKAO

Kila mwongozo wa kikao unaanza na utangulizi mfupi **ni kikao katika sentensi.**

**Sehemu ya kikao katika sentensi** inatoa mafundisho ambapo kikao kimezaliwa, utaka kusoma hii kabla ya kuongoza kikao kwani utakusaidia kukupa ufahamu wa kina sura ya kikao. Jisikie huru kuingiza nyenzo hizi zozote kwenywe kikao ikiwa una wakati na ufakiriki kuwa itaweza kusaidia, lakini cha msingi imekusudiwa kukusaidia kujiandaa kuongoza mafundusho yanayofuata.

Kutoka hapa unaweza kufuata mwongozo wa kila kikao kutoka kwa yaliyomo hadi wakati / muda wa kila kikao (kwenye mabano karibu na kila sehemu ya kikao) kwa karibu ama kwa uhuru unavyohisi unasaidia mradi hoja kuu ya kikao inawasilishwa wazi kwa usahihi. Walakini ni wazo nzuri kushikamana karibu iwezekanavyo na mwongozo wa kikao ili kuweza kufaidika zaidi kutokana na nyenzo ya mafundisho.

**Kila kikao kinaanza na wakati wa mapatanisho**, katika vikao vya awali hii ni wakati wa kujaribu kujuana na kuchunguza/kujadili jinsi kikundi kitaendeshwa, vikao vinavyozidi kuendelea muda mwingi unapeanwa kwa kushiriki hadithi na kila mmoja na kupotoa maoni kutokana na matumizi katika kikao kilichopita.

**Kisha kuna wakati wa maombi**, hakuna mwongozo jinsi hii inafaa kuchukua muda gani, wala njia nzuri au mbaya ya kuomba, munaeza kuomba kama kikundi au na mwenzio, kwa kifupi au kwa muda zaidi.

**Sehemu kuu ya mafundisho unafuata** na inajumuisha marejeleo ya maandiko, nukuu, na hoja za maswali ya majadaliano. Hapa ndipo utahitaji zaidi kutazama muda/saa. Bado kuna wakati zaidi wa majadiliano., la muhimu unahitaji kuacha nafasi/muda ya sehemu ya uwajibikaji mwishoni mwa kikao.usiruhusu wakati ufinywe kwa sababu unachukua muda zaidi kueleza hoja fulani ya mafundisho(pia kumbuka nyakati za sehemu hizi zinatofautiana kutoka kikao hadi kingine, kwa hivyo hakikisha kuzingatia wakati uliopendekezwa na urekebishe ipasavyo)

Baada ya sehemu ya mafundisho, **kuna sehemu ya majadialiano** na inahusisha maswali na nukuu inayohusiana na mada ya kikao. Labda hautakuwa na wakati wa kujadili kila kitu kilicho hapo, lakini tumejumuisha yaliyomo zaidi ambayo unahitaji ili uweze kuchagua kile kitakachokusaidia zaidi. Usione/ usihisi kana kwamba inabidi uharakishe kupitia kila kitu katika sehemu hii, badala yake zingatia tu vipengele vichache.

Kila kikao kinahusisha sehemu ya **matumizi** kuelekea mwisho wa kikao ambacho ni kitu cha kufanywa kati ya sasa na kikao kijacho kulingana na mafundisho. Jisikie huru kubuni yako mwenyewe maadamu inasaidia kufundisha na itasaidia kikundi chako kukua katika eneo hilo.

wakati mwingine wa **maombi** unafuata wakati huu na mwongozo kwa kile ambacho utaombea kama kikundi kulingana na mafundisho ya kikao, lakini utakavyoitekeleza/kuifanya na muda utakaochukua ni juu yako.

Mwishowe, kila kikao kinamalizika **na wakati wa uwajibikaji** ambapo karatasi za kujithamini zinaweza kukamilishwa/kujazwa, kugawanywa kuombewa. Unaweza pata nakala za makaratasi haya kutoka ukurasa wa sitini na tisa au pakua toleo ya PDF kutoka advancegroups.org/accountability

## VIPENGELE VYA VIKAO VYA HIARI

### MWELEKEO MAALUM WA MAOMBI

Chukua muda kwa kikundi chote kuombea watu wachache katika /ndani ya kikundi –omba juu ya maisha yao, familia, huduma, na chochote kingine wanachopendekeza. Jaribu kuombea kila mtu kila baada ya mikutano tatu kisha uanze tena.

### MAZOEZI YENYE FAIDA

Unaweza kutak a kuenda mitaani kwa saa li moja, ili uweze kutumia uliyo jifunza kwenye majadialiano na maombi kwa ushuhuda wa kibinafsi au usemi mwingine wa vitendo vya uinjilisti, vikundi vimeundwa kutusaidia kujiandaa kwa uinjilisti, lakini ikiwa una hamu, wakati unaweza kutolewa ili ufanye uinjilisti. Hakikisha kutoa wakati wa kujadili na kutoa maoni kutokana na zoezi hili.

### WAGENI

Ikiwa unapata msemaji au mgeni ambaye anaweza kuchangia wakati wa kufundisha na kujadili na kuleta uzoefu tofauti au kitu kipya kwa kikundi, basi waalike washikiri na kikundi chako.

### VIDOKEZO VYA KUSAIDIA KUENDESHA KIKUNDI

Panga mikutano ya kikundi kabla ya wakati na mbele sana zaidi ya kikao kinachofuata (miezi sita mbele ikiwezekana) tumia kitu kama doodle.com kama kifaa kinachofaa kwa kazi hivi.

Whatsapp au programu ingine ya mawasiliano/ kutuma ujumbe ni sawa/ kamili kwa

mawasaliano ya kikundi, maombi, na hadithi za wakovu kati ya wakati wa vikao. Kama kiongozi wa kikundi jaribu kuendeleza hili kwa kuchangia mara nyingi iwezekanavyo. shiriki hadithi zako, uliza watu wapeane ombi lao la maombi, toa viungo vya raslimali,podikasiti, video fupi fupi za YOUTUBE. Ikiwa utakuwa mstari mbele dhidi ya kufanya mambo haya basi wengine pia watajihusisha.

CHAKULA pia inaweza kuwa njia nyingine ya kuwaleta watu pamoja na kuwapatanisha, kwa hivyo unaeza taka kuendesha kikao hivi wakati wa chakula cha jioni.

Fanya wanachama wa kikundi chako wafikirie juu ya kuanzisha vikundi vyao mapema ili wakati wengine wenye uwezo wakujiunga na kukundi chako watakapokuja unaweza kuwaunganisha na vikundi vipya vinavyozinduliwa kutoka kwako.

Kutana mahali ambapo watakuwa huru kujadili, kuomba na kushiriki wakati wa uwajibikaji. Mkahawa ni nafasi nzuri kwa wengine lakini wengine hutaka/wanahitaji faragha Zaidi wanaposafiri/shiriki kwa hivyo fikiria sehemu/ nafasi yako ya mkutano kwa uangalifu Zaidi.

Vitabu kama UKRISTO WA KIMSINGI/BASIC CHRISTIANITY cha JOHN STOTT na INJILI RAHISI/ THE SIMPLE GOSPEL cha BEN JACK ni vitabu vifupi vya mada husika ambavyo vinaweza kutumiwa kama kazi ya ziada ya nyumbani kwa kusoma aidha kwa kufuatilia sura kwa sura kila mwezi au kutumika kwa maudhui ya kikundi na majadiliano baada ya kumaliza vikao katika mwongozo huu.

# KIKAO CHA KWANZA

# KIKAO CHA 1:
# KARIBU KIKUNDI CHA ADVANCE

**Mkutano wa kwanza unafaa kutimiwa kama nafasi ya kujuana,kujadili jinsi kikundi kitaendeshwa na pia kuanzisha majadaliano kuhusu uinjilisti na sifa tano za mwinjilisti.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI

Kupitia Kikundi cha Advance tutakua pamoja katika sifa tano za mwinjilisti, kuhimizana na kuandaa kila mmoja tugitegemea uwezo wa mungu.

## ASILI YA KIKAO

Mahali pazuri pa kuwakaribisha watu na katika safari ya Advance ni kukumbuka kwamba wito na uinjilisti ni kitu binafsi. Tazama jinsi yesu anavyomuita Andrea na Petro wamfuate mwanzo wa injili ya (Marko 1: 16-18) anamwita mvuvi mdogo kutoka ukingoni wa bahari na kuwaambia waweke nyavu zao chini (biashara yao) na wamfuate, kwani atawafunza kuwa wavuvi watu. Je! Mungu anakuita kwa kutumia maneno haya? labda iwe unafanya kazi sawia na ndugu ambao yesu aliita. Yesu aliwaita kibinafsi Andrea na Petro kwa kutumia uvuvi kama kipatanisho.

Mungu anaita kila mtu kibinafsi kuwa mwinjilisti kwa kuunganisha au kupatinisha shauku zetu na fursa ya kuelewa mungu ni nani. Uwe mwana mziki, msani, mwana sayansi, muuguzi, mmliki biashara. Iwe ni wito, au kipaji chako mungu anaweza kukitumia kutengeneza fursa ya kutangaza habari njema ya mungu. Lengo la uinjilisti ni kuunganisha watu kwa habari ya mungu. Ujumbe wa mwinjilisti ni wito wa Imani katika yesu kristo-kuamini na kuwa mtiifu kwake, kwamba tutageuka kutoka kwa kumkataa mungu na kukubali utawala wake. Tunapotambua kwamba tumeumbwa kwa ajili yake, tunaelewa kuabudu ni nini, na tunaona nguvu ya mabadiliko ya roho mtakatifu katika maisha yetu. Watu hujua utakatifu tunapogeuza maisha yetu yawe maisha ya kujieleza au yanayoonyesha maabudu kwa kupitia utii, dhabifu, imani na upendo (WAGALATIA TANO: 13 –29)

Katika Kutoka Nne: Moja ; mungu anamuagiza Musa kwenda kwa Farao na kumwambia: 'waacha watu wangu waende '. Leo mungu anatamani kuwaweka mateka huru kotoka kwa dhambi.

Kama Musa tunaombwa kwenda ulimwenguni na kutangaza ujumbe wa uhuru: kwamba hakuna haja ya kuwa mtumwa tena kwani mungu amefanya iwezakanavyo kwetu kuishi kwa uhuru kupitia kwa Yesu na kwa nguvu ya roho yake (Warumi 8:2). Kusudi la uinjilisti ni kama ilivyokuwa kwa Musa na watu wa Israeli- Kuabudu.

"Wacha watu waangu waende ili waweze kuniabudu"

Tunapaswa kuwa waabudu ambao wanashuhudia ili wengine wa mwabudu na kushuhudia.

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 20-30)

*Chukua muda ili uweze kuwatambulisha kila mtu kwenye kikundi na waanze kujuana. Unaweza hitaji mchezo mfupi au uliza kila mtu aeleze kwa kifupi kujihusu. Baada yah ii kwa mtindo wako mwenywe au soma sehemu ya utambulisho*

*ukurasa wa Sita kama njia ya kueleza jinsi kikundi kitaendeshwa miezi ijayo.*

## MAOMBI

*Omba kutoa muda kwa Bwana na juu ya hali yeyote ile au changamoto iliyoangaziwa wakati wa mapatanisho.*

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

*Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe, ama kwa kusoma neon kwa neno, au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.*

> "lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kumaliza mwendo wangu wa huduma ile niliyopokea kwa Yesu Kristo, kuishuhudia habari njema ya neema na mungu."
>
> **MATENDO YA MITUME 20:24 BIBLIA TAKATIFU**

Kwa kifupi "uinjilisti" au "kueneza injili" inamaanisha "kutangaza habari njema". Habri njema inayozungumziwa ni injili ya yesu Kristo: kwamba ubinadamu wenye dhambi(waasi) umepatanishwa na mungu kupitia kwa kazi ya kuokoa ya yesu. Tunawqeza kujua uzima wa milele na kufurahia uhusiano kamili wa mungu kwa sababu yesu alichukua kifo ambacho tulistahili.

Angalia mafafanuzi haya mawili ya uinjilisti:

> "uinjilisti **ni kuwasilisha yesu kristo** kwa **watu wenye dhambi** ili kwa nguvu ya roho mtakatifu **waweze kumtumainia yesu kristo**."
>
> **J. I. PACKER**

> "**Tangazo la kristo wa kihistoria, wa kibiblia**, kama **mwokozi na Bwana** kwa nia **ya kuwashawishi** watu waje kwake **kibinafsi** na hivyo **wapatanishwe** na mungu"
>
> **BILLY GRAHAM**

**SWALI:** Je! Tunaweza kujifunza nini juu ya jukumu la uinjilisti kutoka kwa muhtasari huu mfupi (maneno mengine yameangaziwa kwa majadiliano maalum)?

Uinjilisti unahusisha ujumbe uliotangazwa wa yesu aliyefufuka na jaribio kumshawishi msikilizaji kupokea na kukubali habari njema. Lakini hata kama maneno ni muhimu katika uinjilisti ni lazima twende Zaidi ya mawasiliano ya maneno.

David Watson alisema kuwa: " isipokuwa kuna dhirihisho la nguvu ya roho, tangazo la injili litakuwa bure, halitakuwa uinjilisti, uinjilisti nbi shughuli ya kiroho inayofaa tu wakati mungu anaposonga kwa nguvu. Ikiwa uinjilisti itakuwa tu juu ya kubadilisha mawazo ya watu; tungetegemea tu ushawishi pekee yake. Lakini uinjilisti unahusu wokovu. kupitia ujumbe wetu roho ya mungu inahukumu, inatoa Imani na .kuanza mabadiliko ya roho. Uinjilisti bila nguvu roho ya roho ni uuzaji tu. Kwa upande mwingine kama Leonard Ravenhill alisema: '' tunaweza kuwa na uhakika kuwa njia yeyote ya uinjilisti itafanya kazi ikiwa mungu yumo ndani ''

Kusudi la uinjilisti ni kufanya wanafunzi-waabudu ambao wanaabudu kwa roho na kweli. Imesemwa kuwa ibada na uinjilisti ni pande mbili za sarafu moja, na kweli kwamba ushuhuda wetu kwa ulimwengu ni tendo la kuabudu, tendo la utii na kujitolea kwetu kwa mfalme.

Vikao hivi nya kikundi cha Advance, vitakusiaidia kukomaa kama mwabudu halisi na kuona na kuona unakua katika sifa tano msingi za mwinjilisti.

### WAINJILISTI WANAOFUNZA BIBLIA

Ni lazima tujue ujumbe tunaotangaza kwa kina/undani iwezekanavyo. Iuli kufanya hivyo ni lazima tujitolee kusoma na kujifunza neno la mungu ili tangazo letu lisiwe kulingana na mawazo yetu au dhana yetu kuhusu injili bali kile ambacho neno la mungu linafundisha.

### WAINJILISTI WAOMBAJI/WANAOSALI

Lazima tujitiishe kwa nguvu ya roho takatifu kwa jukumu la uinjilisti kwani siuo nguvu zetu bali ni nguvu ya mungu ambayto huleta wovovu, kwa hivyo tunajitolea kuishgi kwa maombi, tukimwomba mungu atupe nafasi za kushiriki

imani yetu na kuona maisha yakibadilishwa kama matokeo yake.

**WAINJILISTI WANAOWAJIBIKA**
Utakatifu ni kiini chsa uinjilisti. Kushiriki nguvu inayobadilisha ya injili kwa njia halisi inamaanisha kuishi maisha ya uwajibikaji. Pale ambapo maisha na mienendo yetu tukiwa kwenye jukwaa inalinga na maisha na mienendo yetu wakati ambapo hatuko kwenye jukwaa. Kushangiliana kwa mafanikio na kusimama na mwengine katika kutofaulu ni muhimu tunapotafuta kukua kama watu watakatifu kushikiri ujumbe mtakatifu.

**WAINJILISTI WALIOJITOLEA**
Nia ni muhimu katika uinjilisti, lazima tujue kutumia kila fursa za kila siku kushiriki upendo wa mungu. Sio tu kushiriki hadithi ya Yesu lakini kuwalika wale wanaoisikia katika maisha mapya amabyo inatoa na kuwasaidia kwa kuwanzisha katika safarti ya uanafunzi.

**WAINJILISTI WA KUHAMASISHA**
Tunaposhikiriki ujumbe wa injikli na ulimwengu unaohitaji lazima pia tuchochee kanisa kufanya vile vile. Uinjilisti ni kazi ya kila mkristo na hivyo kutia moyo au kuhimiza na kuchochea kanisa kwa jukumu hili ni lazima pia iwe jukumu la kila mwinjilisti.

**SWALI:** Zingatia sifa hivi tano za msingi, je! unatambua wapi nguvu na udhaifu wako katika kila sehemu?

## MAJADILIANO (DAKIKA 15)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadaliano:

- Ni nini jukumu letu katiuka uinjilisti? na jukumu la mungu katika uinjilisti ni nini?
- Je! tutahakikishaje kuwa sisi ni wainjilisti halisi na waabudu halisi?
- Je! unatarajia kukua aje katika miezi zijazo kupitia kikundi hiki cha Advance?

> "Ikiwa watenda dhambi watahukumiwa, angalau wacha waruke kuzimu juu ya miili yetu. Na ikiwa wataangamia, wacha waangamie na mikono yetu ikiwa kwenye magoti yao na kuwashinikiza wa baki, ikiwa jehenamu lazima ijazwe, angalau iwe imejazwa kwenye vinywa vietu. Na mtu yeyoye yule asiendee kule bila kuonywa na bila kuombewa."
>
> **CHARLES SPURGEON**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Buni ufafanuzi wako wa kibiblia wa uinjilisti (ikiwezekana na marejeleo ya maandiko) na ulete kwenye kikundi wakati ujao kwa majadialiano na kukosoa (kusoma vitabu vilivyopendekezwa juu ya uinjilisti vinaweza kusaidia!

## MAOMBI

Mshukuru mungu kwa injili yake ya kushangaza mshukuru kwamba amekuchagua kuwa sehemu ya kazi yake ya kuokoa ulimwengu. Omba ili awape nguvu ya kuwa wajumbe wake kwa maneno na matendo munapomwabudu kwa roho na kweli.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

Jaza fomu za uwajibikaji shiriki kwa jozi au kwa vikundi vidogo na muombeane.

## UJUMBE NA TAREHE (DAKIKA 10)

Funga kikao cha kwanza kwa kulliza wenye kil mtu aingie kwenye mfumo wa wa ujumbe amabo hufanya kazi kwa kila mtu kwenye kikundi: mitandao ya kijamii kama whatsaap na facebook messenger zote ni bure na hufanya kazi vizuri, unda kikundi ambacho utakmia kuwasiliana wakati wa vikao, sasisho/ habari za hivi upunde, ombi la maombi, ushuhuda nakdhalika.

Panga mikutano ya kikundi kabla ya wakati na mbele sana zaidi ya kikao kinachofuata (miezi sita mbele ni vizuri ili kila mtu ajitolee kuhudhuria vikao hivyo na kufanya kipaumbele katika sharaja..

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 2:
# UTAMBULISHO WAMWINJILISTI

**katika kikao hiki au mnkutano huu wa pili wa kikundi, tutachunguza utambulisho wa mwinjilisti na vile unahusiana na utambulisho wa mungu mwenyewe na hadithi yake ya injili.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Kitambulisho cha mwinjilisti kimekita mizizi katika utambulisho wa mungu Baba: sisi ni watoto wake wajumbe.

## ASILI YA KIKAO

Katika kilele ya huduma ya Billy Graham, vijana wa kikristo walichochewa kufuata mfano wake na kuwa wahubiri wa habari njema. Zaidi ya miaka ishirini iliyopita kumekuwa na mabadiliko yanayaonekana kwa matakwa ya vijana wa kikristo,ambapo jukumu la mwinjilisti linaonekana kama kilele cha huduma ya kikristo, matarajio ya kawaida kwa vijana wa kikristo sasa leo ni kuwa kiongozi wa ibada, mfanyikazi wa vijana, au ,mchungaji wa kanisa.

Kanisa kwa hakika limefaidika na wanamziki wenye kipaji,watengenezaji filamu na ubunifu mwingine wakitumia vipaji vyao katika ibada ya kibinafsi na ushirika, na mungu ameradhimishwa na kutukuzwa kupitia jitihada za watu hawa waaminifu. Hata hivyo kabla mtu awe mwabudu wa kweli katika roho na kweli (Yohana 4: 23) lazima wawe wamesikia na kuitikia injili (Warumi 1o: 14-17).

Vivyo hivyo jukumu la mchungaji au mwalimu ni muhimu kwa uanafunzi na sio la kutengwa. Lakini mchungaji hatakuwa na wanafunzi wa kufunza ikiwa viti vitabaki vitupu kwa sababu ya ukosefu wa ushiriki wa kimisheni au uinjilisti ulimwenguni.

Kuawaleta watu mahali pa maabudu ya kweli, kunahitaji tuwaeleze injili na kwa kuzingatia hilo hakuna yeyote anapaswa kukwepa jukumu letu la kushiriki habari njema kwa ulimwengu, kwa kushudia Imani yetu katika Yesu kwa watu wote kwa nguvu ya roho(Matendo 1: 8). Biblia inatufundisha kwamba waumini wote wameitwa kufanya kazi ya uinjilisti (Mathayo 28: 19,2 Timotheo 4: 5)

Walakini kuna wale ambao wameitwa haswa kuwa wainjilisti (Waefeso 4: 11), kwa hawa watu kuhubiri injili sio tu ushuhuda wa kila siku lakini ni lengo kuu la maisha yao.

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 20-30)

Chukua muda kujuliana hali, kuhimizana, maoni juu ya fursa na kitu kingine choichote ambacho kitahimiza kikundi, uliza kikundi waeleze ufafanuzi wao wa kibiblia kuhusu uinjilisti (KIKAO CHA KWANZA: MATUMIZI) na wajadili kwa pamoja.

Kwa vikundi vidogo hii unaweza kufanywa kama zoezi zima la kikundi, kwa vikundi vizima unaweza kutaka kuyagawanya katika makundi madogo madogo kwa majadiliano. Unaeza kuchukua fursa hii kueleza sheria za kikundi na jinsi kikundi kinaendeshwa kwa wale ambao walikosa kikao cha kwanza.

## MAOMBI

Patia Bwana muda na uombe juu ya hali yeyote nzuri, chanya, changamoto au jambo lolote lile liloangaziwa wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> “Nakuagiza mbele za mungu na mbele za kristo yesu anayewahukumu waliofariki na na walio hai: kwa kufunuliwa kwake na ufalme wake ; lihubiri neno, uwe tayari wakati ufao na wakati usiokufaa: karipia,kemea,na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana itakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makunfdi makundi kwa kuwa wana masikio ya utafiti. Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli na kuzigeukia hadithio za uwongo. Bali wewe uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa injili, timiliza huduma yako.”
>
> **TIMOTHEO WA 2: 4: 1- 5**

Je! Unamaanisha nini kuitwa mwinjisti? Je! si waumini wote wameitwa kushiriki habari njema na ulimwengu? Agizo kuu la yesu katika mathayo 28 linaonekena kuwa wito kwa wafuasi wake wote kwenda ulimwenguni na kufanya wanafunzi. Lakini tunapatana na kifungu katika Waefeso 4: 11-12 ambacho kinaangazia jukumu maalum la mwinjilisti sawia na la mchungaji,mwalimu, nabii na mitume ambazo zinafaa kutumika kujenga mwili wa Kristo. Pia tunakutana na mtu anayeitwa philipo katika matendo ambaye amepewa jina maalum mwinjilisti (Matendo 21: 8), kwa hivyo tunapaswa kufanya nini juu ya wito wa mwinjilisti, Je! uinjilisti ni kwa kila mtu au kwa watu wachache maalum?

Unaweza kuwa u najua maneno ya Wakorintho wa Pili, mlango wa tano mstari wa kumi na saba ambapo Paulo anazungumzia kuhusu kuwa kiumbe kipya kupitia kristo. Kuna uhakika kuwa umetumia kaya wakati wamahubiri yako. Walakini hatupendi kunuku kifungu chote:

> “hata imekuwa mtu akiwa ndani ya kristo amekuwa ni kiumbe kipya, ya kale yamepoita tazama yamekuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na mungu aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwaa Kristo naye alitupa huduma ya upatanisho. Yaani mungub alikuwa ndani ya kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yakeasiwahesabie makosa yao naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristokan mwamba mungu anasihi kwa vinywa vyetu .twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na mungu’”
>
> **2 WAKORINTHO 5-17**

Mungu yuko katika biashara ya kupatanisha uumbaji na yeye mwenyewe na anataka tuwe mabalozi wa ujumbe wake wa mabadiliko. Hiin siuo tu kwa wainjilkisti ‘’ wataalamu’’ huu ni wito kwa waamini wote. walakini ubalozi huu unaweza kuonekana tifauti sana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Fikiria juu yake hivi: katika timu ya mpira wa kandanda/ kabumbu kila mchezaji nafuata lengo la kushinda mechi, hata hivyo washambuliaji ndio wamepewa jukumu maalum la kufunga mabao. Hii haimaanishi kuwa wachezaji wengine hawawezi na hawatapata kufunga mabao mara kwa mara, lakini kazi msingi ya mshambuliaji katika timu nni kufiunga mabao. Vivyo hivo kama kanisa sote tunaendelea na lengo la kurudishwa kwa ufalme kamili wa mungu, kwa sababu hii sisi sote tuna jukumu la katika kushuhudia na uinjilisti. Lakini kuna wengine ambao wameitwa hasa kutanguliza kuhubiri injili labda kwa gharama ya shughuki zingine. Hawa ni wainjikisti nkama vile filipo ambayer tuansoma juu yake katika (Matendo 21: 8)

Ikiwa baaadhi ya taarifa zifuatazo ni za kweli kwako basi wito wa uinjilisti/mwinjilisti unaweza kuwa juu ya maisha yako:

- Unatamani kuona waliopotea wameokolewa.
- Unashinikizwa kuhubiri injili kwa msimu na nje ya msimu.
- Unavumilia katika majukumu bila kujali shida zioi zinakufuata.

- Hautavunja uadilifu wa ujumbe unaoshiriki bika kujali masikio ya wasikilizaji yanawashwa kwa kupenda kusikia ukisema nini.

- Una nia moja katika kuwafikia waliopotea na ujumbe huu wa kuokoa na kuleta mabadiliko.

- Umesikia maneno ya kinabii yaninenwa juu yako juu ya kuwa mwinjilisti.

- Upo tayari kuenda popote injili ambapo injili itakupeleka.

**SWALI:** Tumia muda kuzungumza kuhusu kauli hizi na kama baadhi aub vitu hivi vyote ni vya ukweli kwako, uliza mtu mmoja kwenye kikundi aelezee jinsi alinyokuja kutambua kuwa/kwamba mungu alimuita kuwa mwinjilisti.

Biblia unatuelezea kuwa mungu hataki mtu yeyote anngamie(2 Petro 2:3-9) mwinjilisti analazimika kwenda kwa ulimwengu akiwa na moyo sawa na Baba. Hatuhubiri kwa sababu ni lazima (kutoka mahali pa wajibu au hofu) tunahubiri kwa sabau mioyo yetu inaambatana babayetu wa mbinguni. Utambulisho wetu haupatikani kwa kuwa mwinjilisti bali kwa kuwa mtoton wa mungu ; tukiwa warithi kupitia injili tunayo hubiri sasa. (Yohana 1:12)

Bila kujali kipaji au wito, hakuna mtu aliye na uwezo wa kujiokoa au kuokoa mtu mwingine yeyote. Tunaweza tu kuwa wajumbe kwa kuwa ni mungu pekee yake ndiye anayeokoa. Anatualika kushiriki katika moyo wake kwa waliopotea tunapokuwa kumjua kikamilifu kama baba yetu wa mbinguni mwenye upendo na kufunua nguvu zake za kuokoa ulimwengu.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! kuna tofauti gani kati ya ushuhuda wa kibinafsi na uinjilisti?

- Je! ikiwa ni wote wanaotarajiwa kufanya kazi ya mwinjilisti, kwanini kuna wale ambao walioitwa kuwa wainjilisti?

- Je! tunawezaje kukuza ndani yetu moyo wa baba kwa waliopotea?

> "Yule ambaye ameitwa na kutengwa kwa ajili ya kazi ya uinjilisti, nikujitiolea muda wake na jitihada moja kwa sababu ya kaziu hii iliyopeananwa na mungu haipaswi kuvurugwa au kachanganyikiwa na kitu chochote ambacho kinaweza kumzuia kutoka kwa hii. Ushawishi wa wengine utaanguka kwa masikio ya viziwi. Ni sauti wazi ya mungu tu itamfanya abadilishe huduma yake."
>
> **BILLY GRAHAM**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Hatushiriki ijnili kwa sabau sisi ni'' wainjilisti'' tunashiriki ijnili kwa sabau tumebadilishwa na upendo wa baba, na pamoja naye tunatamaninuliwengu uweze kumjua/ kumfahamu.

Katika mwezi ujao weka injili ya Marko katika wakati wako wa ibada ya kilasiku na uangalkie mada moja kuu ya Marko- kwamba yesu ni mwana wa mungu, mtumishi ambaye amekuja kufnaya mapenzi ya baba. Unavyisoma na kuisoma ttena injili kwa matazamo huu, omba mungu athibitishe utambulisho wako kulingana na yeye.

## MAOMBI

Toa shukrani kwa mungu ,baba yeti wa mbinguni kwamba hatamani yeyote kuangamia nanamefanya njia ambayo wore wanaweza kuokolewa kupitia imani katika yesu Kristo. Chukua miss kuombeana kwamba mungu ataleta uwazi zaidi kwa wito wall kama mwinjilisti ili apate kutoa fursa zaidi ya kushiriki injili na utakuwa na ujasiri zaidi unapofanya hivyo.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji shirki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 3: UJUMBE WA MWINJILISTI

**Katika kikao hiki tunachunguza ujumbe wa injili yenyewe. Je! injili ni nini? je! tuna uelewa wa kutosha wa ujumbe tunaohubiri ili kuuwasilisha kwa usahihi?**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Ujumbe wa mwinjilisti ni yesu Kristo. Kristo alikuja, Kristo alisulubiwa, Kristo alifufuka na Kristo anarudi.

## ASILI YA KIKAO

Mtume Agustine alitangaza na kusema: **’”umetuumba kwa ajili yako eh! Bwana na mioyobyetu haina utulivu hadi itulie ndani yako’’**

Injili inawahamisha watu kutoka katika kukata tamaa, giza, unyongena udhaifu, kukosa tumaini, na kuwaeka palipo furaha, nuru,upendo na amani.injili inahimiza mioyo isiyotulia kutimizwa na muumbaji wao. lakini la kusikitisha inaonekana kuwa wafuasi wengi wa Kristo wamepoteza Imani kwa nguvu ya ijnili leo. Kuna sababu nyingi ambazo ni kwa nini waumini hawashiriki ijnili na wenzaom sabau hizi ni kama: hofu, hisia za kutoshahili na kutumaini kuwa/ kwamba mtu mwingine atafanya. Yote haya yanachangia. Kiini chake ni kwamba, sababu hizi mahali pamoja: ukosefu wa kutoelewa injili ni nini na ukosefu wa Imani kwa nguvu zake.

Katika Warumi moja Paulo anatangaza kwa ujasiri kwamba: ‘’ kwa maana silonei haya ijnili ‘’ na kisha anaendelea kuhitimu kwa nini ni hivyo; ‘’ kwa sabau ni uweza wa mungu uletao wokovu’’ (WARUMI 1: 16) kuelewa injili kama nguvuya mungu ya kuleta wokovu ni kuelewa kitu kuhusu mungu ni nani, kile alichokifanya na kina maana gani kwa ulimwengu. yote haya yamefungwa katika uhalisi wa Yesu Kristo ni nani. Lakini hii haijatengwa wala sio falsafa ya kufikiria isiyto na umuhimu Zaidi ya ukumbi wa mihadhara au chumba cha mijadala. Kuelewa injili hutasaidia kufikia maswali msingi juu ya uwepo wetu na utambulisho wa mungu aliyetuumba.
Maswali kama:

### JE! MIMI NI NANI?

Kila mtu huuliza swali hili kwa njia moja au nyingine, je! maana ya maisha ni nini?je! kuna kusudi la maisha? je! kitambulishio changu ni nini. Jibu ni kwamba wewe ni mtoto wa mungu, aliyeumbwa na kupendwa na yeye (mungu)

### JE! MUNGU NI NANI?

Kuna dini nyingi sana duaniani/ulimwengunui. Hata ikiwa mungu yupo, tunawezaaje yeye ni na nani na kwamba tunaabudu mungu aliye wa kweli?

Mungu amejitambulisha kupitia uumbaji, kupitia Biblia, kupitia ushuhuda wa wakristo ulimwenguni kote na kupitia yesu kristo. Yeye ndiye muumbaji na mutunzaji wa maisha, mfalme wa ulimweng, baba wa mbinguni, na mwenye upendo ambaye anatamani kurudisha/ kuregesha ubinadamu uliovunjikla na waasi katika uhusiano na yeye mwenyewe.

### JE! YESU KRISTO NI NANI?

Mtu mwenye ushawishi zaidi kwenye historia ya wanadamu. Ni wasomi wachache wa kihistoria walio na shaka kuwa alikuwepo. Lakini alikuwa nani? Mwalimu mwenye busara? Mtu mjanja? Mtu mwenda wazimu? Kwa kweli yeye ndiye anayesema yeye ni; mwaokozi wa ulimwengu mabaye kupitia maisha yake, kifo chake na ufufuo wake amemwezesha mtu kuwa mwana wa mungu.

Wakati aina hii ya maswali yanaweza kuwa mwanzo wa mazungumzo kuhusu injili, hyasababishi ufahamu Zaidi au wakutosha kuhusu maana ya injili bali ni kiunganishi

ambacho tuanweza kutumia kujenga uhusiano. Na kwa hivyo ni lazima kuchambua kwa ndani/ kina Zaidi maandiko ili kuhakikisha kwamba kupitia swali hili tunaweza kuelekeza kwa injili ya kuvutia na yenye nguvu ya yesu Kristo.

# WAKATI WA MAPATANISHO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 15-25)

*Chukua muda ili iuweza klujuliana hali kuhimizana na maoni kuhusu fursa ya uinjilisti na kitu kingine ambacho kitahiza kikundi. Uliza kikundi waeze kujadaili na kutoa maoni yao kuhusu safari yao katika injili ya Marko mwezi uliopita (kikao cha pili> matumizi) tumia hii kama nafasi ya kueleza na kuthibitisha utambulisho wa mwinjilisti kwa kutumia mfano wa yesu kama mtumishi wa mungu.*

## MAOMBI

Patia Bwana muda na uombe juu ya hali yeyote nzuri, chanya, changamoto au jambo lolote lile liloangaziwa wakati wa mapatanisho.

## MAFUNDISHO (DAKIKA 25-35)

Tumia nyenza zifuatazo za mafundisho kwa njia yako mwenyew, ama kwa kuisoma neno kwa neo, au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> ‘’ basi ndungu zangu, mimi nilipokuka kwenu, sikuja niwahubiri siri ya mungu kwa ufasafa wa waneno wala kwa hekiuma ,maana niliazimu nisijue neno lolote kwenu ila yesu kristo, naye amesulubiwa’’
>
> **1 WAKORITHO 2: 1-2**

Paulo anaonyesha kujitolea kwake kwa ukweli na nguvu ya nguvu ya hadithi ya yesu kwa kutangaz: “ niliamua wakati nipokuwa nanyi kutojua chochote isipokuwa yesu kr=risto, naye amesulibiwa.” Huu ndio moyo wa ijnili, kwamba mwenyewe aliingia kwenywe fujo za ulimwengu wetu katika nafsi ya yesu kristo, aliishi maisha kamili na kuchukua kifo tulichostahimili na kufufuka tena baada ya siku tatu. Alivunja laana ya kifo mara moja na kwa wote. Wokovu na maisha ya kweli yanapatikan kupitia kwake pekee. Tumashiriki ukweli hu sio tu kuleta mawazo yaliobadilika bali kuleta maisha mapya- mabadiliko amabayo yanamweza kupatikani tukatika yesu kristo.

> **SWALI**: Mengi katika kikao hiki yatachunguza ijnili ni nini, tumia sehemu zifuataz (zinapatikan katika Viambatisho) kuzua mjadala juu ya kile tunachaomini injili kuwa.

**MAFUNDISHO YA INJILI (UKURASA WA 80)**
Mpangilio wa injili.

**SIMULIZI YA INJILI (UKURASA WA 81)**
Kwa ujumla injili hiyo hiyo imewasilishwa hapa kwa njia ya kimfumo Zaidi, lakini hapa kuna mpakazo Zaidi juu ya maelezo ya hadithi ambayo husomeka kama hadithi.

**MFANO WA MAZUNGUMZO YA IJNJILI YA VIJANA MFANO WA HOJA NNE, MIVIRINGO MITATU (UKURASA 82)**
Mifano hii inaweza kutumiwa kukosoa njia maalum ya uwasilishaji wa ijnili chagua moja au Zaidi ukiwa na muda na angalia jinsi injili inaelezewa, ni nini kinafanya kazi vizuri na nini kinaklosekana?

Frank Turek anasema hivi: “ unachowashawishi watoto nacho, ndicho unacho waelekeza kwacho, ukiwashawishi na mhemko unawaelekeza kwa mhemko, ikiwa ujumbe wetu wa ijnili umemwagiwa maji na ni njia moja tu tunayotumia kujaribu kuvutia moyo wa msikilizaji, tunaweza kuona mikono mingi imeinuliwa “ikiitikia” ujumbe, lakini ni nini haswa wameitikia (ujumbe au njia tuliotumia kuwasilisha ujumbe huo)

Ujumbe wa ijnili huleta maoni yenye changamoto nyingi sana; unaelezea sisi wote kama “ wenye dhambi” na inadai kuwa sisi ni viumbe wenye unyionge na udhaifu/ viumbe vilivyovunjika na tunastahili kifo. Habari njema

ya injili ni njema kwasababu ni kwa ajili ya hali ya kibinadamu iliyo mbaya Zaidi.

Dhana yetu ya jinsi mungu ni mungu mwenye neema inategemea jinsi tunavyofikiria dhambi yetu ni shida. Watu wanapambana na wazo la mungu anahukumu kwa ajili yay a dhambi zetu na mawazo mungu mwenye upendo ambaye hupeleka watu kuzimu. Ni rahisi kujaribu kutupilia mbali au kupuuza mambo haya ya injili, lakini hii haifanya. Mwinjilisti anajukumu la kuvungua kwa wazi shida ya dhambi ili nguvu ya mslaba na tumaini la ufufuo lieleweke kwa kweli-neema isiyostahiliwa ya mungu ilitolewa kwa upendo wa watoto wake na tumaini la pekee kwa binadamu.

Dhambi ni shida kubwa inayotatuliwa na mungu mkuu, na kulimwagalia maji jambo moja kati ya haya na lulifanya lisiwe la maana ni kudhoofisha mtazamo wetu wa linguine. Na kwa hivyo ni lazima tujitolee kwa ukweli bila kujali ni chgangamoto gani unaonekana.

Sehemu ingine amabyo ni rahasi kuikosa ni wazo kwamba tupaswa kufa kwa ubinafsi wetu, kuchukua msalaba wa maisha yanafafanuliwa na maisha ya kujitolea mara nyingi hupuuzwa na badala yake ujumbe wa " mungu atakufanya iwe na furaha" unapewa kipaumbele.

Matt Chandlier anasema hivi: " nguvu ya kiroho katika ijnili inakataliwa wakati tunaongeza au kurekebisha injili na kuifanya kutokuwa ijnili tena. Tunapotilia shaka kuwa ujumbe pekee yake ni nguvu ya mungu ya wokovu, tunaanza kuongeza, kutoa au kubadilisha tukiamini nguvu zetu za ushawishi au uwasilishaji"

Ni lazima tuwasilishe ijnili kamili na kwa uwazi, kwani injili yenye upungufu itasababisha wakristo wenye upungufu.

Kuweka kipaumbele masomo ya biblia ya kila siku ni muhimu sana kwa kila muumini, lakini haswa kwale wanaotangaza ukweli wake mara kwa mara. Je! Tunaawezaje kudai kuwa na ufunuo kutoka kwa maandiko ikiwa haturuhusu ya maandiko kulisha maisha yetu kila siku?

Tumeitwa sio tu kuwa wainjilisti bali wainjilisti wa kufundisha biblia

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadialiano:

- Je! ungeelezeaje uelevu / uelewa wako mwenywe juu ya ukweli wa injili?
- Je! kuna changamoto gani za kuelezea injili leo?
- Je! tunawezaje kujenga uhusiano wa wasikilizaji wa kisasa?
- Je! inammanisha nini kuwa wainjilisti wanaofundisha Biblia?

> "injili ni damu ya uhai ya ukristo na unatoa msingi wa kupoinga utamaduni. Kwani tunapoiaminiinjili ya klweli, tunaanza kugundua kuwa ijnili haiwalazimishi wakristo nkukabiliana na maswala kijamii katika unayowazunguka tu bali pia ijnili inaleta makabiliano na tamaduni zinazotuzunguka na zilizo ndani yetu."
>
> **DAVID PLATT**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Himiza kila mshiriki wa kikundi kuanza au kuendelea na mpango wa kila siku wa kusoma Biblia kwa kutumia YOU VERSION ama maandishi mengine ya usomaji wa Biblia. Uhusiano wetu na maandiko ni muhimu sana ikiwa tutakua kama wafuasi na kuelewa injili kwa kina ili tuweze kuishiki kwa urahisi.

Ukitumia habari kuhusu injili katika kijitabu hiki na Biblia yako, toa maelezo mafupi (matatu au tano) ya ijnili na kuunga mkono kwa kutumia mistari za biblia ambazo unaweza kujadili na kikundi wakati mwingine. Maelezo haya yatakosolewa kwa teolojia yao na kwa ufanisi wao kama kipande cha mawasiliano.

## MAOMBI

Mshukuru yesu kuwa alikuja na kuishi maisha kamilifu, kwamab alichukua nafasi yako juu ya msalaba, kwamba kwa njia ya ufufuo wake tunaweza kushiriki katika maisha mapya. Mwambie akusaidie umutumaini na kukua katika upendo wake. Mwambie akusaidie kuelewa neno

lake kikamilifu, kujua injili yake kwa kina zaidi, na kuwa na uwezo wa kushiriki injili hii kwa urahisi na kwa kweli kwa wale ambao walio karibu nawe. Omba kuwa utakuwa utaandaliwa kuwa mwaminifu kwa fursa hizo unapotumia muda katika neno lake na mbele zake

## UWAJIBIKAJIO (DAKIKA 15)

Jaza fomu za uwajibikaji, shiriki katyika jozi na makundi madogo, kisha muombeane.

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 4:
# JUKUMU LA MWINJILISTI

**Je! kuhuburi kuna umuhimu gani kwa mwinjisti? kikao hiki ni furs aya chunguza mada hiui kibiblia na kuhimiza kila mmoja mmoja kukuza na kunoa stadi zetu bza mawasiliano na mahubiri kwa kutii nguvu za roho mtakatifu kwa kazi hii kabisa.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Jukumu la mwinjilisti ni kuitangaza injili kama ilivyofunuliwa kupitia neno takatifu la mungu kwa nguvu ya roho.

## ASILI YA KIKAO

Kulingana na mila mtakatifu Francis wa ASSISI aliwahi kusema: '' hubiri ijnili wakati wote na ikiwezekana/ ikibidi tumia maneno''

Nukuu hii ni maarufu kwa kuonyesha umuhimui wa kuishi maisha yaliyowekwa na injili, ila tu kuna shinda mbili hapa, kwanza hakuna ushahidi kwa mtakatifu Francis aliyasema maneno haya angalau kuyaandika.

Pili nukuu hii haishikilii kama taarifa, wakati ni sawa kwamba maisha yetu yanafaa yaonyeshe habari njema juu ya ufalme sawa na maneno yetu, kuhubiri injili ni kwa ufafanuzi injili ni mchakato unaotumia maneno. Sentensi hii inaweza kurekebishwa na kusema hivi: '' hubiri ijnili kila wakati, na lkwa sababu ni muhimu, tumia maneno''

Maneno **''hubiri**'' na ''tanganza'' hubeba kiunga kisichoweza kutengenishwana neno simuliz. Baada ya yote unaweza kushi maisha makanilifu ya ''injili''. Lakini imkiwa hautaelezea tumaini uliulo nalo kwa yesu basi ulimwengu utajuaje sababu ya wewe kuishi maisha yako hivo?

'' kukaa kimya na kuwacha wengine watafsiri matendo yetu ni makosa, mungu mwenywe hakufanya hivi, hatua muhimu hautua ya ukombozi wa mungu katika historia inaambatan na matamko."

**WILL METZGER**

Kuhubiri ilikuwa muhimu katika kueneza ijnili kama ilivyoandikwa katika Agano Mpya (Matendo 2:12), lakini kuna wale wanaamini kuwa ijnili ni mtindo wa zamani sio tena njia bora ya kuwasiliana injili kwa ulimwengu.

Hakikaa tunataka kuwa wabunifu katika mahuburi yetu na kuhusisha katika mawasiliano yetu (labda tuchunguze njia zingine za mawasiliano kama vile utengenezaji filamu, utunzi wa nyimbo/ mashairi) laikini bibllia inatulazimu kushikilia pa kuu kuhubiri kama sehemu kuu ya jukumu la kushukiri ijnili. (1 wakorintho1:21. 2 timotheo 4: 1-2).

Kwa mwinjilisti injili ni kiini cha kazi mabayo wameitwa, mahubiri haya ni lazima yafafanue habari njema ya yesu kristo kwa njia ambao wasikizaji wanaweza kuelewa na pia uwape mwaliko wa kujibia yale waliosikia kwa kumchagua kumfuata yesu (MARKO 1: 17, LUKA 9: 23). Walakini maneno pekke yake hayatafanya. Maneno yaliyosemwa kutoka kwa kutoka kwa maisha yasiyo matakatifu yatakuwa ya uwongo na ya unafiki, maneno yaliyojitenga na nguvu ya roho ya mungu hayana uwezo wa kuleta wokovu.

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili kujuliana hali, kuhimizana, maoni ju ya fursa ni kitui chochote kile

kitahimiza kikundi. Uliza mtu mmoja au wawili katika kikundi wajitolee na wawasilishe uwasilishaji wao kuhusu injili (KIKAO CHA TATU: MATUMIZI) Toa maoni kuhusu uwasilishaji wao na kumbuka kuwa mzuri.

## MAOMBI

Chukua muda ilikuweza kuomba, na uombe kuhusu hali yoyote ile nzuri au chanya, au jambo lolote lililoangaziwa wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> "Kwa sababu hii umkiri yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana,na kuamini mopyoni mwako yakuwa mungu alimfufua katiaka wafu utaokoka, kwa kuwa kila atayeliita jina la Bwana ataokoka, basi wamwiteje yeye wasiomuamini?, tena wamwaminije yeye wasiyemsikia?, tena wamsikieje pasipo mahubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? kama ilivyoandikwa ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema"
>
> **WARUMI 10: 9, 13-15**

Kuna mazungumzo wengi juu ya tangazo katika biblia. Tim Keller anatambua maneno angalau thelathini na tatu ya kigiriki(kiyuyani) tunayotafsiri kama '' kuhubiri '' au '' kutangaza'' katika kifungu hiki cha warumi tunapata Paulo akilitumia neno hilo akimaanisha kushikiri habari njema. Kulingana na Paulo kuhubiri ni muhimu sana kwake, kwani anamueleza Timotheo aweke kuhubiri mbele (2 timotheo 4: 1-2)

Tunaona pia wakati wa pentekoste jinsi mungu anavyoamua kuitumia. Maelfu waliokolewa sio tu kwa kutana na ishara na maajabu yasiyo ya kawaida (ndimi za moto, kunena kwa lugha nyingine), lakini kwa kusikia tangazo la Petro lilijaa roho.

Lakini kuhubiri ni changamoto kwa sasa(leo) na kuna wengi wasioamini kuwa kuhubiri injili ndio njia bora ambayo ulimwengu unaweza kupokea habari njema. Ushiriki wa kibanafsi, uinjilisti wa kirafiki na miradi ya vitendo vya kijamii, imekuwa njia maarafu ya kushiriki imani kama kile kinachoonekana kama njia isiyo na mapingamizi. Walakini hatuwezi kukana kuwa kuna nguvu katika kuhubiri, na neno la kiyuyani (kigiriki) tunapopata neno '' uinjilisti'' kimsingi inammanisha '' kutangaza habari jema '', ambayo asili yake ni shughuli ya kuzungumza. Ikiwa hatuwezi kamwe kutoa uffanuzi au kueleza jinis tunavyoishi au tumaini tunalo, vi vipi mtu mwingine yeyote atajua uwekli wa Yesu Kristo (1 Petro 3:15)

> **SWALI:** Ikiwa tunajua kwamba kuhubiri ni muhimu kwa jukumu la mwinjilisti. Je! tutahakikishaje kwamba ujumbe wa injili unawasilishwa wazi kwa kutosha, kwa wasikizaji kuilewa na kuwa na nafasi ya kujibu kwa yale ambayo wamesikia?

Kujua hadhira yetu na mazingara yao ni muhimu kwani inatusaidia kufikiria kwa uangalifu juu ya vielezo na sehemu za utapatanisho ambazo zinaweza kuwasaidia kushiriki na kuelewa kile tunachoshiriki. Ikiwa tunahuburi ijnili kwa kikundi cha vijana, tunaweza kutumia maneno tofauti kulingana na wakati tunaposhiriki injili na kikundi cha wazee., ujumbe wa injili wenywewe haubadiliki, lakini jinsi tunavyoilezea na vielezo tunavyotumia na marejeo ya kitamaduni tunayoitumia yanaweza kulenga watu walio mbele zetu. Kile tunachohubiri hakibadiliki bali jinsi tunavyohuburi hubadiliak.

Hii ndio sababu mwijilisti lazima atumue muda kujiandaa. Ikiwa tunategemea mazungumzo yale yale ya zamani ya injili kila wakati tunapoinuka kuhubiori, kuna uwezekano wakuwa wahubiri wavivu na wabovu.

Kwanza kabisa tunapaswa kukaribia maandalizi yetu na maombi, kumwomba zungumze kupitia sisi kwa roho yake na tupe maneno. Tunapaswa pia kuandaa mazungumzo ambayo huzingatia wasikilizaji ambao watasikiza ujumbe wetu.

> **SWALI:** Angalia vidokezo vifuatavyo vya kuhubiri injili na ffikiria mifano kadhaa katika huduma yako.

Tunapaswa kuhubiri:

**KWA URAHISI:**
uwazi ni muhimu katika mawasiliano mazuri. Kuelezea kwa urahisi ni lazima kwa tuelewe ujumbe wetu kwa undani.

**KWA UJASIRI:**
ni lazima tuhuburi kwa kusadika na kwa ujasiri au kuamini katika ukweli wa ujumbe wetu.

**KWA KIROHO:**
li mioyo iliyokufa ikpokee ujumbe wetu wa kuishi, roho ya mungu lazima ifanye kazi. Kwa hivyo mahubiri yetu lazima yawe chini ya nguvu za roho kwa kazi hiyo.

**KWA KIPEKEE:**
Ni lazima kristo awakilishwe kam wa kipekee mbele ya wengine wote na abaki katikati ya mahubiri yetu.

**KWA UPENDO:**
hutushindi watu kwa mawazo yetu wenywe na hekima lakini kwa ukweli pekee wa yesu Kristo. Tunapaswa kuhubiri kwa unyenyekevu na kumheshimu yule tunayeshiriki(mungu) na kwa huruma kwa wale tunaowashirikisha (watoto wake)

**KWA UBINAFSI:**
tunaweza kuonyesha ukweli wa injili kwa kushiriki juu ya athari zake katika maisha yetu wenyewe na kujenga daraja kwa wasikilizaji na hali yao.

Hata kama hivi bvidokezo vinaweza kuwa vya manufaa, ni muhimu kukumbuka kuwa hakuna kiwango cha mazungumzo ya ujuzi yataleta mtu katika ufalme wa mungu.

> "ni jambo moja kujifunza mbinu na ufundi wa kuhubiri, ni jambo lingine kabisa kuhubiri mahuburi ambayo yatafungua pazia na kufanya vizuizi vinavyoficha uso wangu kuanguka."
>
> **DAVID WATSON**

Ni lazima mahuburi yetu yatoe nafasi kwa roho mtakatifu kusonga kwa nguvu. Ingawa ni muhimu kufikiria kwa makini kuhusu jinsi tunavyowasilisha injili, hatimaye tunatafuta mungu kuchukua maneno yetu na kuzalisha miujiza wa maisha mapya. katika kikao awali tuliangalia kujitolea kwa Paulo kujua na kuhubiri hadithi ya mungu katika Wakoritho 1:2. Katika mistari unayofuata, Paulo anaendelea kushriki/kuelezea kujitolea kwake kutangaza hadithi ya Yesu kwa nguvu ya roho, ili imani mpya itulie juu ya mungu badala ya sababu ya kibinadamu:

> '' na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu bali kwa dalili za nguvu za roho za nguvu. Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvui za mungu''
>
> **1 WAKORITHO 1: 2, 3-5**

Tunatamani kumuabudu mungu kwa roho na kwa ukweli (YOHANNA 4: 23) na uinjilisti wetu haupaswi kuwa tofauti, tunatangaza uweli wake kwa nguvu ya rohho kama waabudu, kutoa ushuhuda kwa yulke tunaye abudu ili wangine waweze kumuabudu.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Pitia maswali yafuatayo au nukku la majadiliano.

- Je! kuhubiri bado ni kitu cha muhimu katika maisha ya sasa?
- Je! tunaweza kufanya nini ili kuwa wahubiri wa injili walio gobea katika uliwmengu tofauti wenye uhitaji?
- Je! nguvu zakio na udhaifu wako ni nini kama mhubiri au anayewasiliana?
- Je! unajiandaa aje kwa ajili ya kuwasilisha injili?

> "tofauti kati ya mahuburi mazuri na mahubiri makuu iko katika kazi ya rorho mtakatifu, inafaa kufanya kazi tunayohitaji kufanya ili mawasiliano yetu yawe mazuri na kumwachia mungu jinsi na mara ngapi yeye itaifanya kuwa kuu kwa msikilizaji'."
>
> **TIM KELLER**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Tafuta videyo fupi kwenye mtandao (YOUTUBE) ya mhubiri injili ambaye unaweza kumkosoa kwa mtindo na yaliyomo uliza kikundi kutazama videyo hiyo fupi kati ya kikao na wawe tayari kujadili wakati ujao.

## MAOMBI

Omba kwa pamoja roho ya mungu ifanye kazi kupitia kwa sadaka ya mawasiliano kwa unyenyekevu. Shukuru mungu amechagua kukufanya msemaji wa ujumbe wake, mwambie akusaidie kusihi injili kwa kweli ili maneno kutoka lwa midomo/vinywa vyenu hayatenganishwi na hali ya mioyo yao kuwapeleka mahali pa ufununuo ambapo wanaweza kuchagua kumtegemea .

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

Jaza fomu za uwajibikaji, shiriki kwenye jozi au kivundi vidogo kisha muombeane.

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 5:
# NGUVU YA MWINJILISTI

**Kama wainjilisti tunatamani kuona mioyo uliyokufa kiroho ikifufuka. Kikao hiki kinachunguza maana ya kuwezeshwa kiroho kupitia maombi, ikituongoza kwenye uamsho halisi moyoni mwetu ambao tunaweza kuutolea ulimwengu.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Sala/ maombi ndio msingi wa uinjilisti na huweka nguvu mahali/pahali nguvu inafaa kuwa na sio katika jitihada za binadamu lakini mikononi mwa mungu.

## ASILI YA KIKAO

Mhubiri wa Kipesbyteria na mmishonari Arthur Tappan Pearson alifanya uthibitisho hu wa kushangaza: "Hakujawahi kuwa na uamsho wa kiroho katika nchi yeyote au eneeo ambao haukuanza na sala/ maombi ya umoja''

Itakuwa ni vugumu sana kupata mfano unaopingana na taarifa hii yake, inaelezea agizo la mungu kwa watu wake katika maandiko yote na ahadi yake ile kitachofuata kuchukua mfano mmoja wakati wa utawala wa mfalme Selemani mungu  anazungumza na Waisraeli waasi na kuwapa tumaini wakati wa uasi wao na matokeo mabaya ambayo yanaweza kuepukika:

> "...ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha na kuomba, na kufatuta uso0 wangu, na kuziacha njia zao mbaya: basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi zao na kuiponya nchi yao."
>
> **MAMBO YA NYAKATI 2:7-14**

Vuvyo hivyo injili ni fursa ya kuachikia kwa unyenyekevu utawala juu ya maisha yetu wenyewe, kutii kristo kukiri kwamba yesu ndiye bwana na kumruhusu kuleta uponyaji na maisha mapya. Tunahama kutoka kwenye uasi (dhambi zetu) na kuelekea kwa ufunuo (wa ukweli wa mungu), kutubu (imani katika yesu) kwa uamsho (mabadiliko ambayo hutoa mabadiliko kwa wengine)

Neno'' kugeuka'' ilivyotumika katika Mambo ya Nyakati mbili, ni neno lile tunalotafsiri katika Agano Jipya kama '' Kutubu''. Yesu alianza huduma yake ya kuhubiri na wito wa kufanya hivyo (MARKO 1:13)

Tatizo la waisraeli katika hadithi hii ni sawa na tatizo letu sasa/leo- sisi kwa mara nyingi hugeukia miungu mingine (wakiwemo sisi wenyewe), katika jaribio la kujaribu ku amri hatima yetu. Kutotii huku kunaweza kusababisha kifo, kuvunjika na machafuko. Mungu amekuwa akituita turudi kwake kutoka wakati tulimpa kisogo. Injili inaonyesha kwamba licha ya uasi wetu, tumaini linapatikana katika neema ya mungu na majibu yetu kwake kwa unyenyekevu.

Kumsihi hakimu kwa kawaida hujumuisha ombi la kutokuwa na hatia kwa matumaini ya kutohukumiwa, lakini hapa tunaambiwa tuiname mbele ya hakimu wa milele na tukubali hatia yetu-hapo tu ndio basi tunaweza kusamehewa. Haki hudai adhabu juu ya hatia yetu sababu ya ukweli wa ukweli wa uasi wetu dhidi ya mfalme mtakatifu, lakini mungu badala yake anatupa msamaha kupitia haki kamili ya msalaba. Badala ya kifo tunapewa uponyaji, marejesho na maisha. Mungu hufufua wanyenyekevu.

Mfano mwingine wa nguvu ya maombi / sala ya umoja (na mungu na kila mmoja) kwa uamsho/ufufuohuaotikan katika hadithi ya Ayubu, sionwakati ule anapata mtazamo mzito kutoka kwa mungu, lakini wakati yeye kwa utiifu anwaombea marafiki amabao walikuwa sehemu ya shida ya kuvuruja maoni na mtazamo wake. Ayubu anayainuwa macho yake kutoka kwa hali

yake na kwa neema kuwaombea wageni (ambao wamemkosea) na anarudishiwa.

Uamsho huanza na mtu mmoja kuchagua anapochagua kutii baba yao wa mbinguni akiitangaza utii wao kwa ufalme wa amani. Inachukua mtu mmoja kutangaza kwmaba yesu ndiye Bwana kwa maneo na kwa matendo, kutegemea roho mtakatifu kuwapa nguvu ya kuzaliwa tena.

Kwa neema ya mungu uamsho huanza na sisi, na kwa neema hiyo hiyo uamsho unaweza kutokea pahali/mahali popote ambapo watu waliokuwa waasi wanaungana kwa unyenyeku kuita/ kuomba nguvu za mungu kuponya nchi/ardhi.

# MWONGO WA KIKAO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 15-25)

Chukuamuda kujukiana hali kuhimaza au maoni kuhusu fursa, jambo lolote litakalo himiza kikundi. Chukua muda huu kuzungumza na kujadili juu ya ile video fupi ya mahubiri (kikao cha nne: matumizi). Ni niini amabacho waliona niche manufaa na kisicho cha manufaa? Nini ambacho wamejifunza katoka kwa mfano ambacho kitawasaidia kukuwa kama watangazi wa habari njema. Epuka kuwa mkosaji sana na kutoa maoni tu ikiwa unapenda au hupendi mtindo wa kuhubiri, badala yake chunguza kwa kina zaidi yaliyomo.

Je! Maelezo haya yalifanikiwa kueleza injili?

Je! Ujumbe uliowasilishwa ulikuwa ujumbe ulio daa kwa handira?

## MAOMBI

Patia mungu muda na uombee juu ya jambo lolote ile chungu au changamoto au jambo lolote lililo angaziwa wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> ‘’ Basi kabla ya mambo yote nataka dua, na sala na maombezi nashukrani zifanyike kwa ajilli ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha yenye utulivui na Amani katika utauwa wotena ustahivu. Hili ni zuri nalo lakubalika mbele za mungu mwokozi wetu, ambaye hutaka watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli’’
>
> **1TIMOTHEO 2: 1-4**

Katika barua yake ya kwanza kwa Timotheo Paulo anampa maaagizo wazi kwa maisha ya kuabudu ya kanisa la Efeso. Paulo anamwambia atangulize wakati wa maombi na maombezi kwa watu wote, kwa sababu inamoendeza mungu na inampendeza mungu kwa sababu anataka watu wake wote wajue Amani ya ufalme wake. Maombi ni njia mab ayi tunamwita mungu afanye kiule yeye tu anaweza kukifanya- kuleta Amani katika machafuko na kuleta maisha kutoka kwa kifo.

Sala/ maombi ndio msingi wa uinjilisti na huweka nguvu pale amabapo nguvu inafaa-sio katika jitihada za binadamu lakini mikononi mwa mungu.

> **EDMUND P. CLOWNEY ANAANDIKA NA KUSEMA**
>
> “Biblia ni neno la mungu, hadithi yake na kazi yake, katika nkurudisha wanaume na wanawake waasi kwake. Haisemi juu ya mwanadamu anayetafuta mungu aliyepotea bali juu ya mungu anayetafuta waliopotea. Biblia haiwasilishi Sanaa ya maombi; inaonyesha mungu wa maombi, mungu ambaye huita kabal hatujajibu na kujibu kabala hatujaita”
>
> **ISAYA 65:24**

Baba mwanzilishi wa umoja wa mataifa wa Amerika Benjamin Franklin aliwahi kusema:” kushindwa kujiandaa ni kujiandaa kushindwa”

Tunapaswa kuandaa mioyo yetu kwa uinjilisti, uwasilishaji na maombi kwa mungu. Tunaweza kuyaandika maneno haya vipya hivi:

> "Kwa kushindwa kujiandaa kwa uinjilisti kupitia maombi, tunajiandaa kushindwa katika uinjilisti."

Hata kwa maombi maaminifu na ujumbe wa injili wenye nguvu ya kiroho, bado watu wanaweza kuchagua kukataa injili. Laikini nguvubya wokovu ni ya mungu pekee, na tunaweza kumtumainia mungu kufanya kazi kupitia maombi yetu hata wakati hatuoni matokeo tarajiwa wakati huo (WAEFESO 6: 18-20). Matokeo ya unjilisti nyako mikononi ya yule anayesikia ujumbe wetu na mungu mwenyewe. Kwa hivyo kufaulku na kutofaulku katika uinjilisti hakupimwi na watu wangaoi wameokolewa, lakini kwa utii wetu na kufanya kile ambacho mungu anatuuliza- kuomba na kutangaza.

Msingi wa msukumo wetu wa kuomba ni kwamba mungu anatuamuru kufanya hivo. Walakini msukumo huu unapswa kukomaa kutokana kuiitikia amri rahisi ya mungu wakati tunakua katika uhusiano na baba yetu wa mbinguni, kwamab tungetamani kwa upndo kumtukuza na kutafuta wema wake na Baraka kwa maisha yetu wenyewe na kwa wale tunaombea, tunagundua dhamira ya mungu kwa uwazi tunavyomjua kikamilifu. Tunapoomba ndivyo tunavyomjua mungu Zaidi, tunanvyojua mungu Zaidi, ndivyo tunatamani kuomba ili mapenzi yake yatimizwe duniani kama mbinguni.

Kwa hivyo hali ya maisha yetu na maombi ikoje? Kwa engine sala/maombi huja kwa kawaida, kwa wengine ianchukua juhudu zadi, wahubiri pia wanapaswa kujiuliza swali hili ili waweze kujitathmini: je! Ninaona ni rahis kuomba au kuhubiri? Ni mara ngapi ungeendelea kuhubiri kwa furaha kuliko muda uliopewa wa mahubiri? Ni mara ngapi unaendelea kuomba Zaidi ya mipika ya muda wako wa kuomba wa kawaida?

Ikiwa tunatak kuwa wainjilisti wenye ufanisi wa kibiblia, tuahitaji kuwa watu waombezi, iwe inakuja kwa kawaida au la. Urefu wa maombi yetu haijalishi lakini ukweli ndio muhimu. Tunapoendelea kumwomba Bwana Mungu kwa dhati, kwa kazi yake ya kubadilisha katika maisha yetu nay a wengine, tunaona kuwa uwezo wetu wa kutumia muda mrefu mbele yake na wakati huu utamheshimu itakuwa nzuri kwetu na Baraka kwa wengine.

**SWALI:** Mafundisho wafupi ya westminister yanaelezea maombi/sala kama "kutoa matakwa yetu kwa mungu, kwa mambo yanayokubaliwa na mapenzi yake, kwa jina la Kristo na ungamo la dhambi na kutambua shukrani za rehema zake" je! Maelezo haya yanaumbaje uelewa wako wa sala/ maombi haswa katika uhusiano na uninjilisti?

Zaidi ya kujitolea kuombea wengine kama sehemu ya uinjilsti wetu, tunaweza kuelewa na kutumia maombi kwa njia tatu tunajiandaa kushiriki injili.

- Kwanza kama njia ambayo sisi wainjilisti tunaweza kukua katika ukomavu kama mtoto wa mungu na kama mwanafunzi mtiifu wa yesu Kristo.
- Pili: kama njia ambao nguvu ya mungu inaweza kuleta fursa za kushuhudia ka kufanya kazi kupitia sisina kubadilisha uinjilsiti wetu kutoka kwa kuuza tu Imani ya kikristo hadi kuchochea mioyo kutoka kifo hadi uzimani (WAKOLOSAI 6: 18)
- Tatu kama njia ambayo yunaweza kuwa na silaha za kiroho kutukinga dhidi ya mashambulizi ya adui tunapoingia katika mstari mbele wa vita vya kiroho(WAEFESO 6:18)

Kama vile Paulo alivyofanya na Timotheo, wacha tuhimize na kutiana moyo, tuwe waombezi kwa wote, na kwamba itampendeza mungu ikiwa tutajitiisha kwa nguvu zake, kwa matumaini kwamab ulimwengu ungejua na kujitiisha kwa uwweli unaokoa.

## MAJADILIANO (DAKIKA 10)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano.

- Je! una desturi na nidhamu gani za maombii kabla ya kuhubiri na kushiriki na nafasi maalum ya ushuhuda?

- Je! unatumia maombi katika kazi yako ya uinjilisti? ikiwa ni hivyo elezea vipi?

- Unaelewaje na unashughulikiaje swala la maombi/sala usiyojibiwa na jinsi gani unaweza kumsaidia mtu kuelewa wazi hili ikiwa utaulizwa wakati kushiriki imani yako nao?

> "uamusho unaokuja lazima uanze na uamsho mkubwa wa maombi, chumbani huku malngio ukiwa umefungwa, ndipo sauti ya wingi wa mvua husikika kwanza. Ongezeko la maombi ya siri itakuwa ya baraka na wahudumu itakuwa kitambulisho hakika ya baraka."
>
> **ANDREW MURRAY**

## MAOMBI (DAKIKA 20-30)

Chukua muda wa ziada kwa maombi katika kikao hiki, ukiombo katika njia tau tofauti, tumia muda huu kuombeana, ombeni kwamba mungu atatusaidia kuwa watu wanyenyekevu, ambao wanakua kila siku katika uhusiano wako na yeye.

Tumia muda huu kuombea jamii yako, mji au jiji, ombea wale waliopotea waokolewena muombe mungu aponye ardhi yetu (kwa jumla: mungu, nipe nafasi ya kushiriki leo ; mungu, chochea mioyo kwa maisha leo)

Tumia wakati huu pia kujiombea, omba ukuandee na sillaha kamili ya mungu unapoekelea katika mstari wa mbele.

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Andika orodha ya marafiki watano, wana familia wenzako au hata wageni unaofahamu ambao bado hawamjui yesu kama Bwana. Weka hii oorodha kwenye simu yako, kwenye mkoba wako, kwenywe Biblia yako ama mahali pengine amabapo unaweza kuiona kila siku, waombee haw watu kwa uaminifu kila siku, ukimuuliza mungu kuwafufua na kuwafanya wamtumainie.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

Jaza fomu za uwajibikaji na shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 6:
# KUJITOLEA KWA MWINJILISTI

**Kama wainjilisti lazima tuhakikishe kwamab maisha na mienendo yetu" kwenya jukwaa" ni sawa na maisha na mienendo yetu "nje ya jukwaa". Je! Tuandumishaje uhalisi katika maisha na uinjilisti wetu? Tujikijenga juu ya uchunguzi wa maombi katika kikao cha awali, hap tunachunguza umuhimu wa kuishi maisha kamili ya kujitolea katika ukristo wetu na uinjilisti wetu.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Kujitolea hutupeleka mahali patakatifu tunapotumia muda wetu na baba yetu mtakatifu wa mbinguni, ambayo hututayarisha kuwa mabalozi vwa ufalme, wanaobeba ujumbe wa tumaini kwenye vinywa vyetu. Ujumbe ambao umeonyeshwa kuwa wa kweli, kwa mabadiliko ya mioyo yetu.

## ASILI YA KIKA

Wakuirudi kutoka kwa hija yao ya kila mwaka kwenda yersusalemu kwa sikukuu ya paska, Mariamu na Yusufu waligundua kuwa Yesu amepotea/ kosekana, mwishowe baada ya siku tatu waliungana tena na mtoto wao, wakimpata na waalimu katika vyunga vya hekalu, Yeu alikuwa ameketi katiu ya waalimu wenye busara akijifunza kutoka kwao., lakini pia akichangia na kuwashangaza kwa uelewa wake wa ajabu wa maandiko akiwa na umri wa miaka kumi na mbili tu. Mariamu alipomuuliza kwanini amewatia wasiwasi kwa kutangatanga, Yesu anaonekana kuchanganyakiwa na swali lake. Yesu amechanganyikiwa kwa sababu amaweza kupotea au kukosekana ikiwa wale wanaojaribu kumtafuta/ kumpata hawajui ako wapi. Lakini wangewezaje kujua kuwa angekuwa katika yumba ya babake? Hapa ndipo mahali pa asili kwake kuwa. Ni kama kuangalia kila mahali isipokuwa ikulu ya rais ya White House, unpojaribu kumtafuta rais wa Amerika, kisha unashangaa unapompata katika ofisi ya oval na kumuliza kwa hasira: "umekuwa wapi?"

Luka anaelezea lugha maalum katika jibu la Yesu kwa Maria ambalo linaonyesha madai yake ya uhusiano wa kipekeena mungu: "je! Hamjui nilipaswa kuwa kuwa katika nyumba ya baba yangu" (LUKA 2: 49) Inanoenekana hakuna mahali kwingine kwenye maandiko ambapo kuna taarifa au maneno haya yaliuonukuliwa na Luka, isipokuwa wakati Yesu apozuingumza. Maneno ya kwanza Ya yesu yaliyoandikwa ananukuliwa aksiema kuwa yeye ni mwana wa mungu.

Msalaba inamanisha tunaweza kuingizwa katika familia ya mungu na kupewa haki ya kuitwa wana wa mungu. Hivi swali linakuwa: ni rahisi aje kwetu sisi kutumia muda katika nyumba ya baba yetu?

Ni mahali pa kujitolea ndipo tunagundua Zaidi kikamilifu sisi ni nani, tunakuwa, tunasafishwa, tunajibika, tunahukumiwa kwa ajili ya makosa yetu, tunaagizwa kwa ajili ya kusudi letu, tunatimizwa katika kuwepo kwetu. Kwa kujitolea tunafanywa watakatifu kwa sababu yeye pia nimtakatifu.

Kujitolea ni muhimu katika maisha ka kikristo, kwa sababu ni aina ya utakatifu na ni muhimu katika kazi ya uinjilisi kwa sababu injili inapaswa kuishgi na kutangazwa na watu watakatifu.

# MWONGOZO WA KIKAO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili kuweza kujuliana hali, kuhimizana, maoni juu ya fursa, na jambo litahimiza kikundi. Zungumza juu ya orodha yako ya watu watano (MATUMIZI:KIKAO CHA TANO) na chochote kile umepata/shuhudia kwa kuwaombea watu hawa kwa uaminifu kila siku.

## MAOMBI - PRAYER

Chukua muda ili uweze kuomba, omba kuhusu jambo lolote, changamoto ama chcochote kilichoangaziwa katika kikundi wakati wa mapatanisho.

## MAFUNDISHO (DAKIKA 25-35) - TEACHING

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> “Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka, akaenda zake mahali pasipo kuwa na watu akaomba huko”
>
> **MARKO: 1:35**

Tunajitolea kwa vitu vyote katika maisha, tunaweza kujityolea jwa familia na marafiki, kuzingadia maadili mazuri. kujtolea kwenye timu ya mchezo au mazoea yetu. Au kupata alama za juu katika mchezo wa video kwenye simu.

Yesu alijitolea kwa familia na marafiki, pia kwa hakika alijitolea kujifunza biashara kutoka kwa yusufu. Alikuwa akijitolea kwa marafiki zake na alionekana akitumia muda Zaidi katika ushirika nao kuliko kuhubiri kwa makundi. Alikuwa amejitolea kwa mamake na kuhakisha kwamab mtume yohanna angemtunza baada ya kifo chake, ufufuo na upaaji.

Yesu anamanisha nini akisema kuwa alikuja kuweka fimilia dhidi ya kila mmoja (luka 12: 53). Tunaweza kuilewa kwa kuzingatia kujitolea kwake kwa baba wa mbinguni. Kujitolea ambao kulikuja kwa gharama ya mengine yote bila kujali nini ilikuwa ya muhimu.

Yesu hakuwa anasema ni makosa kuwapenda wazazi wako au kwamba haswa alitaja kuvunja familia, lakini yesu alijua chochote kinachoondoa utii wako msingi kwa mungu hatimaye kitafanya tusiwe watakatifu na ni katika kujitolea kwetu kwa mungu ndipo tunatakaswa.

> **SWALI:** baadhi ya mambo gani ambayo yanavutia kwa urahisi na kusababisha kutojitolea kwako kwa mungu. Ongea hasa mambo yasiwo mabaya na yao wenyewe, lakini yanaweza kuwa kikwazo kwa uashisi, kikwazo vya kutotii mungu?

Inawezekana kujitolea zaidi kwa uinjiisti kuliko yesu mwenyewe! Lakini tupo ili tumuabudu mfalme na sio huduma yetu. Lazima tupate msingi katika maisha ya kiroho, ambayo husikiliza mungu kwa ufanisi.

Haikujalisha mahitaji ya huduma yake wala mahusiano yao kidunia, yesu alitanguliza uhusiano wake wa kibinafsi na babake, alienda faraghani, kuomba na kusikiza, kwa yesu kuwa na babake ilikuwa mahali pa asili Zaidi kwake. Kuwa. Injili ya Markon inasimulia kuhusu hafla tatu za faragha. chukua muda juu ya kutafakari kuhusu vifungu hivi.

- Marko 1:35-39 kuamka mapema na kuomba mahali pa faragha, Je! Hii inamaanisha nini juu ya kupokea maagizo kutoka kwa mungu?
- Marko 6: 45-46 kuenda katika faragha na kuenda kilele cha mlima kuomba Je! Hiui unafunza nini kuhusu kufanywa upya na mungu
- Marko 14: 32- 41 kuuomba akiwa gethesemane kabla hajashikwa? Je! Hii unatufundisha nini juu ya kuleta uzito wa hali zetu mbele ya mungu?

Maombi yasiyokuwa ya kawaidana ya hiari kwa siku nzima ni nzuri, lakini kuweka kando muda wa ziada wa kusali na kusoma biblia ni muhimu. Baadhi ni wazuri wakati wa kuomba na sio wazuri wakati wa kufungua biblia. Wengine huwa na maadali makubwa ya kujifunza biblia

lakini hukwama wakati wa kuomba. Linaweza kuwa jambo la ufanisi kuchanganya zote mbili kwa kusoma sura zaidi ya maandiko na kuomba juu ya kile ambacho kifungu kinasema na jinsi inaweza kutumika katika maisha yetu. Pia ni muhimu kutumia kwa kusifu na kutoa shukrani kwa mungu na kulleta maombi na mahitaji yako kwake.

Yesu hakuwa na haja ya kukiri dhambi, lakini kukiri ni sehemu kuu ya sala anayofundisha wanafunzi wake: "utusamehe dhambi zetu" (MATHAYO 6, LUKA 11).Zaburi 51 ni nyenzo kubwa kwa maombi ya toba na tafakari. Hatua yetu ya kwanza katika utakatifu ni kutambua ya kwamba mungu ndiye mtakatifu na sio sisi. Tunamhitaji na tunapochukuwa wakati wa kila siku kuingia mbele zake, nguvu ya kubadilisha ya upendo wake itahakikisha kwamba hatuko vile tena. Nimabadliko haya ambayo yanasimama kama ushahidi wenye nguvu kwamba injili ni ya kweli na una nguvu ya kuokoa. Tunapotangaza wema wa mungu na kushiriki hadithi ya yesu, wale tunaowafikia wanaweza kukua kwa ujasiri wa ukweli wa ujumbe wetu wa injikli kwa kuchunguza kazi ya mungu kupitia maisha kwetu ya kujitolea kikamilifu.

Yesu ametufungulia njia ya kuwa watakatifu kupitia kazi ya kuokoa ya msalaba, akiyuta tufe kwa maisha yetu ya zamani na kumtumaini tunapoingia kwa maisha mapya yesu ametuonyesha inavyoonekana kufuata utakatatifu kupitia kujitolea kwetu kila siku kwa baba aliye mbinguni.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! ungeelezeaje wakatui wako wa sala/ maombi na wakusoma biblia?
- Je! unaona uhusiano kati ya afya ya maisha yako ya ibada na ubora wa unjilisti wako?
- Je! unaweza kujifungua kwa maagizao zaidi, kufanywa upya mtazamo na kutunu kupitia kujitolea kwa kusudia katika wiki zijazo?

"'kusudi na nidhamu za kiroho ni uhuru. Lengo letu ni uhuru sio nidhamu, wakati tuanfanya nidhamu kuwa lengo kuu tutageuka sheria na kupoteza uhuru huu.

... milele tuweke yesu kati na kutazama nidhamu za kiroho kama njia ya kutuvuta karibu na moyo wake."

**RICHARD FOSTER**

## MATUMUZI (DAKIKA 5)

Anza kuomba ukitumia/ukipitia kitabu cha zaburi, ukitumia dakika chakre kusoma kila siku na kuomba zaidi ya wakati wawakati wa Biblia na wakati wa maombi. Ikiwa unaweza jinyoshe zaidi ili uitumie kwa mwezi mzima au mwaka mzima. Unaweza kufanya hivyo kwa kufungua Biblia yako na utumie kitabu cha Zaburi moja kwa moja au kwa kufuta mpango mpango wa Ibada kama vile: MY ROCK, MY REFUGE> A YEAR OF DAILY DEVOTIONS IN THE PSALMS. / MWAMBA WANGU KIMBILIO LANGU: MWAKA WA IBADA ZA KILA SIKU na TIM KELLER.

## MAOMBI

Mshukuru mungu kwamab anatamani uhusiano na watoto wake. Jitoe kusali kwa maisha ya kujitolea ambayo inatutoa kutoka kuwa watali wa kiroho hadi kuwa watoto ambao wanaishi katika nyumba ya baba na mbele zake. Omba mungu akusaidie kuwa mtakatifu kama yeye alivyo mtakatifu, na mabadiliko haya ya maisha yenu yatakuwa msingi ambao uinjilisti wako umejengwa juu yake.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji na shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 7:
# UTII WA MWINJISTI

**Katika kikao hiki tutafafanua wazo la utakatifu tulilo chunguza katika kikao cha awali, haswa kwa vile unahusiana na utambulisho wa mungu, tumaini la injili na maisha ya mwinjilisti. Ututangalia uwajibikaji kama kitu cha muhimu katika safari ya mwanafunzi.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Mungu anataka watu wake wawe watakatifu kama yeye alivyo mtakatifu na ni kwa kutii roho mtakatifu na uwajibikaji katika jamii ili kukua katika utakatifu.

Habri njema ni kwamba mungu ametoa njia amabyo watu wasio watakatifu wanaweza kuingia mbele ya mungu mtakatifu na kukaa pamoja naye milele (Waefeso 5: 25-26). Maisha ya kweli ni maisha matakatifu.

Utakatifu pia ni mada ya ujumbe wa yesu kuhusu chumvi kwenye Mathayo 5: 13. Vivyo hivyo chumvi haina maana ikiwa itapoteza ladha yake ujumbe wetu hauna matumaini ikiwa tunapoteza utakatifu wetu wa kipekee. Ingawa maisha yetu ni kazi isiyokamilika u[pand huu wa milele. Tumeitwa kuishi tofauti ili ulimwengu utambue ukweli wa ujumbe tunaotangaza

Injili ni ujumbe mtakatifu unaoshuhudia kwa mungu mtakatifu amabaye alitenda kwa njia takatifu ili kuwezesha wasio watakatifu kurudishwa kwa utambullisho wao wa kweli-kama watu watakatifu wa mungu

## ASILI YA KIKAO

maneno "**utakatifu**" na "**takatifu**" yanapatikana zadi ya mara mia tisa katika Biblia, zaidi ya maneno upendo, Imani, kusamehe na kuomba pamoja! Utakatifu ni mada kuu ya Bibklia na mungu anatamani iwe msingi katika maisha yetu.

Mungu ni mtatakatifu, amabyo inammanisha kuwa ametengwa, yeye ni mkamifu, huru na wa kipekee na hakuna mwingine kama yeye. Sisi sio watakatifu kila mmoja wetu amepungukiwa na kiwango kamili cha mungu wetu mtakatifu. Mwandishi kwa Waebrania anatuambia kwamba watakatifu tu ndio watakaomwona mungu. (WAEMBRANIA 12: 14). Na yesu anatuambia wenye moyo sati watamuona mungu (Mathayo 5:8) ukosefu wetu wa utakatifu ni shida kubwa kwa wanadamu ikiwa tutakuwa na matumanini yote ya uhusiano mungu. Je! Asiye mtakatifu anawezaje kuwa mtakatifu, kukubalika kwa Bwana na kuweza kukaa katika ufalme wake?

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua musa huu kujuliana hali, kuhimizana, kusikiza maoni juu ya fursa na jambo lolote lile litakalo himiza kikundi, uuliza wana kikundi waeelezee juu ya uzoefu wao wa kusoma kwa maombi katika cha Zaburi (**Kikao cha sita: Matumizi)**.

### MAOMBI

Peana wakati kwa Bwana na uombe juu ya hali yoyote ile, nzuri au changamoto, au jambo lilili angaziwa wakati wa mapatanisho.

# MAFUNDISHO (DAKIKA 25-35)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

### 1. NI MUNGU PEKEE NDIYE MTAKATIFU

> "Na jina langu takatifu nitalifanya kuwa limejulika kati ya wangu wa Israeli;wala sitaliacha jina langu takatifu kutiwa unajisi, tena nayo mataifa yatajua kuwa mimi ndimi Bwana na aliye mtakatifu katika Israeli."
>
> **EZEKIELI 39:7**

Biblia unafunua mungu ni nani ilikutuweza kumjua na kumwabudu kwa roho na kweli. Tunaposoma tunangudua kwamba yesu ndiye mungu mmoja wa kweli. yeye niasiyeonekana na alielezwa katika asili tatu (Baba, Mwana na Roho mtakatifu), yeye ni mtakatifu yeye ni wa milele, yeye ni mfalme. Lakini kile mabacho biblia inafanya wazi kumhusu yesu niu kwamba yeye niu mtakatifu. Utakatifu ndio sifa kuu ya mungu inammanisha kuwa hakuna kiumbe kingine/ mwingine anaweza kufanana na utambulishio wake, taibia yake au hali halisi ya kuwa yeye ni nani. Na ni hii tabia/sifa amabo mungu natamania watu wake-kwamba tungekuwa watu watakatifu, kutengwa katika maabudu na utii wetu kwake. Watu wenye haki na usafi (Mambo ya Walawi 11:45). Ukosefu wetu wa utakatifu –kukataa kwwtu kwa utukufu wa mungu- umetia ubinadamu tabani. Ugfalme wa mungu ni ufale uliokamilika lakini tumechagua kuto kamilika na kwa hivyo kutengwa kutoka kwa uwepo wake.

### 2. UTAKATIFU WA MUNGU UNAWEZESHA UTAKATIFU WA WATU WAKE

> "...Basi yeye kwa kuwa anakaa milele, anao uhakika wake usioondoka. Naye kwa sababu hii anaweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee. Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliyemtakatufu asiyekuwa na ouvu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji aliyekuwa juu kuliko mbingu ; ambaye hana haja kila siku mfano wa wale mahuhani wakuu wengine, kwanza kuytoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu. Maana yeye alifanya hivi mara moja apipojitoa nafsi yake."
>
> **WAEBRANIA 7:24-27**

Tumeumbwa kwa mfano wa mungu na tuna iuwezo wa kuwa watu watatifu, lakini uasi wetu unatuzuia. Ikiwa mungu ataruhusu hata kipande kidodo cha kutokamilika katika ufalme, basi ufalme wake utakoma kuwa kamilifu. Kwa hivyo kukataa utakatifu wa unatutenga na utakatifu wa mungu na baraka za ufalmre wake.

Bubklia inatueleza kuwa yesu alichukua nafasi yetu msalabani, huku akuchukua kifo ambacho tulichagua sisi wenyewe. Ailiweza kuchukua nafasi yertiu lkwa msalaba kwa sababu utakatifu wake ni kamili/umekamilika (bila dhambi au kasoro). Deni lisilo weza kulipwa la uasi wetu/ wa dunia limelipwa kupitia hazina ya milele ya utakakatifu wake Yesu Kristo. Sasa wakati mungu anapowaangalia wale wanaomtegemea Yesu Kristo haoni kutokamilika (ukiwa) wa binadamu bali ukamilifu (utakatifu) wa Ysu Kristo.

Fikiria juu yake kama hivi: je! Uwewahi kuvaa nguo ikafanya ujisikie vizuri zaidi juu yako mwenyewe? labda ulikuwa unava mawazi kwa hafla maalum na ulipotak nje ya nyumba ulijihisi kujiamani zaidi. Biblia unatuambia tunapo mtegemea mungu, mungu hupatia haki/ ukamilifu wa yesu na tumevikwa ukamilifu wake. (WARUMI 5:18, Wafilipi 3: 9,1 Wakoritho 1, 30).

Paulo anatuambia kwamba badaka ya kupendekezwa na tamaa zetu za kimwili tunapaswa '' **Kujifunika na kristo**'' kwa halisi kuvaa zuri/wema wake (WARUMI 13: 14). Linganisha hii kwa yakobo mabaye anawahiumiza wasomaji wake kuondoa (kutafsiriwa kutoa/kuvua) uchafu wote wa maadili (Yakobo 1:21) Tunapaswa kuondoa mambo ya zamani ,ambayo ni kinyume na mungu na kumpa kristo na katika kubadilishana anabadalisha na kutupa haki yake mwenyewe.

Uwewahi kuondolewa/kufukuzwa kutoka mahali kwa sababu haukukidhi kiwango cha kanuni cha mavazi? mahitaji ya kuingia katika iufalme kamili wa mungu ni utakatifu kamili ambao hatuna. Lakini watu wasio wakamilifu tunaweza kuingia katika ufalme wake kamili bkwa sababu sasa tunaweza kutoshea ''kanuni la mawazi'' klupitia kristo. Hakuna chochote chini ya ukamilinifu kutakachofanya tuiingie ufalme na hakuna

chochote chini ya ukamlifu wa kristo tunapewa kuvaa siku tutakoingia katika ukweli kamili wa ufalme wa mungu, hatutaleta kutokamilika kwetu lakini wavazi ya haki.

### 3. KUTII ROHO NA KUJITIA NIDHAMU HUZAA MAISHA MATAKATIFU

> "Na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya mungu katika haki na utakatifu wa kweli."
>
> **WAEFESO 4:23-24**

Mungu anataka tukue katika ukomavu bila kurudia makosa yale yale mara kwa mara (dhambi ya kawaida) tupoishi kwa ajili yake leo. Tumefuunikwa na neema yake lakini ushahidi wa imani ya kweli ni mabadiliko na ukuaji (ufuasi). Hatupaswi kuridhika tu na kuvaa haki ya krsito kama kitu ambacho kitatuzuia kutiwa mbaroni, lakini chagua kuheshimu gharama ya haki tunayovaa kwa kushi kwa utii wa yule aliyetulipia. Hii ni safari yetu ya ufuasi ; kuhama kutoka katika wakati wetu wa awali wa kuzaliwa upya (kuhesabiwa kam wenye haki) na kuenda kwenye maisha mapya yenye uendelevu (utakaso).

Hii haitupi tu hakikisho la ukamilifu wa milele baadaye ambao unatungojea, lakini unatupa njia ambayo tunaweza kuishi kitofauti leo. Mabadiliko yanaotokea katika maisha ya mwanafunzi ni kwaa nguvu iulionyeshwa na ufafanuzi wa Paulo wa matunda ya Kristo ambayo inatoka katika maisha ya mfuasi wa kweli wa yesu. (WAGALITIA 5: 22-23). Kipengele cha mwisho cha matunda ni kujidhibiti. Mungu kwa roho ametuwezesha sisi kujitayarisha lakini tunapaswa kushiriana naye. (WAFULII 2:12-13)

Tukizangatia haya hapa kuna maneno manne ambayo tunaweza kufanya ili kukua katika utakatifu na utii kwa mungu:

#### KUJITOLEA

Kadiri tunavyotumia wakati mwingi katika neno la mungu, ndivyo tunavyojua zaidi mungu anataka tuwe nani. Vivyo hivyoi kwa kutumia muda katika katika maombi tuinawez pia kumuomba mungu utusaidie kushinda udhaifu wetu na majaribu. Kutumia wakati na yesu ni kujifunza maana ya kuiwa mtakatifub wakati huo tunapewa nguvu ya kuwa hivyo pia.

#### KUJITAMBUA

Tunaposoma neno, neno pia hutosoma ikitusaidia kuchunguza maisha yetu wenyewe na kuzidi kujitambua. Kujitambua huku kunatusaidia kutmbua udhaifu wetu na inamaanisha tunaweza kujima mambo ambayo yanatudhulumu.

#### JAMII

Kuwa mwangalkifu kwa maidsha tunayoishi haita tekelea tu kwa kujielewa tu. Kwa kujitolea kwa ushirika wa kikristo na jamii, tunajifungua kwa uchunguzi wa upendo kwa wale walio karibu nasi. Kuwekeza katika jamii kuzalisha fursa kwa wengine kuzungumza katika maisha yako na wewe pia kufanya vivyo hivyo. Kuwa wazi kunaweza kuleta changamoto, lakini hathari ya kuathiriwa haipaswi kuwa kizuizi kwa wazo la kibiblia la kusafiki pamoja kwa neema ili kukua kama watu binafsi na familia ya mungu.

#### UKIRI

Yakobo anatuambia tukiri dhambi zetu kwa kila mmoja, sio kwa kusamehewa lakini kwa uwajibikaji. (YAKOBO 5:16). Kupata kikundi cha marafiki wa kuaminika ambao unaweza kuwa mwaminifu na wazi nao juu ya mapambano, majaribu, na kutofaulu kwako ni muhimu.

Adui anataka kuficha mapambano/masumbuko yako ili aweze kuipotosha kuwa aibu, lakini mungu anatuita tusafikiri kwa pamoja, tukisaidiana kuajibika kwa kuleta udhaifu wetu kwa nuru amabapo anaweza kurudisha na kukomboa, kushindwa haipaswi kuwa jambo la mwisho na mungu. Uwajibikaji ni njia ambayo tunaweza kushugulukia udhaifu wetu kwa unyenyekevu na kujisalimisha kwa neema yake.

Kama mwinjisti ujumbe tuaotangaza sio tu kwa sababu tunataka kuona majibu lakini kuona wanafunzi wanaokuwa na kukomaa –watu watakatifu (WAKOLOSAI 1:28-29). Ni wanafunzi halisi ambao watabeba ujumbe hu vyema kwa ulimwengu kwa uadlifu na nguvu. Ni kazi takatifu kwa watu watakatifu.

## MAJADILIANO (DAKIKA 15)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiano:

- Je! Unawezaje kuelezea utukufu wa mungu kwa mtu asiyemjua?

- Je! ni jinsi gani ''tunajivika'' katika kristo?

- Je! ni nini ambacho kinakusaidia au kinakuzuia kuwajibika kihalisi kwa wengine?

> "Ikiwa unafikiria kuwa unaweza kutembea katika utakatifu bila kuweka ushirika wa kudumu na kristo, basi numefanya kosa kubwa sana. Ikiwa utakuwa mtakatifu basi lazima uishi karibu na yesu."
>
> **CHARLES SPURGEON**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Ikiwa tayari hauna kikundi cha marafiki unaowaamini (tofauti na uwajibikaji tunaofanya katika vikundi vya Advance ) amabao unakutana nao mara kwa mara amabo unaweza kuwa mwaminifu kabisa, wazi na kuwajibika, fikiria ni nani ambaye munaeza fanya hiuvi naye na upange hivyo haraka uwezekananvyo. Ikiwa tayari unaye ambaye unashiriki nao/naye elezea na mtu mwingine ambaye sio kwa nini ni muhimu kwao wewe kuwasaidia kuanzisha, na ushauri wowote, jambo la kuhimiza na vidokezo unavyoweza kutoa.

## MAOMBI

Tambua na kusherehekea utakatifu wa mungu wa mungu kwa maombi, omba msamaha kwake kwa uasai wako na shukuru kwamab kwa sabau ya kazi ya kuokoa ya yesu unaweza kushuiriki katika haki /uadilifu wake. Omba kwamba mungu ataendelea kufanya kazi maishani mwako kukufanya uwe mtakatifu na kujitolea kuishi na nidhamu kwa kutii nguvu za roho wakati unatafuta kukua kama mwanafunzi wake na kua zaidi kwa kusudi kama watu watakatifu walio na ujumbe mtakatifu.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 25)

*Jaza fomu za uwajibikaji shiki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane. Chukua muda zaidi katika kikao hiki kufikiria kuhusu maswali yaliyo kwenye fomu na kupeana maoni yaliyo ya kweli, tumia muda kuomba kuhusu hivi vitu.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 8:
# SIFA ZA MWINJILISTI

**Wakristo watakatifu ndio wanyenyekevu zaidi. Kwa hivyo. Je! ushara ya unyenyekevu katika uinjilisti ni nini?**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Unyenyekevu ni madli kuu ya mhubiri: yesu akiwa kielelezo, kusafishwa na kuwezeshwa ndani yetu na roho takatifu kwa utukufu wa baba.

## ASILI YA KIKAO

Kuanzia wajati malaika Gabrieli Maria anatarajia mtoto, '' unyenyeku'' maada ku katika hadithi ya yesu inaibuka, Maria anaabudu mungu na namshukuru yeye kwamba amemkumbuka mtumishi wake, katika hali yake ya unyenyekevu, kwa maneno mengine anasema: '' mimi ni msichana wa kawaida tu, kwa nini mungu anataka kunutumia?''

Je! umewahi kujiuliza ni kwa nini mungu anataka angekutumia?

Wakati mwingine tunaweza kujihakikishia karama/kipaji na tanta zetu tukiamini kwamba mungu anachagua kutumia kwa sababu ya hivi vitu. Wito wa mungu ni kwa tabia zetu ,sio talanta/kipaji/karama yetu na tabia inayompendeza mungu sana ina unyenyekevu ndani yake. Maria anaendelea kusifu jini mungu wake mtakatifu anavyotawanya watu wengi nwenye kiburi na kuwainua wanyenyekevu. Kama mwanamke mdogo wa kiyaudi kuelewa kwake kwa agano la kale ungempa kil akitu anachohitaji kusema madai haya juu ya mungu kwa ujasiri, na sas alikuwa akijionea kweli huu mwenyewe. Daima mungu amechagua kutumia wanyenyekevu kwa kusudi lae, kwa njia zisizotarajiwa, akikadi hekima ya ulimwengu na kufdunua nguvu na neema yake kupitia watu walio na uwezekano mdogo.

Hatua ya kwanza ya kuelekea kutumiwa kwa mambo makuu na mungu ni katika kutambua utegemezi wetu kamili kwake. Kuzaliwa kwa yesu hakuyngefanyika katikamazingara duni zaidi. Mfalme wa wafalme alizaliwa kwenye zizi la ng'ombe na kuwekwa ndani ya hori- chombo cha kulishia wanyama. Utajiri wa kuzaliwa ulipadilishwa na umaskini wa kuzaliwa kwa mtu yeyote. Upatanisho wetu kwa muumba vyote ulianzishwa kwa unyenyeku wa kushangaza.

Popote tunapoangalia katika maandiko iwe Isaya 53, amabpo tunaambiwa juu ya mtumwa wa bwana ambaye atachomwa mkuki kwa makosa yetu, au tangazo la yesu kuhusu kuja kuhudumu sio kuhudumiwa au kuosha/kunawa miguu ya wanafunzi wake, ama kujisalamisha kwake kwa mapenzi ya Baba yake katika bustani ya Gethsemane au kuruhu kupigwa, kudhihakiwa na angeweza kuangamiza mtu yule aliye mdhulumu.Biblia inanaonyesha picha ya mfalme mtumwa amabye anashinda laana ya kiburi cha binadamu kwa nguvu ya unyenyekevu mtakatifu.

Mungu huwaokoa watu wake kwa njia ambayo anawakusudia waishi. Kiburi kulituongoza kwenye uharibifu na unyenyekevu utakoaturudisha/rejesha.

> "mana mmejua neema ya Bwana yesu Kristo jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yeni, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba nyinyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake."
>
> **2 WAKORINTHO 8:9**

# MWONGOZO WA KIKAO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Tumia muda kujiliana hali, kuhimizana, maoni juu ya fursa na kitu chochote kitahimiza kikundi, kwa makundi dogo uliza kila ashiriki ushindi mmoja na jambop moja analo pambana nao. Kwa makundi makubwa chagua watu wanne au watano washrirki/watoe ushuhuda maalum tangu kikao kilichopita.

## MAOMBI

ComPeana wakati kwa Bwana na uombe kuhusu hali yoyote nzuri au chanya, ama jambo lolote lile liliongaziwa kwa kikundi wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 25-35)

*Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.*

> "Msitende neno lolote kwa kushindana wa majivuno, bali kwa uyenyekevu kila mtu amuhesabu mwenzake kuwa bora kuliko nafsi yake, kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.
>
> Iweni na nia hyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya yesu.
>
> Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya mungu, naye hakuona kuwa sawa na mungu kuwa nitu cha kushikamana nacho ; bali ajifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akwa ana mfano wa wanadamu ; tena alipoonekana kama mwanadamu alijinyenyekeza awa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba!"
>
> **WAFILIPI 2:3–8**

Akitoa maoni yake kuhusu unyenyekevu C.S Lewis aliandika hivi:

> "unyenyekevu wa kweli sio kufikiria/kuwazia au kujiona duni bali ni kutojiwazia."

Biblia haituulizi tuwe wenywe kujishusha au tujine duni. Unathamaniwa na kupendwa na mungu bna amekuita mtoto wake wa thamani. Lakini kuna mstari, kujifikiria sana sisi wenyewekunatuweka katika hatari ambao ilitia ubindamu katika dhambi. Kufikiria na kujiona duni ni kukataa litambulishp ambacho mungu ametununulia na kujiwazia ni kushindwa kutambua enzi kuu na ufalme wangu.

Kiburi kipo katika kila dhambi, methali unatuambia kwamba: ''kiburi kinapokuja tunapta aibu, lakini kwenye unyenyekevu huja heshima'' (Methali:11-2) Fasihi ya hekima ya Biblia inathibitisha mara kwa marea fadhila ya unyenyekevu kama kinyume cha kiburi na kusherehekea baraka zinazoambatana nayo.

Tunaishi katika umri na enzi ya kukuza ubinafsi, je! hebu fikiria ikiwa Daudi angemuuwa Goliath leo? Jaribio la kupiga picha ya kibinafsi ya ushindi huku ameshika kichwa cha Goiliathi kilichokatwa damu ikitiririka litakuwa zito sana. Wengi wetu tutakaribisha wazo la nyimbo za sifa zitungwe ju ya wafanikio yetu, sinema, filamu zifanywe na hata tupewe vyeo na majina makuu. Na bado kama D.L Moody anavyosema katika mahubiri yake- Daudi hasemi wala kutaja ushindi wake katika Zaburi zake zote. Leo hii tukinusa ukuu kidogo tunahimizwa kujitetea na kujenga hadhii na jukwa letu. Mungu hakuulizi ujenge huduma au ujinyanyue kwa nafasi. Mungu anavutiwa zaidi na tabia yako na jinsi anavyoweza kuinuliwa kwa malengo kwa malengo yake kupitia unyenyekevu (LUKA 14:11)

Yesu alichukua njia ya chini, akachukua nafasi ya mtumishi, yeye ndiye mfalme ambaye hakuja kuhudumiwa bali kuhudumu (MARKO 10:45). Angalia jinsi Yohana anasema kuhusu yesu ; kabla ya yesu kunawisha miguu ya wanafunzi wake:

> "yesu hali akijua ya kuwa baba amempa vyote mikononi mwake na ya kuwa alitoka kwa mungu naya anakwenda kwa mungu ; aliondoka chakulani ; kaweka kando mavazi yake, akatwaa kitambaa akajifunga kuononi."
>
> **YOHANA 13:3-4 MSISITIZO UMEONGEZWA**

Akijua ya kuwa vitu vyote vilikuwa chinin ya uwezo wake na kujua utambulisho wake kamili, Yesu alichangua kluwa mtumishi, kuonyesha mapenzi ya baba yake. Labda umewahi kufanya somo la biblia juu ya hii iluhusisha kuosha miguu ya mwingine. Lakini kuosha miguu ya mtu haifanyi haki kwa umuhimu kamili wa kile ambacho yesu alikuwa akiwaonyesha wanafunzi wake. Ni vigumu kwetu kuelewa jinsi inghekuwa vibaya kwa Rabi wao, mesaya wao afanye jukumu hili la kuosha miguu zao kama ishara ya unyenyekevu wake na moyo wa mtumishi.

Fikiria hivi unasikia hodi mlangoni, unafungua mlango na kupata mfalme mtawala wa taifa lako mlangoni pako, wananingia ndani ya nyumba na kumchukua mtoto na kuanza kubadilisha nepi iliyojaa. Hariufu ni mbaya na unatazama kwa hofu pale mabapo uchafu wa nepi unamuendea mfalme kwenye mikono, lakini bado mfalme anaonekana kuwa mwenye raha kabisa na hali hiyo, akifurahia wakati wao na mtot katika shughuli hii mbaya lakini ya lazima.

Usisahau wakati yesu alikuwa akiosha miguu ya wanafunzi wake, mara nyingi walikuwa wenye kiburi na dhaifu, na bado kwa nguvu na utakatifu wake alijinyeyenyekeza mbele yao, akiwapa mfano wa kufuata. Sio tu walipaswa kuosheana miguu bali walipaswa kuwa watumishi wanyenyekevu katika kila jambo.

Kuna hadithi fupi unayojulikana juu ya Charles spergeon, alipomwona mmoja wa wanafunzi wake wa kuhubiri akipanda juu ya mimbari na kikubiri, baadaye aliposhuka kwenye mimbari na soni akilalama jinsi mahubiri hayakuwa mazuri inasemekana Spurgeon alisema: "**ikiwa ungepanda jukwaa vile ulivyoshuka, ungeweza kushuka vile ulipanda**"

Bila kujali ukuuwa wito wetu, uvutio wa karama/kipaji chetu, ukubwa wa nafasi au sifa ya huduma yetu. Hatuna nguivu ya kuokoa mtu yeyote. Mshahara wa dhambi ni mauti (WARUMI 6:23), Lakini mshahara wa unyenyekevu ni uzima (methali 22:4). Kupitia mtumwa mnyenyekevu anayeteseka ambaye alichukua adhabu yetu msalabani, sasa tunaweza kumtumainia nakuchukua msalaba wetu wenyewe kwa kufa kwa kwa unyenyekevu kwa maisha yetu ya zamani ya kiburi. Tunaweza sasa toka kwenye kifo na kuelekea kwa uzima. Unyenyekevu sio sifa tu, ni jibu pekee linalofaa kwa Yesu tunapogundua yeye ni Bwana.

> "kwa vile Bwana awaridhia watu wake, huwapamba wenye upole kwa wokovu."
>
> **ZABURI 149:4**

Unyenyekevu k\tika uinjilisti haimanishi kwamba tuwasikize watu na kuwa sifu au kuilowesha injili na kufanya isiwe ya maana, au kuwacha kushiriki injili ambapo inaweza kusababisha kukosana/kuleta ugomvi na vikwazo (na injili mara nyingi ni ujumbe wenye kuudhi) saw vile ujasiri katika uinjilisti haimaanishi kutalazimisha kwa kutumia nguvu kuieteresha chininkwenye koo za watu bila kuzingatia ni njia ipi tunaweza kuwasaidia waelewe tumaini tunayi. Unyenyekevu uinjilisti angalau inaamisha maneno haya manne.

**SWALI:** Chukua wakati kuzungumzia kuhusu kanuni hivi nne za unyenyekevu katika uinjilisti. Je! Ni jinsi gani unawez kutumia nkanuni hizi nne katika huduma yako?

### KUMTUMIKIA MUNGU KWENYE UNYENYEKEVU

Lengo letu la msingi na hamu ni kumtumikia mungu, haie ni vigumu kiasi gani, iwe inazua wasiwasi, au gharama kubwa Je! Tuko tayari kuvaa asili ya mtumishi na kumtii bwana Yesu?

### UNYENYEKEVU UNAJITOA

Unyenyekevu unajumuisha kujididmishs ili tuweze kujazwa na roho mtakatifu tendo hili lenyewe ni la unyenyekevu. Tunapomwalika tunahoma kutoka kujitolea kwa unyenyekevu na kuwezeshwa kupewa nguvu kwa akili yake.

### POKEA NENO LAKE KWA UNYENYEKEVU

Jinyenyekeze mbele ya neni la mungu, jufunze kuisoma vizuri na kuikubali kwa masharti yake sio kulizamisha kusema kile unachotaka ili kukidhi mahitaji yako. Tafuita kwa unyenyekevu kusikia ukweli wa mungu bila kujalim changamoto ya kimatamaduni. Gundua ukweli wa mungu kwa kutumia hekima yake inahitaji unyenyekevu.

#### WAHUDUMIE KWA UNENYEKEVU WALE AMBAO TUNAWAHUBIRIA

Tngazo ni muhimu lakini lazima pia tupende ulimwengu, lazima tuawahudumie wale ambao wana mahitaji, tunapolenga kupenda watu wazuri lazima tuwasikilize vizuri. Ikiwa kile tunachofanya ni kuzungumza nao tu basi tunaweza kukosa sehemu muhimu yay a upatanisho kati ya injili na maisha yao na kupunguza uwezekano wa uhusiano wa maana nao.

Kwa kumheshimu mungu na kupeana nafasi ya roho yake kufanya kazi yetu na kujenga juu ya ukweli wa neno lake tunaweza kuwa watumishi wenye ufanisi ulimwenguni ambao tunakidhi mahitaji, kusikiliza viizuri watu wake na kutangaza kwa uawaminifu hadithi ya yesu. Ikmiwa tunataka kuzaa matunda katika uinjilisti wetu, msimama wetu wa kuanzia ni lazima uwe na unyenyekevu mbele za Bwana. D.L Moody anaiweka hivi.

D.L. Moody puts it this way:

> "Nina mtu wa pea kwenye shamba langu ambalo ni nzuri sana, inaonekana kuwa miti muziri sana mahali yangu, kila tawi linaonekana kufikia mwanga karibu sawia na mshumaa, lakini sijapata matunda yeyote kutoka kwenye miti hii. Nina miti mwingine ambao ulikuwa umejaa matunda mwaka jana kwamba matawi karibu kugusa ardhi. Ikiwa tutashuka chini vya kutosha, basi marafiki zangu mungu atatutumia kila mmoja wetu kwa utukufu wake."
>
> **DL MOODY**

## MAJADILIANO (DAKIKA 15)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! kuna sehemu ya maisha yako ambayo umepata changamoto na unyrenyekevu?
- Je! kunao mzozo wa asili kati ya kushiriki injili kwa ujasiri na kushiriki ijnili kwa unyenyekevu?
- Je! tunwazeje kushughulikia ukosefu wa unyenyekevu au kuwepo kwa unyenyekevu wa owongo kwa wengine?

> "Nina hakika kwamba upendo na unyenyekevu ni mafanakio ya juu katika shule ya Kristo na ushahidi mkali zaidi kwamba yeye kwa kweli ni Bwana wetu."
>
> **JOHN NEWTON**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Fikiria kwa makini kuhusu jinsi unanyoweza kutumikia na kubariki wale walio karibu na wewe nawe kwa njia usiyotarajia na ya gharama kubwa. Je! kanisa lako au huduma yako hutumia mtu wa usafi? Waambie wachukue siku ya kupumzika ili kutumia muda huu na familia zao au kwenda faragha ya kiroho na uwafanyie kazi zao. Kuwa kwanza kutengeneza chai naun kahawa ofisini kila siku. Mpe mhudumu wake mkahawani au hoteli kiunua mgongo kizuri baada ya hao kuhudumia na baadaye uwaandikie barua kuelezea upendo wa mungu kwao- kusudia na kuwa mbunifu.

Kwa upande mwingine hakuna moja ya mambo haya mabayo yanaweza kuchukua athari kamili ya Yesu kuwaosha miguu wanafunzi wake, lakini kwa upande mwingine hayapaswi tu kuitwa '' matendo ya fadhili yasiyo na mpangilio '' haya ni matendo ya maksudi wa watu wanaofikiria, wenye upendo na wanyenyekevu ambao wanaona fursa kila mahali ya kubariki wengine kwa njia ambazo zinaelekeza kwa mtumishi anateseka. Hatufanyi mambo hya ili kupata neema na mungu ama kuonekana kuwa mzuri mbele ya wengine (kwa kweli usiende kwenye mitandao ya kijamii na kupiga kelele juu ya mambo unayofanya. Tunafanya haya yote kama njia ambayo tunaweza kutumia kukua kwa unyenyekevu na kama matokeo asili ya unyenyekevu ambao mungu anakuza ndani yetu.

## MAOMBI

Shukuru kwa unyenyekevu wa Kristo na mfano wake wa moyo wa mtumishi. Omba mungu akusaidie kujiona kama vile anavyokuona na ili uweze kukua katika unyenyekevu na hekima kila siku. Ombeaneni ili mpate kuwa mjasiri na wanyenyekevu katika kutangaza injili.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 9:
# FURSA YA MWINJILISTI

**Ishara moja ya mwjilistin aliye na kipaji ni uwezo wa kuona- na hamu ya kutumia fursa yeyote na kila furs aya kushiriki ijnili na wale walio karibu nasi. Katika kikau hiki tutachunguza jisi tunaweza kutumia kila fursa.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Mhubiri anapaswa kuwa tayari kuchukua fursa yeyote ambayo inatokea mbele yao, akielezea injili kwa uwazi katika hali ya mazingara yao.

## ASILI YA KIKAO

Petro anatueleza kuwa tunapswa kuwa tayari kushiri ijnili na mtu yeyote anayaulizia juu ya tumaini ambalo tunalo (1PETRO 3:15). Paulo namwambia Timotheo awe tayari kuhubiri katika kila msimu na hali yoyotre ya maisha (2 Timotheo 4: 2) na anaandika mahali kwingine tunapswa kutumia yote ile i patinakapo(WAKOLOSAI 4:5). Yesu anaonyesha maisha ya utayari wa kutumikia na kushiriki wakatinwowote. Wakati mwingine inaamanisha kuangalia katika maeneo yasiyo tarajiwa ili kuona fursa(Zakayo katika LUKA 19: 1-10), Kuwa tayari katika maswala changamoto ya kijamii (kama vile mwanamke Msamaria katika Yohana 4: 1-26) kuwa na tayari katika maeneo ya upendeleo (kumbuka mwanamke mwenye dhambi nyumbani kwa mfarisayo katika Luka 7: 36-50), akiashirian na watu waliotengwa kijamii (kama vile uopnyaji wa ukoma katika Luka 17: 11-19), au kutangaza ukweli wakati wa mateso yako mwenywe (kama vile mwizi mslabani katika LUKA 23: 39-43) nakadhalika.

Mikutano ya injili ya Billy Graham ambayoalihubiri kwa watu wengi kuliko mtu mwingine kuwahi kuishi ilikuwa sehemu maarufu sana katika uinjilisti wake, lakini hii haikuwa njia pekee ambayo Billy Graham alishiriki injili katika maisha yake yote. Iwe ni kukutana na ma rais au wafalme, kuonekana kwenye vipindi vya mazungumzo kwenye mitandao ya habari, kulea misaada kwaq maeneo yaliyokumbwa na majanga, kuhudumia wanajeshi walio ng'ambo, au kushiriki na watu ambao alikutana nao njiani. Billy Graham alikuwa tayari kila wakati, amejiandaa kushiriki kwa hiari na wale amao alikutana nao.

Billy hakuwa tu na utii wa maandiko au kufuata kwa njia ya nguvu agizo kuu na kwenda zaidi ya fursa za wazi. Uhamasisho wake wa kuona na kuchukua kila fursa ulitokana na kuelewa kikamilifui, kupokea na kutii injili.

Mwinjilisti atakuwa mna huruma isiyo ya kawaida kwa waliopotea ambayo inapita zaidi ya kuridhika kwa kutimiza ushiriki wa injili au furs aya kuhubiri. Mwinjilisti anatamani kila mtu asikie na kupokea injili hata kuwe na tishio la kukemewa na matokeo mabaya hayataweza kumzuia kuzuia kuzumgumza juu ya yesu kwa kila fursa (MATENDO 4: 18-20)

Hadithi ya kweli ya Desmond Doss iliyoelezewa hivi karibuni katika filamu ya Holywood ya HACKSAW RIDGE inaelezea mtu ambaye alishinikizwa kujiunga na jeshi kama daktari jeshi, wakati wa vita kuu vya dunia vya pili, lakini alikata kuchukua/kutumia bunduki kwa hali yoyote ile kwa sababu ya iumani yake kwa mungu. Alipoagizwa atumike katika kisiwa cha Okinaewa kule Japani, Doss alijukuta kwenye eneo la adui jeshi, juu kwenye safu ya mlima wa cha Hacksaw kati ya mashambulizi makali ya adui, lakini aliwqeza kusikia kilio cha majeruhi wakiwemo wajapani na wamerika. Doss alianza kuokoa mtu yeyote aliweza ambapo ilimhusisha kushusha chini ya safu wa mlima huo kwa kutumia mfumo wa kapi wa muda mfupi. Doss alipigwa rihasi mkononi na mpiga risasi hodari, baadaye aligundulika kuwa na vipande vidogo vidogo vya chuma kumi na saba kwa mwili wake kutokana na milipuko ya mabomu lakini bado aliendelea kuokoa watu wengi kadri ya

uwezo wake. Alipohojiwa juu ya klitendo hiki cha ajabu, Doss alielezea kuwa wakati wowote alihisi uchovu ukimwingia na hawezi kumsaidia mwingine tena aliomba mungu nakusema: '' bwana nisadie niokee mtu mmoja zadi''. Doss aliweza kuwaokoa watu sabini na tano kwenye safu hio.

Ombi la Doss ni ombi la lika mwinjilisti: '' Bwana kupitia kila fursa hata iwe ngumu au ya gharama gani, nisaidie kupata mmoja zaidi''

# MWONGOZO WA KIKAO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili kuweza kujiliana hali, kushiriki hadithi, mmaoni juu ya fursa, na jambo lolote litakalo himiza kikundi.kwa makundi madogo uliza kila mtu ashirki ushindi mmoja na jambo moja nalo pambana nalo, kwa makundi makubwa chagua watu wane au watano washiriki ushuhuda maalum tangu mkutano wa mwisho.

## MAOMBI

Toa muda kwa mungu na uombe juu ya jambo lolote zuri na choichote kiulichoangaziw wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> "Basi Petro na yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni saa ya kusali saa tisa, na mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka tumbonio mwa mamaye alichuliwa na watu ambaye walimweka kila sikun katika mlango wa hekalu kwa jina "mzuri" ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndanin ya hekalu. Mtu huyu akiwaona Petro na Yohana wakiingia hekaluni aliomba apewe sadaka, na Petro pamoja na Yohana akasema: "tutazame sisi, akiwaangalia akitaraji kupata kitu kwao lakini Petro akasema, mimi sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho, kwa jina la yesu kristo wa nazareti, simama uende."
>
> **MATENDO 3:1–6**

Ni rahisi sana kukosa fursa, majuto mengi ambayo watu wanakabiliana nayo baadaye maishani mwao zinahusu fursa zilizokosekana, mamboi ambayo watamani wamgefanya iiwa tu wangekuwa na ujasiri wa kujaribu au wangekuwa na wasiwasi mdogo juu ya kile watu wanawaza juu yao.

Ulimwengu wa mnitamdai ya kijamii umesababisha jambo jipya: - HOFU YA KUKOSA, katika ulimwengu uliounganika wakati tunaona watu wengine wana maisha mazuri kutuliko, hofu huu ya kukosa hutujia. huu hii uanchukuliwa kuwa isiosaidia ni athari mbaya kwa uhbusiano wetu, na ni vipi unaposoma biblia. uwewahi kuhisi hofu hii ya kukosa unaposema Biblia? Umewahi kuhisi hii hofu unaposema juu ya wnafunzi wa kanisa la awali kwa waliotemda katika matendo ya mitume?

Kusoma juu ya mitume katika gano jipya, kunaeza kufanya ujihisi kuwa unakosa kiwango sawa cha bahati waliopta kushikiri katgika ijnili wakri wengi wetu hatutamani vitu vya kutisha kama kupigwa kwa mawe hadi kufa tongependa kuona na kupta uzoefu zaidi wa ishara na maajabu yalioambatana na huduma mitume.

Katika Matendo tatu Petro na Yohana wanakumbana na hali ya kila siku. Mwombaji aliye kiwete akiwaomba pesa. Ingekuw rahis kwa mitume kumpita mtu hyu mwenye bahati mbaya, au kutoa mchango mdogo na kuendekea na shughuki zao.

Tazama jinsi lugha ilivyo maalum hapa. Badala ya kuenmdelea na safari yao wamkodelea macho, tafsiri ya NRSV inaonyesha Petro na yohana wakimtazama kwa makini sana mtu huyo ambaye pia aliwatazama kwa tarajio la kupata msaada.

**SWALI:** Je! Unatazama dunia unayo kuzunguka kwa umakini hgani? Je! Una uwezo gani wa kuona na kuchukua fursa ya kushiriki injili amabyo ikonje ya huduma yako ya kawaida (kwa mfano kuhubiri ijnili uspokuwa kwa jukwaa)?

Yule kiwete aliona fursa ya kupoata kile alidhanui alihitaji sana-pesa. Kwa bahati nzuri mitume walikuwa wakizingatia fursa iliyokuwa mbele yao, kumaanisjha walikuwa na uwezo wa kumpsa kile alichohitaji zaidi-Yesu. Huu ilikuwa upendo kwa walio potea ambao ilisababisha Petro na Yohana kusimama, sio tu huruma kwa ulemavu au hadhi ya kijamii.

Biblia inatueleza kwamba: yeye anaye mheshimu mungu, ataheshimika na mungu pia, (1 SAMUELI 2: 30). Hii ni kweli haswa tunapo mheshimu mungu kwa ''vitu vidogo'' vya maisha. Tunapodhihirisha kuaminika mahali pa siri sehemu ndogo zisizonekana za maisha, mungu hutakabidhi vitu vikubwa. Hii unawezekana kuwa vitu vikubwa, hii inaweza kuwa jukwaa kubwa, lakini kwanini uridhike tu na hadhiri kubwa? Bora kuliko jukwa kubwa ni onyesho la nguvu ya roho mtakatifu katika maisha yertu. Kipimo kamili cha roho wa mungu aliyehai kinapatikana kwako leo unapojitiisha kwa Bwana, lakini anaonekan mara nyingi kukabidhi kikamilifu wale anajua wataitumia vizuri kwa huduma yake.mtu yeyoye katika jeshi la waisraeli angeweza kumshinda goliath kwa msaada wa mungu. lakini ni Daudi amabye alijitokeza na kudhibitisha kuaminika kwa kazi hii maalum, kwa hivyo barabara ya kuelekea katika kiti cha enzi ikawekwa.

Ikiwa unatyaka kuhisi kwamba umekamilika au jinsi mitume walihisi basi kuwa mwaminifu katika vitu vidogo, fursa za kila siku na ushuhudie kile mungu atalkachofanya. Ikiwa unajihadi kupata motisha juu ya kutumia fursa hizi muombe mungu akutoe katika nje ya eneo lako la faraja na uenndelee kuchagua kuwa maksudi hata wakati haujisikii. Ikiwa unajihisi lkuwa na hatia juu ya fursa ulizo zikosa na kuhisi kwamab umemuangusha mungu, kumbuka kuwa mungu hataki ujihisi kuwa na hatia juu ya fursa ulizozikosa ila anataka upende waliopotea kutokana na upendo wako kwake.

Hakuna hata mmoja wetu aliye mkamilifu, hata mitume walifanya makosa katika uinjilisti wao kwa kweli walipoteza fursa. Jambo sio kushikilia/kujipima kwa kiwango kisichowezekana, kinachongeza presha ila ni kushilias kwa upemndo usiolinganishwa wa mungu inayoongeza neema. Ni kwa ukweli huu ndio tunakua, tukikomaa kwa uaminifu zaidi kwa kupitia kursa anazoweka mbele zetu kila siku.

D.L. Moody aliwahi kusema: “Mungu amenipa mashua la maisha na kusema:” Moody okoa wote amabo utaweza, uwezo wetu wa kupiga mashua, kuwaona wale wanaozama na kuwavuta kutoka kwenye maji kunapatikana katika upendo wako kwa mungu na upando wake kwa ulimwengu.

Hapa kuna mapendekezo matatu ya jinsi unavoweza kujua fursa za kila siku na kuwa mwaminifu katika hizo.

### 1. WEKA JARIDA

Kuna faida nyuingi sana kwa kuweka jarida, ukiwa na fursa akilini, andika maelezo juu ya siku yako. Unakaa na nai kazini, je! Wewe humpita yule mtu asiye na kazi jijini mwako mara kwa mara? Je! Unazunguimza nani kwenye lango la shule? Kuandika kwenye jarida litakuwezesha kueka hawa watui akilini mwako ili uweze kuwaeka katika maombi pia unaweza kutumiwa kama ukaguzi wa uwajibikaji wa kibinafsi.je! uankusudia kufanya mazungumzo nao juu ya Imani? Ukihisi unaweza, unaweza pia kuuliza uwajibikaji mwemzi wako asome jarida lako na akuulize maswali kuhusu sehemu hizi.

Jadili mapendekezo haya matatu (JARIDA, CHANGAMOTO, SHANI) Je unaona thamani ya hivi vitu na unaweza kuvitekeleza.

### 2. CHANGAMOTO

Kwanini ujipe changamoto ikiwa ikiwa unajitahidi kuchukua fursa kila siku? Kwa mfano wiki hii nataka kuzungumza na angalau mgeni mmoja kuhusu kristo. changamoto hii inaweza kuwa vitendo na vile vile kutangazwa, na inafaa kuonyoshwa zaidi ya harakati zako za kawaida za uinjilisti...

### 3. SHANI

Badilisha mawazo yako kutoka kwa wajibu kwa shani. tuko na jukumu la uinjilisti na tunataka tu tiii kile ambacho mungu anataka tufanye, lakini

bila upendo tunakosa hoja. Kwa wiki yako fikiri kuhusu fursa sio tu kawa majibu mzito lakini kama kilele cha shani, watu wengi wanofanya kazi kila siku kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni na wanapend kazi zao husubiria wikendi kwa hamu sana. Je! Tunaweza kuwa watu ambao tunahamu ya fursa ya unjilisti/kushiri yesu jinsi ya vile hawa pia wana hamu ya wikendi? Ikiwa tunaweza tutaanza kukubalki shani kwa ukomavu wa akili, ili hata iwe ni vigumu aje, tunaweza kujifuta vumbi na kuendelea tena.

## MAJDILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! Umewahi kukosa fursa ya wazi, ulifunza nini kutokana na kukosa fursa hii?"
- Je! Ni chamgamoto zipi kubwa unazokabiliana nazo unapotumia kila fursa kushiriki injili?
- Je! Unawezaje kuunda kwa maksudi fursa na kushiriki ijnili ambapo vingenevyo inaweza kuwa haipo.
- Jadili naomi haya matatu kutoka kwa mafundisho (Kuweka Marisa, kujipa changamoto na shani) je! Unaona umuhimu wa mambo haya? na je! Unaweza kuyahitimiza?

> "Hapa kuna kanuni na Badilisha hatua zako kwa hitaji la watu ambao unawahudumia. Unapswa kuchukua ijnili kwao kwa njia na hali ambayo faida tutapata kutoka kwao ni kusikilizwa."
>
> **CATHERINE BOOTH**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Kuwa na nia au kusudi mwezi huu juu ya kutumia fursa ambazo kwa kawaida ungezipita au kuchagua kutoshirikiana nazo. Je! Kuna rafiki wa zamani amabye unaweza kufikia? Unaweza kuchukua muda wa ziada kukaa na kuzungumza na mtu asiye na makazi, je! Wewe hupata kahawa au chai au chakula chas mchana kutoka mtu yule yule? Ikiwa ndivyo, je! unaweza kubadilisha mazungumzo yenu yawe juu ya Yesu?

Ni hakika kwamba kila mtuy katika kikundi ataweza kufikiria fursa katika wiki yao uya kawaida amabayo wangeweza kuwa na nia au kusudi ka kushiriki juu ya yesu Kristo. Jitolee kuchukua fuirsa hizi ili kuhakikisha kila mmoja kweenye kikundi anawajibika katika fursa hii na mtajadili mwezi ujao. Kumbuka hii sio tu juu ya kuweka malengo ya kiholela lakini kubadilisha tabia na mwelekeo wa tabia.

Kila kinachoanza kama mazoezi ya kusudia kinaweza kukua kuwa tabi aya asili kwa muda.

## MAOMBI

Shukuru mungu kwamba anakupa nafasi ya /fursa za kutangaza injili yake na kushiriki imani yetu na wengine, mwambie atoe fursa maalum katika hali ambazo umelkuwa ukitarajia mafanikio na kwa fursa za jumla za kila siku. Muambane ili muwe na matazamo kuhusu fursa zilizo karibu nanyi na muwe waamifu kwa kila fiursa.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji, shiriki katika jozi, au makundi madogo na muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 10:
# KUJIZATITI KWA MWINJILISTI

**Biblia ni ufunuo wa mwaliko kutoka kwa mungu tuachane na uasi wetu na tuwe na uhusiano naye, kupitia Imani katika Yesu Kristo. Je! Tutahakikishaje hatulezei na kuwasilisha injilin nin nini tu lakini kwa ujasiri tunaita watu wajibu na kuchukua hatua b juu ya yale waliosikia?**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Mwinjilisti amejitolea kutangaz ujumbe kamili wa injili ambayo nin pamoja na au inahusisha mwaliko kwa msikilizaji kubadili mwelekeo na kupata maisha ya kweli kupitia Imani katika yesu Kristo.

## ASILI YA KIKAO

Fikiria bwana harusi mbele ya kanisa siku ya harusi yake, anatazama jinsi jingo lilivyopamvwa vizuri, limejaa marafiki na familia yake yenye msisimko kwa kutarajia kuingia kwa bibi harusi, mwanamke wa ndoto zake anapswa kufika wakati wowote. Dakika kumi zinapita bibi harusi hajafika. Bwana harusi anawaa: "ni kawaida ya bibi harysi kuchelewa" Dakika ishirini zinapita nab ado hakuna dalili zake kuonekana, acnacheka kwa woga/ wasiwasi, dakika thelathini zinaoita bna bado hakuna bibi harusi na hakuna neno ni kwanini amechelewa, sasa wasiwasi imemuingia na anaanza kuogopa, kidogo manung'uniko ya umati uliokusanyika yanaanza kuongezeka. Dakika arobaini na tano zinapita, halfu saa moja nab ado hakuna bibi harusi. Manung'uniko kati ya wageni yamefika kiwango cha juu szaidi: " Ni nini ambacho kinaendelea?, je! Kuchelewa kwake ni juu ya ujanja au mzaha, au amefanya kisichofikiriwa na kuamua kutokuja kabisa"

Akili ya bwana harusi ikileta kwa kasi sabau ambazo zinzowezesha bibi harusi kutofika, halafu kwa ghafla utambuzi unamfikia: hakuwa amempa bibi harusi posa!

Mwaliko ni muhimu iukiwa fursa unayo kwa mtu inahitaji majibu. Toleo fupi zaidi ujumbe wa injili ya yesu limeandikwa katika Marko kama ifuatavyo: "wakati umefika" alisema, "tubu kwa maana ufalme wa mungu umekaribia na amini habari njema!" Marko 1:15).

Neno "kutubu" linaweza kusababisha shida nyingi haswa kwa sababu sio watu wengi wanajua inamaanisha nini, kila wakati neno hili linahusishwa na " badilika" au "uchomwe" kama njia ya kuhibiri injili, ikimanaisha kwamba wengii husikia ndani yake tangazo la hukumu. Neno " kutubu" au " tubu" halisikiki kama neno la " habari njema" kwa watu wengi.

Lakini tunapolielewa vizuri neno" kutubu" linashikilia ufunuo wa ajabu wa ukweli wa injili, maana yake ni kuwa na badiliko la mawazo, kubadilisha mwenendon wa maisha yako. Yesu anasema kuwa: " unaelekea kwa njia mbaya, lakini kwa sababu yangu unaweza kwenda njia sahihi njia ya ukweli inayoongonza kwenye baba" Kutubu au toba ni habri njema iliyo nzuri kwa sababu inampa mtu yeyote fursa ya kujua maisha badala ya kifo, sisi wenyewe tumejiletea hukumu kwa kumuasi mungu, na kutubu au toba ni kengele ya moto, kutuonya juu ya ukweli huu na mwaliko wa kugundua tyumaini la Yesu.

Kulingana na Walter.A. Elwell na Barry.J. Beltzel kutubu au toba (uongofu) ina mambo matatu:

> "kwanza ni kugeuka kutoka kwa kitu kinachohusisha dhambi maalum, mungu au maisha ya kujipenda (1wathesolonia 1: 9; Ufunuo 9: 20,21, na 16:11), pili uongofu ni zao la mapenzi ya mungu na kazi yake ya neema ulimwenguni (Matendo 11:18; Warumi 2:4, 2Wakorintho7:10, 2Timotheo 2:25; 2Petro 3:9). Tatu, uongofu ni kugeukia mtu, kujitolea kwa maisha yako yote kwa mungu katika Yesu Kristo (Matendo 14: 15;1 Wathesalonike1:9;1petro 2: 25). kwa hivyo ni

> kujipanga teana, iwe kwa njia ya kushangaza au isiyo ya kushangaza, ghafla au taratibu, kwa kihemko au utulivu, ambapo mtu huhamisha uaminifu wake wote au utii wake wote kabisa kwa mungu."

Wahubiri wa kwanza wa injili walikuwa wa kwanza kujumuisha fursa kwa wasikilizaji wao kujibu ujumbe wao kama vile Yesu alifanya. Wito wa kutubu au toba ulifanywa kama kile cha mahubiri ya hadithi ya Yesu: (Matendo2: 37-39, 3: 25-26, 4: 12,5:31, 10:23).

Injili inatoa mwaliko kwa wanadamu waache kumkimbia mungu, kupitia imani juu ya Yesu Kristo ,tunaweza kugeuka na kukabiliana na mungu-na tunapofanya hivyo, kukubali/ kuruhusu akili/mawazo yetu kubadilishwa na ukweli wa yeye ni nani na kuona maisha yetu yamebadilishwa na nguvu ya Roho yake.

# WAKATI WA MAPATANISHO

## WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili kuweza kujuliana hali, kushiriki hadithi, maoni ya fursa, jambo lolote litakalo himiza kikundi,shiriki/jadili kuhusu zile fursa za ziada ambazo ulikumbatana nazo kulingana na kikao kilichopita (KIKAO CHA TISA: MATUMIZI).

## MAOMBI

Toa muda kwa mungu na umpe shukrani kwa guess ambazo umekuwa nazi wiki zilizopita ili ushiriki injili, ombea wale ambao wameweka imani yao kwa Yesu kupitia guess hizo.

## MAFUNZO (DAKIKA 30-40)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako.

> "Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo zao wakamwambia Petro na mitume wengine tutendeje ndugu zetu?, Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lakew Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mpatapokea kipawa cha roho mtakatifu kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili ya yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali,na kwa wote wataokitwa na Bwana mungu wamjue.'"
>
> **MATENDO 2:37–39**

Mwaliko ni sehemu ya injili kama vile msalaba. Baada ya kupata ujio wa roho takatifu wakati wa pentekoste, Petro alianza kuhubiria umati uliokusanyika. Kupitia nguvu ya roho mtakatifu iliyokuwa ikifanya kazi katika kuhibiri kwake watazamaji walikuwa " wakikatwa moyoni" waliposikia ujumbe wa injili.

Hebu fikiria ikiwa hii hadithi itachukua mtindo mwingine, ile wakati umati upo tayari kuweka imani yao kwa Yesu Petro anasema: " asanteni na usiku mwema" na kulekea pamoja na marafiki kula maalum anachostahili cha baada ya mahubiri huku umati umeachwa na uguzo wa ujumbe lakini umechanganyikiwa kuhusu namna ya kutumia ujumbe huu maishani mwao,warudi kwenye maisha yao na shughuli zao za kawaida wakiwa na maswali mengi kuliko majibu, kwa kuwa hawakupata fursa ya kutoa imani yao kwa yule Yesu kristo Petro aliwaambia,

Uzuri hicho sio kile kilichotokea. Petro alipeana mwaliko na kuwaambia watubu-akiwapa njia thabiti ya kuchukua hatua juu ya ujumbe amabo wameelewa na kuitikia wa roho waliopata mioyoni mwao. Injili kamili inajumuisha mwaliko wa toba/ kutubu na ufafanuzi wa jinsi ya kuchukua hatua juu ya kile kilichosikizwa. Wanafunzi wa Yesu walijitolea kabisa kuhubiri injili kamili, na hivyo hivyo ni lazima sisi tuwe hivyo.

Kwa wale ambao mara kwa mara huandaa mahubiri au mazungumzo mtajua jinsi ilivyo muhimu kujumuisha njia kadhaa za kutumia ujumbe wako kwa maisha ya kila siku. Mahubiri ya yesu na ya mitume yalijaa matumizi. Uwasilishaji wa kwanza wa wa injili ya Yesu katika Marko- wito wa kutubu kwa maana ufalme wa mungu umekaribia ni matumizi-anasema: " njia uliko ni mbaya unahitaji kugeuka na ushuhudie mabadiliko"

Katika ijnili zote Yesu anatoa mwaliko mara kwa mara " njooni kwangu wote waliochoka (Mathayo 11:28) " njoo uone" (Yohana 1:39), "njoo unifuate" (Mathayo 4: 19), " kila aliye na kiu

na aje kwangu anywe" (Yohana 7:37),"Njoo ule" (Yohana 21: 12).

Mialiko hii sio ya kiholelaau isiyo ya maana, mialiko hii hufunua utambulisho wa yesu kwa ulimwengu na ina hathari alisi wakati umechukuliwa au kakataliwa, kipengele kikuu cha mwaliko ni kwamba inahitaji mwitikio. Hata kukaa kwenye uzio ni kukataa mwaliko, kwa kuwa ni " ndio" tu inayoleta/ huleta kukubalika kwa mwaliko na baraka zinazofuata.

**SWALI:** Angalia mifano mitatu ifuatayo ya mialiko na ujadili kama kikundi.

### KUITWA KWA WANAFUNZI (MARKO 1:17)

Wito wa Yesu ni wa kibinafsi.

### WITO JUU YA KIJANA TAJIRI (MATHAYO 19:16–22)

Wito wa yesu ni wa gharama sana.

### WITO WA WAFU (YOHANA 11:43)

Wito wa Yesu ni wa nguvu.

Fursa ya kuitikia injili ni jambo la muhimu sana katika mahubri yetu,kutangaza injili kwa kweli ni lazima kwa kila mara tupeane nafasi ya mwaliko wa kumpokea yesu kama Bwana na Mwokozi.

Hii inaweza kuwa ngumu na fursa zingine za injili huwa bora kuliko zingine kwa kualika jibu/ majibu. Kwa hivyo kwa uaminifu tunawezaje kualika jibu katika uinjilisti wetu, katika muktadha wowote na katika hali tunayojikuta ndani? Ikwe kwenye jukwaa au mpangilio wa moja kwa moja, tunapaswa kujitolea sio tu kuwauliza watu ikiwa wanataka kuja kanisa ibaada ya jumapili tu (ingawa fanya hivi kwa njia zote) bali tujitolee pia kuwakabisha watu katika ufalme wa mungu. Hakuna mwongozo wa hatua kwa hatua kwa jinsi ya kufanya hivi katika maandiko lakini lakini kanuni hizi zinatoa mahali pazuri pa kuanzia

### ULIZA MASWALI YA MOJA KWA MOJA

Hakikisha kuwa maswali yako ni ya moja kwa moja na mafupi. Kwa mfano baada ya kuelezea Yesu ni nani na maana ya kumfuata ni nini uliza:" je! Ungependa kuweka imani yako katika Yesu Kristo leo na kuanza maisha yako katika uhusiano naye?" ikiwa ulitumia kielelezo au fumbo lililokuunganisha na hadhira yako, tumia hii kama kiini cha msingi, kwa mfano ikiwa unashiriki kutoka hadithi ya mwana mpotevu: " mungu anakuita nyumbani leo. Je! Unataka kuingia katika kumbatio la Baba kama vile alivyofanya mwana mpotevu?" swali hili linakusaidia kuona ikiwa msikilizaji yuko wazi kusema " NDIYO" kwa Yesu Kristo. Lifuatalo unaweza kuleta uwazi zaidi kuhusu jibu hilo, laiki swali lako la kwanza lazima liwe la moja kwa moja, rahisi na lililounganishwa na jumbe ambao umeshirika tayari.

### CHUKUA MUDA UNAOHITAJIKA

Unavyozungumza na umati, subiri kwa muda hadi unavyohisi kuongozwa, ili roho iguse mioyo ya watu. Sio la muhimu unachukua muda (au inakaa vibaya) cha muhimu ni kwamba watu wana wakati wakuzingatia kile kilichoshiriwa kwamba unapena nafasi ya mungu kufanya kile anachotaka kufanya. Katika hali ya moja kwa moja, inawezekana kuwa mtu anahitaji muda na nafasi ya kufikiria kwa hivyo unaweza kupanga kukutana tena wakati mwingine kujadili zaidi na kuchunguza hili jambo tena.

### WEKA/ YAFANYE MATARAJIO YAKO YAWE WAZI

Elezea ni nini kitatokea ikiwa atasema ndio/ kukubali na anaalikwa ndani ya nini. Kwa mfano mueleze kuwa mutasali pamoja ,labda kwamba mtawapa Biblia na mpangilio wa kusoma na kwamab mtawaunganisha na kanisa lako au kikundi cha ufuasi cha ufuatiliaji. Iweke wazi kuwa masiaha yao hayatabadilika mara moja na kuwa bora lakini kupitia kujitolea kwao wa kila siku kwa Yesu, utimilifub na maisha anayotoa/ anayopeana utaonekana kwa wazi. Elezea hatua zinazofuata na ukweli wa kiroho wa maisha ya ufuasi uaofuata majibu yetu ya kwanza kwa yesu.

### SHEREHEKEA UKUBALI/KUKUBALI NA UWE NA NEEMA WAKIKATAA

Ikiwa mtu anaonyesha anataka kukubali mwaliko thibitisha na kufurahi. Na furaha yako hii na Uthibitisho usiwe wa bandia. Ikiwa hufurahi kwa kweli katika jibu hili basi kuna uwezekano kuwa wito wako wa kushiriki injili sio wa kweli.

Vile vile ikiwa mtu atasema: " hapana" au "la" kwa mwaliko, kuwa na neema nya unyenyekevu. jaribu kuondoka kwa mtu anayekataa mwaliko na mwaliko wa wazi kwamba wanaweza kukubali wao wenyewe ikiwa mungu atajifunua kwao wakati mwingine. Ikiwa itawazekana wape maelezo au jinsi wanaweza kuwasiliano nawe au kanisa lililom karibu nao tukio hili litakopotokea.

Moja ya sababu za kawaida kwa nini watu hawajibu ujumbe wa injili ni kwa sababu hakuna mtu nayewauliza. Moja sababu za kawaida wainjilisti hawapeani mwaliko ni hofu kuwa hakuna mtu atakaye jibu na kisha wao (au injili) wataonekana wajinga. Lakini nguvu ya wokovu sio yako hata Yesu alikuwa na watun waliokata mwaliko na kuenda zao. Tuinaitwa tu kuwa waaminifu kwa ujumbe wa injili, mwaliko na yote, na chochote kile kinachofuata. Kwa kweli mwaliko wa Kristo ni kwa sisi kuja na kufa kwa nafsi zetu, kuchukua msalaba na kumfuata. (MATHAYO16:24)

Hii iinamaanisha kufa kwa nafsi yako katika uinjilisti pia licha ya gharama na jinsi tunavyokaa wajinga. Yesu na mitume walitoa mwaliko wakati walihubiri injili na sisi pia ni lazima tufanye hivo licha ya jibu tunaweza kuhakikishiwa kuwa tumekuwa waaminifu kwa ujumbe wa injili na wito mkuu wa kutubu na kumwamini Yesu Kristo. Mungu atayashughulikia mengine.

## MAJADILIANO (DAKIKA 15)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! Inawezekana kuhubiri injili kwa kweli bila kutoa mwaliko na jibu kwa imani katika Yesu?
- Je! Ni nini unapata rahisi/ ngumu juu ya kipengele cha mwaliko na jibu katika uinjilisti?
- Je! Umejifunza nini kuhusu jinsi ya kuwasaidia watu kutoa jibu kwa injili kama ilivyoinjilisha?

> "injili ni wito wa mungu kupitia tendo la kumhubiria msikilizaji ili kufanya uamuzi utakao muingiz katika mwelekeo mpya wa kuishi."
>
> **MICHAEL GREEN**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

Kuwa na nia ya kutoa mwaliko wa kuitikia injili kila wakati unavyoshiriki injili, labda wewe ni mhubiri jukwaa ambaye amekuwa akihangaika katika eneo hili. Jaribu njia tofauti za kiuta majibu kutoka kqwa hadhari yako, usiogope kuokekana mjinga/ mpumbavu ikiwa hakuna anayejibu. Vile vile unaweza kuwa mtu anayefaa katika kuanzisha na kufanya mazungumzo na watu juu ya yesu lakini kuunganisha hatua zifuatazo ni vigumu. Jitoe kwa ujasiri huu mwezi na uliza angalau mtu mmoja baada ya mazungumzo yaliyozingatia injili ikiwa wanataka kumwamini yesu.

## MAOMBI

Shukuru mungu kwa mwaliko anaotupa sisi kuunganishwa na yeye, muombe akupe ujasiri unaposhiriki injili na kwamba tutakuwa wazi na wajasiri katika kuwaita watu watubu na kuwasaidia kuona matumaini na sio hukumu, omba kwamba mioyo itaweza kukubali mwaliko huu.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 11:
# MSUKUMO WA MWINJILISTI

**Kama wainjilisti kazi yetu sio tu kuhubiri injili kwa waliopotea bali pia kuchochea kanisa kwa uinjilisti. Katika kikao hiki tutachunguza jinsi tunaweza kuwa wainjilisti wa moto wa uinjilisti kanisani., ili kuwasaidia na kuhimiza au kuwaandaa waliotuzunguka ili wawe waaminifu kwa mungu katika uinjilisti.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI:

Pamoja na kutangaza injili kwa ulimwengu, mwinjisti pia atajitolea kuchochea kanisa kwa uinjilisti kwa kuwatia moyo na kuwapa vifaa ambazo watakatifu wanahitaji kwa kazi ya utumishi.

## ASILI YA KIKAO

Tukirudi nyuma katika kikao cha pili cha kikundi hiki cha Advance/utangulizi tukiwa bado katika hatua za mwanzo za safari ya kikundi cha Advance tulielezea utambulisho wa mwinjilisti kama mtoto mjumbe wa baba yetu wa mbinguni. je! Tuna jukumu gani kama wainjilisti sio tu kwa ulimwengu lakini pia kwa familia yetu wenyewe (kanisa) tangu ufumbuzi wa mitandao wa kijamii aina mpya ya mtu mashuhuri imeibuka - mtu anayeitwa" mshawashi " hawa ni watu ambao wamejenga/unda wafuasi katika mitandao ya kijamii (haswa Youtube) kwamba wanaweza kuwashawishi watu wengi sana. Hio sio dhana mpya kabisa, kwani kuna watu mashuhuri kutoka ulimwengu wa michezo na burudani wamekuwa wakituambia kupitia matangazo ya biashara ni nini ambacho tunafaa kuvaa,kula, kunywa na jinsi tunafaa kunukia. Lakini kizazi hiki cha watu mashuhuri ni cha kwanza kuweza kupata wafuasi kwa sabau ya ushawishi pekee yake.

Paulo anatueleza katika Warumi kwamba tusifuatishe namna ya dunia hii bali tugeuzwe kwa kufanya upya nia zetu kwa kutii roho mtakatifu (WARUMI 12:2). sisi ndio washawishi asili walio na ujumbe wa maisha ,uhuru na tumaini kama watu watakatifu wa mungu.

Katika kikao cha saba ,tulijikumbusha kwamba vhumvim isiyo na ladha haina maana na sio nzuri. nguvu ya mshawishi katika mitandaon ya jamii imeegemea sana kwa nambari ya wafuasi na jinsi wanavyoshiriki kwa chochote wanachotangaza. Kwa kanisa tofauti nyetu ni ya muhimu sana na kuipoteza ni gharama kubwa zaidi. Mshawishi ma mtandao wa kijamii anaweza kupoteza umaarufu wake na taaluma/ kazi yake kadri ushawishi wake unavyozidi kufifia. Lakini ikiwa kanisa litafifia kwa nguvu yake ya ushawishi na kupoteza utofauti wake basi ulimwengu utakosa fursa ya kuona injili ikiishi na fursa ya kuisikia ikitangazwa kwa njia ambayo wnaweza kuilewa.

Mwinjilisti ana shauku na upendo wa kuona ulimwengu ukipokea injili, lakini pia lazima tuwe na shauku ya kuendelea kuchochea kanisa liwe na ushawishi wa injili duniani/ ulimwenguni kwa maana " hakuna mpango wa pili au Ba" pale ambapo injili unahusika na kanisa la Yesu Kristo ni mabalozi wake tu. Wakati wowote ambapo kanisa linasahau hili ama linavurugwa, wainjilisti ni lazima kwa upendo kuongeza mafuta na kupepeta moto wa uinjilisti mara nyingine tena ili ushawishi wa injili uweze kung'aa sana ili wengine waweze kuona.

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili muweze kujuliana hali, kushiriki injili na kuhimizana na maoni nkuhusu fursa na lolote lile litahimiza kikundi. Shiriki kuhusu

kuwaita watu kujibia injili kulingana na kikao cha awali (KIKAO CHA KUMI; matumizi)

## MAOMBI

Toa muda kwa mungu na uombe juu ya jambo lolote zuri na choichote kiulichoangaziw wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za kufundisha kwa njia yako mwenyewe ama kwa kuisoma neno kwa neno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako mwenyewe.

> "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu. Kwa kusudi la kuwakamisha watakatifu hata kazi ya huduma itendekwe hata mwili wa Kristo ujengwe. Hata sisi tunapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa mungu, hata kwa mtu mkamilifu hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utmilifu kwa Kristo."
>
> **WAIFESO 4:11-13**

Hata wale ambao wana jukwaa kubwa wanahitaji msukumo fulani katika maisha yao, kama vile shujaa wa filamu/cinema za mate do kule Hollywood Dwayne "The Rock" Johnson alivyosema: " Nilipokuwa until wa miaka nane millions filamu ya Waramizi wa Safina iliopotea/ Raiders of the Lost Ark" kule Charlotte Carolina Kaskazini, nilitembea kule nje na nilikuwa na msukumo Sana,nilifurahia/nilipenda Filamu hiyo na nikajua ninataka kuwa huyo mtu"

**SWALI:** Je! Umewahi kukutana na mtu ambaye ana msukumo sana hivi kwamba ulitamani mara moja kufanya/kuwa kama yeye? Ni nini ambacho walikuwa wakifanya au walijihusisha nacho kilicho kuwa na athari hii kwako?

Iwe ni kwa mwanafamiia, mwanamzuki mashuhuri wa miziki ya pop,au hata mhusika wa uwongo tunaweza kupata msukumo katika kila aina ya maeneo. Baadhi ya msukumo huathiri burudani zetu na hata kazi tunazofuatilia na kutaka kufanya na zinaweza hata kuunda tabia zetu na mtazamo au maoni yetu kuhusu ulimwengu. Wakati mwingine msukumo hufanya kazi kwa njia nyingine pia. Unaweza kuona mtu ana kipaji sana hadi inakuvunja moyo wa kufuta kitu:" kuna maana gani yakulifuatilia hili jambo siwezi ni kama mzuri zaidi au kama wao"

Kuna watu wa kibiblia wenye msukumo na vizuri kutazama mashuja hawa wa imani ndani na nje ya kurasa za Biblia haswa tunapogundua licha ya uvutio walio wao wa likuwa watu wa kawaida tu waliokuwa/wakiwa waaminifu kwa mungu.Kujua kwamba kwa sababu ya Musa kusema kwa nguvu na ujasiri mbele ya Farao haikuhusiana na ustadi wake usemi ila ilikuwa sababu ya uaminifu wake kwa wito wa mungu na kujiitisha kwa nguvu zake kunatia moyo na kupeana msukumo. Mungu ni yule yule tu kwa hivyo tunaweza kufanya yale walifanya.

Mwishowe kuna mmoja tu ambaye anaweza kutuhamasisha na kutuwezesha ,katika Yesu tuna mfano kamili wa vile maisha yetu yanafaa kuwa, yanapaswa kuwa na nguvu kamilifu amabyo tunaweza kutumaini kushi kwa njia kama hiyo.Yunavyolazimishwa na mfano na mafundisho ya yesu Kristo na kadri ya imani, tunapaswa kuzingatia ushawishi ambao tunaweza kuwa nao kwa wale walio karibu yetu.

Paulo anafundisha katika Waefeso kwamba Yesu alibariki kanisa na vipaji tofauti ambazo ni muhimu kwa malengo yake ya ufalme, wainjilisti wameorodheshwa pamoja na mitume, wachungaji waalimu na manabii, na Paulo anasema kuwa watu wana vipaji vya kutimiza miito hii ni kwa kuandaa kanisa kwa kazi za huduma za kujenga mwili wa Kristo au ujenzi wa mwili.

> "...mahali kwingine wazo liliibuka na kuwa maarufu sana katika jamii ya wakristo.. ni kwamba huduma ya kanisa inapasawa kufanywa na makasisi wanaolipwa, wenye taaluma na waliofundishwa kitheolojia. Kulingana na maoni haya kusudi la walei ni kupokea faida za huduma kwa upande wa mahubiri, uhauri, faraja na vitu vingine ambavyo tunatafuta kupata kwa kanisa. Lakini sababu ambayo karama fulani hutolewa kwa uongozi ni kuandaa waumini kwa huduma, kanisa linafaa kuwa jeshi lililohamsishwa."
>
> **R.C. SPROUL**

Ingekuwa kosa kungalia majukumu ya huduma katika Waefeso nne na kuhitisha kwamba wanataja kikundi cha watu maalum katika makanisa yetu. Barua ya Paulo inaonyesha kitu bora zaidi. huduma hizi zipo kwa sababu kanisa ni maalum na mungu anafanya kazi kwa njia ya watu wa kawaida ili kuhakikisha unakuwa kwa ukomavu kama mwili mmoja. Tunawajali wale walio katika jamii yetu wakati pia tunawafikia wale walio nje ya jamaa, kila mtu na jukumu la kucheza.

Tuma jukumu la kutumia vipaji vyetu vizuri na hiyo inamaanisha kuwa na maksudi juu ya kuwa na msukumo, inamaanisha pia kwamba kwa unyenyekevu na utukufu tuliochunguza katika vikao vilivyopita, lazima tuongoze njia ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya ya vipaji/karama hizi ambazo zinaweza kusababisha mgawanyiko kanisani, kiburi,ubinafsi, wivu na matumizi mabaya ya madaraka ni njia za makato za kugawanya.

**SWALI**: Ni nani katika kanisa lako anaweza kuwa msukumo, na kwa kuzingatia hilo na majukumu na kazi gani unaona watu wanatamni kanisani leo? Labda ni kuwa mchungaji, au mfanyikazi wa vijana, kiongozi wa ibda, au mwalimu wa Biblia. Je! Kuna watu ambao wanataka kushuhudia na kuinjilisha na ikiwa sivyo ni kwa nini?

Hapa kuna njia nne ambazo tunaweza kujaribu kuhamasisha watu wengine washiriki injili kwa uaminifu.

### 1. TANGAZA INJILI

Njia moja bora ya kuhamasisha watu kushiriki injili ni kufanya hivyo mara kwa mara katika mikusanyiko yetu. Njia ingine ni katika kuwaalika ndigu na dada zetu wa kikristo katika mikutano yetu kuja kwenye hafla ambazo tunahubiri- sio kwa msaada wao wa maombi tu lakini pia kujenga imani yao kwani wanaona nguvu inafanya kazi wtuinjilisti ni fursa/upendeleo wa waumini wote.

### 2. TAYARISHA USHUHUDA

Kusaidia watu kufikiria kupitia ushuhuda wao na ni athari ambayo mungu amekuwa nao maishani mwao hivi karibuni. Kuandaa kwa maksudi ushuhuda wa kibinafsi ni njia nzuri ya kuhamasisha na kuandaa kila mmoja kwa uinjilisti na ni tendo la ibada tunapomshukuru mungu kwa kile alichokifanya katika maisha yetu.

### 3. WEKA USILIMUZI WA HADITHI KIPAUMBELE

Katika mikusanyiko yetu na mazungumzo tupaswa kushiriki mara kwa mara hadithi zetu za uinjilisti/uinjilishaji. Kusherehekea na kuhimizwa unapoona mungu akifanya kazi kupitia wewe/kwako na uchague kufikiria mema na mawazo ya kujenga juu ya kile ambacho unaweza kujifunza katuka kwa hali hizi kuonekana kwenda vizuri. Jamii yako inaposikia hadithi za mungu akifanya kazi kupitia watu wa kawaida kama wao watakuwa na ujasiri kwamba mungu anaweza kuwatumia pia,

### 4. PEANA/TOA FURSA

Kupitia kanisa lako na kikundi chako cha marafiki/urafiki andaa nafasi ya kushiriki katika uinjilisti, panga fursa za misheni ndani na nchi na nje mwa nchi/kimataifa, waalike watu wawe sehemu ya timu yako ya huduma katika hafla unazoendesha au chukua marafiki wachache kwa masaa kadhaa kwa unjilisti wa barabarani, njian ambazo unawqeza kufanya hivyo ni nyingi peana mafunzo kabla ya kwenda na m ujadili maoni wakati mutakapo rudi,baadyae watu watakuwa na uzoefu wa kuchukua fursa hizi “rasmi” katika maisha yao ya kila siku, uinjilisti wao utahama kutoka kwa “ wiki ya misheni” iliyopangwa na kwenda kwenye fursa za kila siku.

Walakini jinsi tunaendelea kufanya kama wainjilisti ni lazima tujitume kuchochea na kusaidia ndugu zetu katika Kristo kuingia utimilifu wa kitambulisho chao kama watoto wajumbe wa Mungu.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! inamaanisha nini kujenga kanisa kwa njia ambayo Paulo anaelezea katika Waefeso?
- Je! Ni vipi tunaweza kudumisha upambanuzi wetu ulimwenguni kama Wafuasi wa Yesu na kanisa kama wafuasi wa Yesu na kanisa kama wainjilisti wenye shauku?
- Je! Zaidi ya njia nne ambazo tumechunguza na kujadili katika kikao hiki, tunawezaje kuhamasisha wengine kwa uinjiliksti?

> "ninyi ni nujru ya ulimwengu, mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima, wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi bali juu ya kiango; nayo ya waangaza waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru iangaze mbele ya watu wote wapate kuayaona matendo yenu mema wa mtukuze Baba yenu aliye mbinguni."
>
> **MATHAYO 5:14–16**

## MATUMIZI (DAKIKA 10)

Nina matumaini ya kuwa utakuwa na hamu ya kukaa kwenye kikundi hiki zaidi ya mwisho wa mwaka wa kwanza na kuendelea kusafiri kwa pamoja, kukua kama wainjilisti,lakini pia kulitia kailini msukumo wa kanisa kwa uinjilisti. Sasa ni wakati wa kuanza kufikiria jisni itakavyokuwa ukiongoza kikundi chako mwenyewe cha Advance.

Kuzidisha ni kanuni ya msingi ya harakati ya advance, kwa sababu hamu yetu kama wainjilisti ni kuhamasisha wengine katika uinjisti wao. Kwa hivyo nchukua orodha ya watu ambao wanaweza kupendezwa na kufuata safari ile ile ambao wewe umekuwemo na uanze kuwafikia kwa kuwasiliano nayo kwa wiki zijazo. Tumia uzoefu wako kutoka kwa kikundi hiki na rasilmali za Advance ziweze kukusaidia kupanga kikundi chako.

## MAOMBI

Tumia muda kuombea kanisa la mahali hapo ulipo ili wote walio ndani nyake wawe waaminifu kwa wito wa injili juu ya maisha hya. Ombea juu ya fursa kuwa kuwa himiza wengine na omba juu ya kumwamuru kila mshiriki wa kikundi asitangaze tu injili kwa ulimwengu ulio na hitaji lakini kuwahamasisha na kuandaa wafuasi wengine wa yesu kufanya viyo hivyo.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji jadili na mshiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# MAANDISHI

# KIKAO CHA 12: FARAGHA

**Kilele cha mwaka wa kwanza wa kikundi cha Advance ni kutumia faraghani. Jinsi unavyoamua kuifanya ni juu yako. lakinin hapa utapata maoni juu ya jinsi kutumia wakati wa pamoja kwa kuzingatia kanuni za jumla za mikutano ya kikundi cha Advance na kumaliza mwaka wa kwanza wa Advance na lengo.**

## JINSI YA KUENDESHA/ KUONGOZA FARAGHA YA KIKUNDI CHA ADVANCE

Wazo la jumla ni kutoka kwenye eneo la kawaida na kutenga muda zaidi kuliko inavyokuwa wakati wa vikao vya kawaida vya kukundi. Ikiwa unaweza tenga asubuhi alasiri au jioni basi fanya uwezavyo kwa wakati huu, lakini ikewezana kwenda faraghani siku nzima kuna faida zaidi. Hapa kuna maoni ya nini cha kufanya wakati wa faragha huo.

### ANDIKO MUHIMU

Kufungu kifuatacho kutoka kwa Wakolosai kitafanya kama maandishi muhimu kwa wakati wenu pamojha na ikiwa unafuta lengo moja maalum wakati wa faragha:

> "dumuni kabisa katika kuomba, mikikesha katika kuomba huku na shukrani. Mkituombea nasi pia, kwamba mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo ambayo kwa ajili yake nimefungwa; ili ni dhirihisho kama inpasavyo kunena. Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje,mkiukomboa wakati waneno yenu yawe na neema siku zote yakikolea mungu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu."
>
> **WALOKOSAI 4:2–6**

Ndani ya kifungu hiki kuna mamb o kumi na mbili ambao yanaweza kuchunguzwa na kuthibitishwa kwa uinjilisti wetu:

1. Moja: Jitolee(jitolee kwa maombi)
2. Mbili: hamasisha ushirika wa kiroho (mutuombe pia)
3. Tatu: tegemea mungu (mungu afungue milango)
4. Nne: jitolee kutangaza injili(tanganza siri ya Yesu)
5. Tano:tamani uwazi (ili niweze kuitangaza wazi)
6. Sita: kubali kujitolea kwa ajili ya injili (ambayo nimefungua kwenye minyororo
7. Saba: tegemea hekima kutoka kwa mungu(kuwa na hekima)
8. Nane: chukuan fursa (tumia vyema kila fursa/fursa zote)
9. Tisa: zungumza na sikiza (mazungumzo)
10. Kumi: kuwa na neema na unyenyekevu (daima unejaa neema)
11. Kumi na moja:kuwa tofauti/wa kipekee (iliyoekwa chumvi)
12. Kumi na mbili: jitayarishe (ili uweze kujua jinsi ya kumjibu kila mtu).

Jinsi unavyojifunza kifungu kwa pamoja aub pekee yako(angalia hapa chiini), jinsi unavyoelezea na jinsi unavyojadili pamoja ni juu yako, ikitegemea muda wako wa faragha, ongeza muda wa faragha. Laklini weka kifungu hikl akili unapotazazama/anagalia hapa chini.

### NENO

Lengo kuu la kundi la Advance ni kusaidiana kukua kama wainjilisti waliojitolea kwa neno la mungu.

### KUSOMA BIBLIA ZAIDI

Muda uliongezwa zaidi kwa neno la mungu haujawahi kuwa muda uliopotezwa. Kuchukua muda ili kusoma injili yote ya Marko au barua moja katika Agano Jipya katika kikao cha mbelew ni jambo la muhimu sana ya kupata mtazamo kamili juu ya yaliyomo kwenye kitabu hicho. Ikiwa ni kitabu ni kupi mbona usikikisome mara kwa mara hukui ukiomba na kutafakari kati ya kila somo kuandika chini maelezo na kisha kusoma tena, wote wanaweza kuchagua kusoma kitu kimoja au uwe na chaguzi tofauti ambalo watu wanaweza kusoma kisha wakubali kushiriki kuhusu muda wao wa binafsi wa kusoma na kutafakari.

### FUNZO LA BIBLIA

Kuna njia tofauti ambazo unaweza kutumia kuongoza funzo la Biblia kwa pamoja wakagti wa faragha. Labda utataka kupitia tena vifungu muhimu ambavyo umechunguza wakati wa vikao vya kundi la Advance. La sivyo unaweza kuhisi kuongezwa kwa kifungu fukani au mada ambayo itawaongoza wakati wa faragha. Kama ilivyo wakati wowote hakikisha inalingana na kukuza kila mmoja kama mwinjisti.

### VIKAO VYA ZIADA NA RASLIMALI NYINGINE ZA ADVANCE

Moja au mbili ya vikao vya ziada katika mwongozo niaweza kutumiwa kuendesha/ kuongoza kikao cha kawaida cha kundi la Advance kama sehemu ya faragha yako, unaweza pia kuwa na maoni jinsi unavyoweza kuendesha kikao cha kundi la Advance kwa kutumia muundo ay njia ile ile ambayo tumekuwa tukitumia lakini yaliyomo yawe yako mwenyewe. Hapa chini kuna maoni machache ju ya mada ambayo unaweza kuchunguza na kikundi chako

- Utatu
- Ufalme wa mungu,
- Msalaba
- Ufufuo
- Matunda ya roho
- Kuabudu na uinjilisti

### KUSHIRIKI NA IMANI ZINGINE

Vile vile unaweza kutaka kuangalia blogi kitu kimoja (ONE THING) kwenye tuvuti ya Advance (advancegroups.org) ambayo ina wainjilisti kadha tofauti wakielezea jambo amabalowangependa wangelijua wakati ambapo walikuwa wameanza kuhibiri injili, vipande hivi vifupi vizuri vya kuanzia majadiliano.

### RASLIMALI MPYA

Tunatumahi kuwa utataka kuendelea kama kikundi zaidi ya mwaka wa kwanza. Njia ingine ambayo unaweza kukisaidia kikundi na rasilmali zaidi ni kusoma vitabu kwa pamoja kati ya vikao na wao kulenda mafundisho na majadialiano kulingana na waliosoam. sehemu ya usomaji uliopendekezwa mwishoni mwa mwongozo huu (ukurasa wa 88-89) utakupa chaguzi nyingiu zaidi. Lakini neno lenye herufi zito limedhihirishwa na kuangaziwa kuwa muhimu sana kwa sababu ni fupi somo mada husika na unahusisha maswali ya majadiliano.

## MAOMBI

Ukiwa faraghani tenga muda wa maombi, panga nyakati za maombi ikiwa na umakini wakati wa kuomba kwa kutumia maandiko na maombi ya hiari. Chochote kile/kingine utafanya/ unafanya katika maombi sehemu hizi tatu zimependekezwa.

### KUOMBEANA

Hakikisha kuwa kuombeana ni msingi wa wakati wenu pamoja. Waulize watu washiriki sehemu ambazo wanahisi wamshukuru mungu na sehemu moja ambayo wnahitaji msada au mafanikio. Himiza watu wawe mahsusib na waaminifu katika maombi yao na usiwaharakishe ila toa muda halisi kwa kila mmoja. Hakikisha unaandika chini maneno yanoyo himiza.

### KUOMBEA WA NDANI (SEHEMU/NCHI ULIYOMO NA KIMATAIFA .

Chukua muda ili uweze kuombea mazingara yako ya ndani na kuenea kwa injili ulimwenguni. Ikiwa kuna hali yoyote maalum ambayo unahisi mshinikizo wa roho kwa mazingara ya ndani na mazingara ya nche / kimataifa basi uiombee. Inua watu binafsi, makanisa, hali

huduma wamishonari hali kutokana na habari na kadhalika

### KUOMBEA SAFARI YA ADVANCE/ UTANGULIZI

Shukuru kwa safari uliyokuwemo katika kikundi hiki, tafakari juu ya ukuaji wa kibinafsi na hadithi za kuzaa matunda na wokovu. Mwombe mungu aendelee kazi iliyo ndani mwako na kwamba ubadilishwe katika sura yake na utukufu unaozidi kuongezeka (unaweza kuomba kupitia 2WAKORITHO 3:17-18)

## MAABUDU/IBADA

Wakati wa maabudu uliotumiwa katika neno la mungu, maombi na ushirika yote ni sehemu ya ibada. Lakini tumia muda huu katika vitendo maalum vya maabudu ya kujitolea. Iwe ni kwa nyimbo au njia nyingine ya ubunifu.

### IBADA YA NYIMBO/ MAABUDU YA NYIMBO

Ikiwa kuna mtu ambaye ana kipajai cha mziki,mwalike kuongoza wakati wa ibada ya kuimba, la sivyo kuna programu na video nyingi za ibada ya ushirika mtandaoni(Youtube) ambazop nyingi zao ni bure. Utaftaji wa haraka kwenye Youtube wa nyimbo unazozipenda za ibada/maabudu unaweza kuleta tolep la wimbo na maneno ambayo yanaweza kuchezwa kwa kikundi na waimbe kwa pamoja. Kuna nguvu katika watu wa mungu kuungana kwa pamoja kwenye nyimbo na kutangaza utukufu wake.

### KUAGIZA

Njia ingina ambayo unaweza kushiriki ibada katika ibada ya ushirika itakuwa kuamuru kila mtu mbele za mungu kwa kazi ya Uinjilisti ambayo amekuita na kukupa nguvu.mwishoni mwa mwaka wa kwanza wa kundi la Advance litakuwa jambo la kuhimiza na uthibitisho kutambua hatua hii muhimuj. Kwa hivyo mshukuru mungu kwa jambo hilo muombeane mnapotazamia kwenda tena na injili ya wokovu kwa dunia na kwa utukufu wa mungu.

## USHIRIKA

Tunapokusanyika pamoja tunakuwa b katika urafiki wa kuaminiana. tunatumaini kuwa ushirika wa kundi lako la Adance umekuwa wa baraka kwa kila mtu na faragha munaweza endelea katika kujitoea kwenu kuhakikisha kila mmoja wenu anawajibika na furuhia uandamani wa mmoja na mwenzake ua uandamani wa kila mmoja.

### KUAJIBIKA/UWAJIBIKAJI

Uwajibikaji umekuwa sahemu ya msingi nya kila kikao hadi sasa na katika kikao hiki cha mwisho wa mwaka, jitolee tena kwa mchakato huo huo kuhakikisha unaishi maisha matakakatifu na kwa unyenyekevu.

### KUFUNGA/KARAMU

Unaweza taka kutoa muda ma mafungi kama sehemu ya faragha ama wakati mabapo mumekusanyika pamoja wakati wa chakula / mamkuli na kutenga nafasi ya majadiliano. Hakuna njia maalum ya kufanya hivi. Cha muhimu mni kwamba unakusisaidia kutimiza malongo ya faragha

### SHUGHULI

Unaweza taka kupanga shughuli ya pamoja kwa mfano ikiwa faragha yako ipo kwenye bustani mahali nendeni mukatembee na ongezea shughuli zingine za ibada katgika wati/muda huu. Ikiwa imemejikita katika mazingara ya mjini munaweza kutembelea nyumba ya sanaa na kufanya lile lile kwa kutumia kama kichocheo cha kutafakiri na maabudu.

Hivyo hivyo unaweza taka kufanya jambo la kujifurahisha kwa pamoja-,shughuli ya timu, michezo, chaguo burudani nakadhalika. Ikiwa ni ushirika ka kuhimiza, maabudu, au ushirika wa k,ufurahia urafiki na kukua katika uhusiano

na kila mmoja. Wekeza kwa wakati mzuri na kila mmoja.

## HATUA ZIFUATAZO

Mwaka wa kwanza wa Advance umemalizika kabla ya kumaliza mwaka na faragha hakikikisha umeangalia hatua zifuatazo la kundi hili na makundi mapya ambayo yatazinduliwa kutoka kwa kikundi hiki.

### KIKUNDI HIKI

Tengeneza nafasi ya watu kushiriki jinsi safari yao ya dvance imekuwa. Toa maoni jinsi mumekua na kuendelezwa na fikiria funzo kubwa limekuwa kutoka sehemu gani huu mwaka huu. Himizaneni katika mambo haya.

Ikiwa bado haujajitolea kuona kikundi kinaendelea uliza kila mtu ikiwa wangependa kuendelea na wape watu chaguo la ikiwa wanahitaji au la. Ikiwa upo na watu wakutosha wa kuendelea na safari pamoja basi kwa pamoja mjadili na mupeane majarajio yenu kwa yale ambayo mtakuwa mkifanya kwa pamoja miezi ikayofuatiya. (ni raslimali gani mpya /nyenzo za mafundisho utakzo tumia katika, ikiwa masaa ya mikutano ibaki vile vile. Omba nashukuru mungu kwa mwaka wa kwanza wa Advance na mkabidhi Bwana yote yalio mbele.

### MAKUNDI MAPYA

Inastahili pia kufuatilia ili kujua maendeleo ya makundi mapya ambao yalianzishwa kwenye kikao cha awali. Fuatiilia kujua jinsi kila mutu anavyoendelea na kuuliza watu wajiunge na makundi mapya.ikiwa wataanzisha moja na ombea vikundi vipya .

Wakati unaendesha wakati wenu wa faragha, zingatia maadili msingi ya kundi la Advance. Tafakari safari muliyokuwa nayo kama kikundi, shukuru mungu kwa ukuaji na uzaaji matunda katika safari hiyo na ukabidhi wakati ujao kwa mungu

# VIKAO VYA ZIADA

# KIKAO CHA ZIADA CHA KWANZA: UINJILISTI WA MAZUNGUMZO

**Kikao hiki kinachunguza umuhimu wa kutumia kila fursa kushiriki habari njema, sio zile zinazotolewa kutoka kwa jukwaa tu.**

## KIKAO KATIKA SENTENSI

Mazungumzo mengi ya injili duniani/ ulimwenguni kufanyika kwa njia ya kibinafsi kupitia mazungumzo. Kwa hivyo ni lazima tuwe tayari kushiriki injili kwa uwazi katika fursa yoyote amabyo mungu anatoa sio tu kwa wakati tuna nafasi ya kuhubiri kutoka kwenye jukwaa.

## ASILI YA KIKAO

Huwa tunajishughulisha na mazungumzo kila siku na mengi ya mazungumzo haya ni ana kwa ana, lakini kupitia teknolojia tunaweza sasa kuzungumza na watu kwa njia tofauti ulimwenguni kote kwa wakati halisi. Wakati mazungumzo haya ya kidigiti hayawezi kutoka kiwango sawa cha unganisho la kibinafsi kama kukutana na kwa ana katika chumba kimoja, zimekuwa njia za kawaida na thamani sana kuungana na marafiki na wageni.

Kuhubiri kwenye jukwaa au kutoka kwa jukwaa haitoi nafasi nyingi kwa mazungumzo mara nyingi inaokenakan kama kutangaza ujumbe wetuna kutumaini itakita mizizi katika mioyo ya wasikilizaji wetu. Hata hivyo katoika mazungumzo kuna nafasi ya kuhoji, kujenga uhusiano na nafasi ya kusikiza. wakati mwingine ujumbe wa mwelekeo au mfumo mmoja unaosikika kutoka kwa jukwaa unaweza kukataliwa ilhali mazungumzo ya kibinafsi hutoa nafasi kubwa ya kuzungumza na kutoa maelezo zaidi ya moja kwa moja kwa waiwasi wa msikilizaji.

Sio utangazaji wote wote wa injili unatoka kwenye jukwaa kwa kweli wakati mwingi katika injili yesu alizungumza na watu kibinafsi kuliko akihuburia umati/ halaiki ya watu." unataka nikufanyie nini?" Yesu anamuuliza Batimayo (MARKO 10: 51) " Nataka kuona" ni jibu rahisi linalodhirihisha hitaji lake na pia imani yake ya kwamba Yesu ana uwezo wa kuleta uponyaji. Mkutano huu wa moja kwa moja haitoi malelezo ya injili lakini inampa Yesu nafasi ya ya kugundua na kukidhi mahitaji/ hitaji la yule anayemtafuta, ambaye anahama kutoka kwa upofu kwa upofu na kwenda kwenye ushirika.

Hata Filipo mhusika mmoja wa kiBiblia kubeba jina la " mwinjiliksti" anaagizwa na malaika wa Bwana kuhudumu mmoja kwa mmoja na towashi wa Ethopia akiwa katinya misheni ya kuhubiri misa (Matendo 4:26-40). Kwa wafasi wengi wa yesu kushiriki injili kutatokea kupitia mazungumzo ya kibinafsi na wanafamilia,marafiki wenzako (wafanyakazi) na hata wageni kabisa. Viangazo vikuu katika huduma vinaonyesha kwamaba yesu na wainjilisti wa kwanza walikuwa wamejiandaa kikamilifu kushiriki habari njema kwa umati na kwa mtu mmoja kwa mmoja. swali ni je? Tupo tayari kufanya hivi?

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili muweze kujuliana hali, kushiriki hadithi, faraja/kuhimizana maoni kuhusu fursa na kitu chochote kitakacho hikiza kikundi. Kwa makundin madogo uliza kila mtu ashiriki ushindi mmoja na jambo moja analom pambana nalo au anapata kuwa changamoto kwake. Kwa makundi makubwa chagua watu wanne au watano watoe/ washiriki ushuhuda maalum tangu mkutano uliopita.

## MAOMBI
Peana muda kwa mungu na uombe kuhusu hali yoyote nzuri au changamoto ulioangaziwa wakti wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)
Tumia nyenzo zifuatazo za mafundisho kwa njia yako mwenyewew aidha kwqa kuisoma neno kwaneno au kuifanya upya katika uwasilishaji wako.

> "mara hiyo wakaja wanafunzi wake, walistaajabu kwa kuwa alikuwa akisema na mwanamke; lakini hakuna aliyesema, unafatuta nini au ombona unasema naye. Basi yule mwanamke akawacha mtungi wake akaenda zake mjini akiwambia watu" njooni mtazame aliyeniambia mambo yote niliyotenda. Je! Hamkini huyu kuwa ndiye Kristo. Basi wakatoka mjini na wakamwendea."
>
> **YOHANA 4:27–30**

Je ni lini uliongea mara ya mwisho na rafiki yako asiye Mkristo kuhusu imani yako? Au mtu mgeni wainjilisti wengi wanaohubiri wanaweza kupata ushuhuda wa kibinafsi kuma ngumu, lakini wape jukwaa na kipaza sauti na watahubiri siku nzima, lakini wakati unashinikizwa na roho mtakatifu uzungumze na mgeni katika mkahawa inaweza kuwa hadithi tofauti sana.

**SWALI:** Je! Ni kwa nini wengine ambao wanaweza kutangaza kutoka kwa jukwaa hujitahidi katika mikutano ya moja kwa moja. Je! Unastawi au unajitahidi katika hali za moja kwa moja?

Yesu anapendekezwa na maisha ya mtu binafsi, ingawa alichukua muda mwingi kuhuburia umati wa watu, agano jipya linaonyesha mara kwa mara akishiriki mazungumzo ya moja kwa moja na watu aliokutana nao katika safari yake ya huduma, na wengine ambao kwa maksudi walimtafuta. Iwe akihubiria umati wa watu wenye hamu ya kusikiza maneo yake, kwa watu wa deni wenye hasira wakijaribu kumnasa ama kwa watu anuwai- matajiri na maskini, waume na kike, wagonjwa na wenye afya, wa dini na wasio wa dini yesu alionekana kuwa na urahisi wa kuwasilisha ujumbe wake.

Yesu napokutana na mwanamke Msamaria katika Yohana nne, kuna mambo mannne muhimu tunapaswa kutambua.

### 1. KUWA TAYARI KWA MKUTANO
Kwa mwanamke msamaria mkutano huu haukutarajiwa kabisa, na haukufaa lakini yesu yupo tayari kuzungumza na yeye na anaanzisha mazungumzo haya kutokana na haja yake ya kimwili ya kutaka maji. Je!, ni mazungumzo mangapi ambayo yanaweza kuanzishwa kutoka kwa mahali petu pa haja au mazingara maishani mwetu? Fundi anayeingia nyumbani mwako ili kurekebisha mfereji wa maji, yule mama mboga au mfanyikazi sehemu ya kula, daktari anayekupa utambuzi mgumu? Tumezungukwa na fursa nyingi za sisi kuzungumza na wakati hizi mikutano zinaweza kumshangaza mtafutaji ni lazima tuwe tayari kushiri tumaini tunalo kwa Yesu. (hata iwe tumechoka jinsi Yesu alivyokuwa hapa)

### 2. JIHUSISHE KIBINAFSI NA VYEMA
Jambo moja zuri kuhusu huu mkutano ni jinsi Yesu anavyomchukulia mwanamke Msamaria: kwa wema, unyeti, na huruma. Njia asili ambayo alimshikirisha katika mazungumzo, uhusiano wa kibinafsi anayofanya na maisha yake na huruma ambayo anafunua ukweli kwake ni mifano uanyo himiza na kuchochea jinsi ya kushiriki katika mazungumzo mazuri.

### 3. SIKIZA VIZURI
Haiepekiki kwamba watu watakuwa na maswali kuhusu kile tunachoamini, badala ya kuwa mahali pa kutojuwa na maswali, tunapaswa kuchukua muda kusikiliza vizuri na kutoa majibu mwafaka na ya dhati na swali lipi tunaweza kujibu. Mara nyingi unajumuisha kuuliza maswali yetu wenyewe kama yesu anavyofanya na mwanamke Msamaria. Maswali yanaalika watu kutafakari juu ya mambo maoni tunayowasilisha (na kutafakari maoni yao pia) kuliko kuwauliza tu kile tunachowasilisha kwao. Yesu alikuwa shupavu katika kutumia maswali katika uinjillisti wake, akikabiliana na watu wenye udhaifu wa maadili yao na mtazamo wao wa ulimwengu na mahali pake kuwapa ukweli.

**4. TOKA MAHALI PA KUTOELEWANA KWA UFUNUO**
Mwanamke haelewi kile yesu anachosema mara ya kwanza (mstari wa pili) Yesu anavumilia katika mazungumzo huku akizidi kujenga msingi ambao utajenga kuelewa kwake hadi atakapopata ufunuo. Kutoelewana na kufatsiri vibaya ni sehemu ya mazungumzo ya kibinadamu. Usiogpe, vumilia endelea kujenga daraja mpaka unachosema kiwe wazi - huu ndio wajibu wako - ni roho ya mungu ambayo hubadilisha uelewa wa rahisi kuwa ufuno wa kweli.

**5. WEKA JAMBO KUU KUWA JAMBO KUU**
Ingekuwa rahisi sana kwa Yesu kufuatilia mazungumzo ya kisiasa na kitamaduni wakati mwanamke huyo alionyesha wasiwasi kuhusu ombi lake la maji, badala yake aliweka jambo kuu kuwa jambo kuu (ili mazungumzo ya injili yasonge mbele. Mara nyingi katika injili ya mazngumzo kutakuwa na fursa za kuvurugwa lakini lengo letu kuu (hata kama kuna njia na kuvurugwa hapa na pale) ni kuweka msalaba katikati ya mazungumzo.

**6. TAMBUA UWEZO**
Mtu aliye mbele zako ana uwezo wa kupokea injili na kuwa shahidi kwa ajili yake. Wale a mbao wamekutana hivi karibuni ni wainjilisti wenye kul;azimisha zaidi. Hii inapaswa kutupatia changamoto kuwa hatupaswi kamwe kupoteza furaha ya kuambukiza ya wokovu na kutuhamasisha kwamba wale ambao tunawashuhudia waweze kuwa mashahidi ka Kristo wenye mvutio na ufanisi.

Wakati sio kila mtu anaweza kuwa na jukwaa la kuhubiri (hata wito na kipaji au karama ya kuwa mwinjilisti anayehubiri tunaitwa kushiriki katika uinjilisti. Mazungumzo mengi ya kiinjili ulimwenguni hufanyika kwa njia ya kibinafsi kupitia mazungumzo na watafutaji wa kibinafsi. Yesu na wafuasi wake walijitolea kwa njia hii ya ufikiaji kwa hivyo pia tunapaswa kuwa hivi.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)
Chunguza maswali yafuatayo au nukuu ya majadiliano:

- Je! Kwa nini kusikiza/ kusikiliza ni muhimu wakati tunapoongea/zungumza na watu kuhusu imani yetu?
- Je! Injili ya mazungumzo inaweza kubadilikaje kulingana / ikitegemea mtu akiwa rafiki au mgeni?
- Je! Unawezaje kuwa na maksudi zaidi unapotafuta fursa za ushuhuda wa kibinafsi?
- Je! Unawezaje kuhimiza na kusaidia wale ambao wanaona ugumu wa ushuhuda wa kibinafsi?

> "mapambano yetu dhidi ya uinjilisti sio hasa juu ya mbinu lakini juu ya kukomaa. Je! Tuna moyo wa mungu na tunajali vitu ambavyo mungu hujali (watu wapotovu waliopotea)? ikiwa tuna moyo wa mungu basi tutafanya kadri ya uwezo wetu kuendeleza malengo ya ufalme wake katika kila mazungumzo tunayo na marafiki wetu wasioamini."
>
> **NORMAN & DAVID GEISLER**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)
Zungumza na mtu kuhusu imani yako kama sehemu ya maisha yako ya kawaida. Sio kupitia fursqa za huduma huduma au ushiriki wa kuzungumza. Katika mazumgumzo ya kila siku waulize ikiwa wana swali lolote kuhusu, wanafikiri yesu ni nan I na uone yanelekea wapi.

## MAOMBI
Omba kwamba mungu akusaidie kuona vyema uwezo unaokuzunguka kila siku kushiriki tumaini lako na engine. Mshukuru kwa kuziweka hizi fursa mbele yako na kwamab anafurahi kukufanya uwe sehemu ya kile anachofanya ulimwenguni. Ombeni kwa wale wanaopata changamoto kubwa na mikutano ya moja kwa moja kwamba mungu atawasaidia kushinda woga wowote na wasiwasi na mtashangiliana munapoendelea.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)
Jaza fomu za uwajibikaji shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.

# MAANDISHI

# KIKAO CHA ZIADA CHA PILI: UTETEZI WA IMANI

**Kikao hiki kinatazama zana ya utetezi wa imani na hutusaidia kutambua ni wapi tunaweza kuhitaji kunoa/ kujiandaa kuhusu mambo kadha ambayo ulimwengu unataka kuzungumza juu yake, wakati tupo na uwezo wa kuelekeza watu kwa mtu ambaye ni Kristo.**

"utetezi wa imani hauwezi kuokoa, Yesu Kristo tu ndiye anaweza kufanya hivyo ,lakini utetezi unaweza unapaswa kutumika kama Yohana mbatizaji, kufanya njia ziwe wazi/ kunyosha njia na kuwezesha njia za msalaba wa Kristo."

**J.W. MONTGOMERY**

## KIKAO KATIKA SENTENSI

Utetezi wa imani ni zana ya uinjiisti inayotusaidia kujibu maswali kuhusu imani yetu na kukutoa utetezi wa injili kwale wanaoipinga.

## ASILI YA KIKAO

Tunapoulizwa maswali kuhusu imani yetu na ujumbe tunaohubiri, ni jukumu letu kutoa majibu halisi yanaonyesha ukweli kuhusu Yesu Kristo.

Utetezi wa dini ya Kristo hufafanuliwa kama "utetezi wa imani ya Kristo" utetezi wa imani sio jambo jipya katika uinjilisti lakini linaweza kupatikana katika Biblia yenyewe. Kutoka kwa matumizi ya neno la kisheria " utetezi" katika 1Petro 3: 15 hadi ujenzi na uwasilishaji wa hotuba ya Paulo kwa Wathene katika Matendo 17.Biblia ina zaidi ya tukio moja la uwasilishaji wenye busara au ubunifu wa imani ya Kikristo kwa kujibu maswali wasiwasi na pingamizi.

Kazi ya utetezi sio ya kumfanya mungu ajulikane bali ni kuwaunganisha watu na ukweli na ukweli wa tumaini ambalo tunalo. Tunatetea imani yetu ili wale wanaouliza wapate kumjua Kristo. Lakini hakuna mtu anayebishana ili aingie ufalme mungu- ni kwa nguvu yake ya kuokoa.

## MWONGOZO WA KIKAO

### WAKATI WA MAPATANISHO (DAKIKA 10-20)

Chukua muda ili kuweza kujuliana hali, kushiriki hadithi, kuhimizana na maoni kuhusu fursa, jambo lolote litakalo himiza kikundi. Kwa makundi madogo uliza kila mtu ashiriki ushindi mmoja na kitu kimoja anachopambana nacho. Kwa makundi makubwa chagua watu wanne au watano washiriki ushuhuda maalum tangu makutano uliopita.

### MAOMBI

Toa muda kwa mungu na uombe juu ya hali yoyote, nzuri au changamoto iliyoangaziwa wakati wa mapatanisho.

## MAFUNZO (DAKIKA 20-30)

Tumia nyenzo zifuatazo za mafundisho kwa njia yako mwenyewe aidha kwa kuisoma moja kwa moja au kuifanya upya katika uwasilishaji wako.

> "Mwe tayari siku zote kumjibun kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu."
>
> **1 PETRO 3:15**

Petro anawaeleza waumini wote wawe tayari kutoa jibu kwa mtu yeyote anayeuliza ni kwanini tuna tumaini tunalo. Tunapaswa kuzingatia kushiriki injili kwa wazi lakini maswali yanapoibuka tuwe tayari kutoa majibu yetu kwa makini na kwa maana.

Maswali kadhaa ya kimsingi ya ufalsafa wa maisha pia ni magumu kujibu;" kwa nini nipo hapa? "ni wapi tumetoka?" ,"ni nini maana ya maisha?". unaweza kuulizwa pia utoe maoni yako ya kile imani ya Kikristo inasema kuhusui maswala haya ya mada kama vile: ujinsia, kitambulisho cha jinsia, talaka au kuaviya mimba. Unaweza kujikuta ikijaribu kutetea nafasi za imani za kale dhidi ya uelewa wa kisasa au kisayansi- kwa mfano kutetea tukio la uumbaji katika Mwanzo kwa kuzingatia nadharia ya Darwin ya mageuzi. Maswali mengine yanaweza kuchunguza madai kuhusu tabia/sifa za mungu- kama vile jinsi mungu mzuri anaweza kuruhusu mateso.

**SWALI:** Je! Ni maswali gani ya imani umewahi kuulizwa awali/zamani na umejiandaa vipi kujibu maswali haya?

Kwa bahati utetezi wa imani hauwezi kuokoa mtu yeyote, vingenevyo shinikizo na jukumu la wokovu lingetemea nguvu za hoja zetu. Utetezi wa imani mara nyingi inaweza kuwa njia ya kumsaidia mtu kutoka kwa kutoamini na kwenda kwa kuamini, lakini ni mungu mwenyewe ambaye huleta mtu kwa uzima wanaposikia na kuitikia wito wake kupitia ushuhuda wa mungu.

Fikiria juu yake hivi: tunasimama na asiyeamini kwenye barabara, upande wa pili ambao ni msalaba mtgupu wa Kristo. Kando ya barabara kuna mashimo, kuta, vizuizi, uchafu na vitu vilivyo na ncha kali msalaba wenyewe hauonekani vizuri kwa sababu ya ukungu.

Utetezi wa imani ni njia ambayo tunawezaa kusafiri kwa usalama barabarani,huku uchafu ukifagiliwa, mashimo yakizibwa, kuta zikibomolewa, vizuizi vikiondolewa na ukungu ukisafishwa. Lengo letu kuu ni kumsaidia mtu kusogelea msalaba, kwani hapo ndipo watakuna na Yesu aliyefufuka. Utetezi wa imani hutumika tu kwa mtu ambaye hajaamini kutoa nafasi kukutana na yesu.

Hapa kuna vitu vinne vya kuzingatia ili kuweza kufanikiwa katika mazungumzo ya utetezi.

### 1. JIHUSISHE NA NGUVU YA MAANDALIZI

Kwa wengine kama watetezi maarufu Ravi Zacharias, Williams Lane Craig na John Lennox, utetezi wa imani ni kiini kikuu cha ufikiaji wao wa uinjilisti na kwa hivyo kusoma theolojia, falsafa, sayansi, historia, maswala ya siasa, dini ya ulimwengu itakuwa chakula cha muhimu. Kwa wengine nia ya kuendelea kujihusisha na masomo tunapokutana nao ulimwenguni na katika mazungumzo itakuwa jambo la busara; haswa tunapojua kuwa mmoja wa marafiki yetu na wasiwasi au ana swala fulani. Hii sio kusema chochote kuhusu kujitolea kwetu kwa kawaida kula neno la mungu kila siku ili tuweze kukua katika ufahamu wetu juu yake na ukweli unaofunua.

### 2. JITOLEE KWA NGUVU YA MAOMBI

Kama ilivyo kwa aina zote za uinjilisti maombi ni muhimu, linakuja swala la utetezi wa imani, muombe mungui akusaidie kujibu maswali kwa upola na heshima.

### 3. TAMBUA NGUVU YA UNYENYEKEVU

Kiburi na ugomvi ni sifa zisizosaidia na zisizo vutia. Kujibu swali kwa kusadika haimaanishi tunapaswa kutuka unyenyekevu wetu nje, unyenyekevu unamaanisha kuwa tuko tayari kukubali hatujui kila kitu. Wakati mwingine kusema: " hilo ni swali zuri, sijui jibu la hilo" ni jibu bora zaidi tunalo weza kutumia.

### 4. TUMIA NGUVU YA MASWALI

Kuwajulisha watu kuwa wana ruhusa ya kuuliza maswali yoyote na kwamba unafurahi kujarinu kujibu bila kukasirika kunaweza kutengeneza fursa nzuri za mazungumzo haswa na wale ambao wangependa kuuliza maswali lakini wana uoga wa kukukasirisha, usiogope kuuliza

maswali yako mwenyewe. Mazungumzo sio njia moja pekee. Hatupaswi kutafuta kwa ustadi kuweka /au kuwasukuma watu kujitetea zaidi, lakini kwa upole kuelezea upungufu wao katika mawazo yao ya awali. yesu alipenda kuuliza maswali alipokuwa akihudumu na aliuliza kwa kiasi kikubwa zaidi ya alivyojibia.

Hakuna mtu awewahi kuingia katika ufalme wa mungu kwa kuwa shupavu katika majadiliano ya utetezi wa injili (au hakuna mtu amewahi kuingia katika ufalme wa mungu sababu ya kupinga majadiliano), au kuwa mfuasi wa Yesu kwa sababu walipoteza mjadala. Lakini mazungumzo ya utetezi wa imani yaliyo ya upole na yenye heshima yanaweza kusaidia watu kusonga mbele kidogo katika barabara ya kuelekea msalabani.

## MAJADILIANO (DAKIKA 20)

Chunguza maswali yafuatayo au nukuu la majadiliano:

- Je! Kwa nini ni muhimu kuchukua maswali ya watu kwa umakini?
- Je! Ni nini upungufu wa utetezi wa imani?
- Je! Unajisikia kuwa na uwezo au umejiandaa kujibu maswali yanayoibuka unaposhiriki injili?
- Je! Masomo ya utetezi wa imani yawezqaje kuwa ya maabudu?

> "utetezi wa imani inaweza kuwa rasilmali ni jukumu la mtetezi kufanya uhusianona maisha ya watu halisi katika ulimwengu wa kisasa, bila muungansiho huu,nadharia zinabakl kuwa nadharia tu, maoni yakufikiria yakining'inia tu hewani na hayana msingi katika ukweli wa maisha."
>
> **ALISTAIR MCGRATH**

## MATUMIZI (DAKIKA 5)

fikiria kuhusu maswali haya kuhusu imani ya Kikristo bna uchunguze jinsi unavyoweza kumsaidia mtu kusafiri kutoka kwa swali lao la kwanza hadi msalaba wa Kristo.

- Je! Ni nani aliyemuumba mungu?
- Je! Ukristo haujakataliwa na sayansi?
- Ni vipi kuhusu nadharia ya BIG BANG na ndharia ya mageuzi?
- Je! Ikiwa mungu ni mwema mbona uanruhusu mateso ulimwenguni?
- Je! Biblia haijajaa makosa na Utata?
- Ikiwa mungu ni wa kweli kwanini asijionyeshe tu kwa ulimwengu?
- Hakuna kitu kama ukweli kamili kwa hivyo sisi sote tunaweza kuamini kile tunachotaka.
- Mimi ni " mtu mzuri" kwa nini mungu anipeleke kuzimu kwa sababu siamini yupo?
- Mbona tu Kristo sio/badala ya dini ingine?
- Je! Unaamini katika miujiza kweli?

## MAOMBI

Omba kwa pamoja kwa hekima ya mbinguni unapojaribu kujibu maswali na wasiwasi wa ulimwengu kwa unyenyekevu na upendo huku ukimwakilisha mungu kwa uadilifu na ujasiri. Ombea akili zilizo wazi na mioyo inayopokea na shukuru kwamba ingawa kuna majibu mazuri na yenye busara ya kushiriki, mwishowe kazi ya kuokoa ya mungu haitegemei uwezo wa watu kujibu maswali magumu.

## UWAJIBIKAJI (DAKIKA 15)

*Jaza fomu za uwajibikaji, shiriki katika jozi au makundi madogo kisha muombeane.*

# KIAMBATISHO:
# MAFUNDISHIO YA INJILI

Wewe sio ajali/ bahati mbaya, umeumbwa na kwa mafano wa mungu mwenye upendo (Baba,roho, mwana) ambaye ndiye chanzo na mtunzaji wa maisha yako (MWANZO 1).

Wote wamemkataa mungu (wametenda dhambi) kwa kwenda njia yetu wenyewe badala ya lkuishi kwa kumtii muumba wetu. Ni kwa sabau hii dunia imevunjika na imejaa mateso. Dhuluma hii humkasirisha mungu ambaye ambaye hazingatii dhambi kwa kuipuuza au kuikubali. Lakini kwa haki huwadhibu wale wanaokosea, (WARUMI 3:23).

Ikiwa tunamuasi mungu hautna uwezo wa kuyaweka mambo sawa. Baada ya kufanya kitendo cha uhaini dhidi ya mfalme wa ulimwengu. Kukataa mungu ni kukataa maisha yenyewe. Tumebaki na kifo cha milele-mazao halisi ya kukataa kwetu maisha na adhabu yha mungu (haki kuu) kwa kuvunja kiwango chake cha kuishi sawa (WARUMI 6:23).

Lakini mungu hataki yeyote ajue kifo /mauti, kwani yeye mwenyewe ni upendo na anataka kuwa na uhusiano wa milele na sisi watoto wake wapendwa. Mungu kwa neema yake alianzisha kazi ya uokoaji ili kutuokoa(1 TIMOTHEO 2: 4-6).

Mungu alimtuma mwanawe ulimwenguni kama mwanadamu, kuishi maisha kam ili ya kibinadamu ambao hayakumkataa Baba yake, Yesu aliliuwa msalabani akifanya kama mbadala wetu, akichukua kifo tulichostahili kwa kumkataa mungu (YOHANA 3: 16, YOHANA 1: 7-9)

Kifo na ufufuo wa Yesu ulileta maridhiano, ukombozi, upatanisho (utulivu) na kushindwa wa uovu. Dhambi zetu zilipewa sifa kwa yesu na tukapewa sifa ya haki hyake (haki iliyohesabiwa). linalohitajika kwa upande wetu kwa shughuli hii kwanza ni kuamani katika Yesu kama Bwana (imani), na kuamini kuwa mungu alimfufua kutoka kwa wafu.

Tunaokolewa kwa imani tu (MATHAYO 20:24, WARUMI 1O: 9, 2 WAKORINTHO 5: 18-21, YOHANA 12: 31, WAKOLOSAI 2: 15). Tunaweza sasa kupata uhusiano uliorejeshwa na baba yetu wa mbinguni. Tuna imani na tumechukuliwa katika familia yake. Tunakufa kwa maisha yetu ya zamani na tumezaliwa tena katika maisha mapya (LUKA 9: 23, WAKOLOSAI 1: 23, 13-24, WARUMI 5: 1-2, WAGALATIA 4: 4-7.

Yesu alipaa mbinguni ambapo anatawala kwa mkono wa kulia wa Baba, lakini amewatumia waumini zawadi ya roho mtakatifu ili kutuwezesha kuishi kwa utii katika utimilifu wa maisha na kutusaidia kushiriki habari yake njema na ulimwengu. Tunakuwa viumbe vipya-wanafunzi waliobadilishwa na kazi ya roho takatifu maishani mwetu inasababisha kuzaa matunda. Tunafanya kazi kama mabalozi wa mungu ulimwenguni, tukiwakilisha ufalme wa amani, tukitumika kama mashahidi wa ukweli wa hadithi ya yesu kwa maneno na matunda (MIKA 6:8, MATENDO 1:8,2, 2 WAKORINTHO 5: 11- 21, WAGALATIA 5: 23-23).

Siku moja yesu atarudi kuwahukumu walio hai na waliokufa, ufalme kamili wa mungu utarejeshwa na uzima wa milele na Baba yetu mwenye upendo unasuburi wale waliomtumaini Yesu kama Bwana. Kifo cha milele (kuzimuj) kinangojea wale ambao hawamtumaini. Habari njema ni kwamba hakuna mtu anayehitaji kuangamia milele, wote wanaweza kujua uzima wa milele na furaha katika uhusiano na mungu, kupitia imani katika Yesu Kristo (1 WAKORINTHO 15, UFUNUO WA YOHANA 21:1, 22: 1-5).

# KIAMBATISHO: SIMULIZI YA INJILI

Kabla ya vitu vyote mungu alikuwepo na uhusiano wa kamili na yeye mwenyewe, baba, mwana na roho. Mungu aliumba ulimwengu na ulikuwa mzuri sana, na alishiriki uhusiano wa kipekee na wanadamu. Tuliumbwa kwa maisha kamili pamoja na yeye wa mfalme wa ulimwengu na wa maisha yenyewe.! lakini mungu hakulazimisha wanadamu kumpenda,alituacha tuchague sisi wenyewe, na hii hiari ya bure ubinadamu uliamua kwenda kwa njia yao wenyewena kumkataa mungu.

Kukataa mfalme wa ulimwengu ni uhaini usio na usawa au linganika, uasi dhidi ya maisha yenyewe, mateso, kifo na maumivu yaliingia ulimwenguni. Ubinadamu umejihukumu kujitenga na Baba yao kamili wa mbinguni bila njia ya kumrudia. Mungu hakuweza kuitikia uasi kwani hapatakuwa na haki kwenye tendo hilo. Mungu mwadilifu na mwenye haki ni lazima adai adhabu kwa ualifu uliofanywa. Adhabu ya uasi dhidi ya maisha ni kifo.

Lakini mungu aliupenda ulimwengu kwamba alianzisha mpango wa kuokoa ubinadamu kutoka kwa kifo na kufanya tuweze kujua utimilifu wa maisha yake na upendo wa Milele. Mungu alimtuma mwanawe Yesu ulimwenguni aishi maisha kamili/ kamilifu ya binadamu. Maisha ambayo hayakuasi kamwe na kuwa na hatia ya uhalifu wowote dhidi ya mungu.

Kwa hiari Yesu alikufa msalabani, kuchukua adhabu ya kifo ambayo wanadamu walistahili kwa uasi na kwa kufanya hivyo akawa mbadala wetu, siku tatu baadaye alifufuka ,kwa sababu yeye ni mungu na mauti haiwezi kumshika. Katika wakati huu iliwezekana kwa ubinadamu kupokea msamaha kwa uasi dhidi ya mungu, kushirikin katika maisha mapya na ya milele amabyo yesu anawezesha. Laana ya kifo ilivunjwa .

Tunachohitaji kufanya ni kuamini kuwa Yesu ni yeye anayesema ni- mkombozi wa dunia aliye sulubishwa msalabani am kufufuka, mfalme wa ulimwengu na chagua kumfanya Bwana wa maisha yako /yetu. Kuna wokovu na uzima kwa wanaomtumaini- na kuwezeshwa na roho mtakatifu kuishi maisha ambayo tuliumbiwa, maisha ambayo yanaonyesha sura ya mungu ili wote wapate kujua maisha ya ukweli,kwa kuweka tumaini letu kwa Yesu tunakufa kwa maisha yetu ya awali/zamani na tumezaliwa tena upya katika maisha mapya. Siku moja Yesub atarudi na ufalme wake kamili utarejeshwa. Wote wanaomtumaini wataishi milele ndani ya ufalme wake na kwa hivyo tunaitwa na kushurutishwa kushirikim upendo wa mungu na ilimwengu ili wote wapate kujua tumaini la milele.

# KIAMBATISHO:
# MFANO WA MAZUNGUMZO YA DAKIKA KUMI YA INJILI YA VIJANA

## 1. WEWE SIO AJALI

Watu wengi huzunguka wakidhani wao ni ajali ya ulimwengu, kwamba wako hapa kwa sababu ulitokea tu kutoka kwa kitu chochote na sisi kwa namna fulani tulifika miaka bilioni baadaye. Lakini hiyo haina maana yoyote wala haitoi tumaini lolote la maana ya maisha inaweza kuwa nini.

Biblia inasema kwamba mungu amekuwepo na aliumba ulimwengu kutokana na hamu yake ya kushiriki upendo wake na uumbaji wa mungu-ubinadamu,

Kwa hivyo wewe sio Ajali, wewe ni uumbaji wa Mungu unapendwa na una kusudi.

## 2. UMEKOSA HOJA

Shida ni kwamba watu wasipojua kwamba waliumbwa na mungu na mungu anawapenda, wanakosa uhakika wa maisha yao. Kunjua mungu ni kuishi maisha kama vile ilivyokusudiwa kuishi- katika uhusiano wa mungu mwenye upendo,mwenye fadhili, mwenye huruma, mwenye neema, mvumilivu na mwenye hekima. Biblia inazungumzia juu ya mungu kama Baba mkamilifu, anayetakia watoto wake vitu vizuri. Huyu n I mimi na wewe.

Kutomjua mungu ni kama kukimbia kwenye uwanja wa fainali ya kombe la dunia bila kujali kuweka goli,hakuna mtu atakuweza kufunga mabao, hakuna ataweza kushinda kombe-itakuwa haina maana kabisa.

## 3. UMEWEZA KUJUA MAISHA KAMILI/ MAKAMILIFU

Tatizo kubwa la kukosa uhakika na mungu ni kwamba hatupotezi tu maisha bora aliyonayo, tunakataa na kumpa kisogo mfalme na muumbaji wa ulimwengu. Biblia unatuambia kwamba tunapokataa maisha ambayo mungu anayo kwetu,vitu vibaya vitakuja ulimwenguni kwa sababu, tunafikiri kwamba tunajua kuishi maisha haya bora kuliko yule aliyetuumba hii Biblia inaita dhambi, Lakini labda ni njia rahisi ya kufikiria tendo hili ni ubinafsi. Tunachagua njia zetu badala ya mungu tunasema: “ hallo, mungu mimi ni bora kukuliko, najua zaidi yako, sikuhitaji”, tupaswa tu kuangalia runinga kuona habari ya ulimwengu uliochanganyikiwa ambao tunaishi ndani na haya ndio matokeo ya watu kukosa uhakika na maisha yao wenyewe, sio badala ya kuishi kwa sababu ya baba yao mpendwa, mungu.

Kutaliwa huku kunaweka kizuizi kati yetu na mungu, unapokwenda kinyume na mungu anayetoa uhai unabaki na kifo tu.

Lakini mungu hataki ufe. Biblia inatueleza mungu alituma yesu katika ulimwengu huu. Mungu katika umbo la wanadamu kusihi maisha kamilifu yanayotuonyesha jinsi ya kuishi maisha kwa ukamilifu. Tunapomkataa mungu kuna adhabu kutokana na hili kama vile mwanafunzi anavyopewa adhabu kwa kuvunja sheria za shule.

Yesu aliuliwa msalabani, kama mfano wa kuchukua kifo ambacho tuachagua tunamkataa mungu kuchukua adhabu yetu.

Alifufuka siku tatu baadaye, baada ya yote yeye ni mungu, kifo/ mauti haiwezi kumueka chini, kuashiria kuwa tunapomwambia “ samahani” tunaweza kurudi kwenye uzima/ kuwa hai tena na kujua maisha kikamilifu.

## 4. NI NANI AMEKALIA KITI MOTO CHA MAISHA YAKO? /NI NANI AMEKALIA KITI CHAKO MAALUM CHA MAISHA

Ni nani hutazama hadharia ya " BIG BANG" katika onyesho hili Sheldon aliye mhusika yupo na kiti chake maalum kwenye kochi ambapo hakuna mwingine anayeruhusiwa kukei pale hapo- ni nafasi yake. Na hivyo ndivyo tulivyona maisha yetu, tunasema: "**Mungu! Huwezi kukalia kwenye kiti/nafasi maishani mwangu,nataka kuthibiti."**

Lakini mungu anatupenda sana hivi kwamba anataka tujue maisha ya kweli ambao kwa ajili ya yao alituumba, kusaidia, kutuongoza kukaa mahali anastahili, katika kiti moto/ maalim cha maisha yetu.

Watu wengi wamechanganyikiwa kuhusu maisha yanahusisha nini,tunapambana na unyokovu, kujidhuru, shida za kula, hatufurahishwi na kile tuanchoona kwa kioo, hatufikiri kwamba tutaafikia chochote, hatuna furaha na tumefadhaika.

Mungu anasema: "**umekosa hakika, rudi kwangu sema samahani kwa kunikataa na nitakusamehe, weka imani yako kwangu nitakuonyesha maisha kamili, maisha ya kweli, na hutaona kifo kamwe**"

Wewe sio ajali, unapendwa. Mungu hatakulazimu umuaamini, chagua wewe mwenyewe mrudie mungu na ujue ,maisha ya kweli.

# KIAMBATISHO: NJIA ZA INJILI

## THE FOUR SPIRITUAL LAWS

(Sheria nne za kiroho (4laws.com)

Maelezo maalum ya Billy Bright ya misingi ya injili

## THE4POINTS

(hoja nne) the4points.com

Toleo la vijana linalo lenga sheria nne za kiroho

## THE THREE CIRCLES

(miduara mitatu)

Mifano tofauti kutoka kwa mtandao hasa YouTube

Maelezo mafupi na rahisi ya injili, iliyopangwa kutumiwa kwa urahisi na mtu yeyote anayejifunza.

# KIAMBATISHO:
# MAKALA YA “KITU KIMOJA”

**Makala haya mafupi ya “KITU KIMOJA” yameandikwa na wainjilisti wenye uzoefu ambao kila mmoja hutafakari juu ya jambo moja ambalo anatamani angejua wakati walipoanza kuhubiri injili. Makala haya yanaweza kutumiwa kama kichocheo cha majadiliano ya kikundi ama kupewa kama kazi ya ziada (somea nyumbani ) au kusoma tu kama faraja ya jumla kama safari yako kama mwinjilisti.**

## TEMBEA KWA IMANI NA SION KWA KUONA

**ANDREW PALAU - USHIRIKA WA CHAMA CHA LUIS PALAU**

> Maana tunaenda kwa imani sio kwa kuona
>
> **2 WAKORINTHO 5:7**

Ninaweza kumsikia baba yangu mwinjilisti Luis Palau akiyarudia maneno haya tena na tena, unyenyekevu wake, shauku yake, kusadikika kwake kwa kina, utii kwa yesu Kristo na safai ya imani kutoka mwanzo hadi mwisho. Baba wangu kwa kweli ameniiga mfano wa furaha inayokuja kwa kutii Yesu sio tu katika huduma pekee lakini katika maisha yake yote - ni safari ya kuwa mfuasi wa Yesu, - kumtii Kristo bila kujali wito wetu. Natamani ningejifunza ukweli huu mapema maishani. Ilinichukua miaka ishirini kufika hapa.

Baba kwa kweli ameishi ukweli huu, tangu siku zake za mwanzo kama muhubiri wa mitaani nchini Agentina hadi sasa akiwa matibabu ya kemikali (chemotherapy) kwa saratani ya mapafu.anachukua kila siku kama fursa ya pekee ya kujifunza kumtegemea mungu an kumsikiliza tena.

Moja ya mashairi ambayo baba alipenda ya kutoka kwa mwanashairi C.T STUDD inasema ”maisha ni moja tu, hivi karibuni yatapita, kile kinachofanywa kwa ajili ya Kristo kitaishi daima” baada ya baba kushiriki hii na mimi unanikumbusha maswali amabyo mungu atatuuliza wakati maisha yetu ya hapa duniani yameisha: “ulifanya nini na kile nilichokupa na ulileta nani?” ni soma gumu kuzingatia yale ambayo yana umuhimu wa millele na kuweka kipaumbele na inaweza kutuongoza kwenye njia ngumu wakati mwingine, lakini ninanvyojua sasa ni kitu bora ambacho tunaweza kufanya na maisha yetu:

> “maana upendo wa Kristo watubidisha maana tumekuhumu hivi, mmoja alikufa kwa ajili ya wote,basi walikufa wote. Tena alikufa kwa ajili ya wote ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe bali kwa ajili ya yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao”
>
> **2 WAKORINTHO 5: 14-15**

Ni fursa kubwa kuwa sehemu ya kushiriki habari njema na watu wengi kama tunavyoweza. Tumejitolea kutangaza injili na kuvuta roho za watu kwa Yesu na kuunganisha kanisa pamoja kwa umoja na kuathiri miji dunia nzima.

Ni siku njema kuwa hai, ni siku nzuri kuhubiri, ni siku nzuri kuwa pamoja katika agizo kuu/ utume mkubwa -ingawa sio rahisi ni wakati tu tunajifunza kumsikiliza mungu na kumuamini kila siku tunaweza jionea maisha bora.

## INATEGEMEA NEEMA YA MUNGU

**ROY CROWNE - MKURUGENZI MKUU, HOPE TOGETHER/ PAMOJA KWA IMANI**

Paulo anatoa taarifa kubwa kwa Wakorintho anatambua kuwa mungu amembadilisha kutoka kwa kuwa mmoja aliyekuwa na kasoro asiye wa kawaida na kumfanya kuwa mtume. Tofautii kati ya hizi mbili ni neema tu.

> “lakini kwa neema ya mungu nimekuwa hivi nilivyo: na neema yake iliyo kwangu ilikuwa siom bure bali nilizidi sana kufanya kazi kupitia wao wote, wals si mimi bali ni neema ya mungu pamoja nami”
>
> **1 WARORINTHO 15: 10**

Natamani mtu nagenieleza wakati nilipoanzna huduma kwamba sio tu juu yangu bali ni juu ya neema ya mungu. Ufunguo wa uwepo wa mungu na kuelewa wito wa mungu ni usemi” ASANTE” mara nyingi ntunawaza kuwa ni njuu yetu, kipaji/karama/kipaji chetu, uwezo wetu na huduma yetu. Ikiwa mtu angeniambia mapema ni neema ya mungu na chaguo lake kututumia na kutubariki na wakati anatutumia kuiita wengine kwak, bado ni neema ya mungu.

Kwa hibyo hebu tutambue kuwa tunaishi tu yale maisha mabayo mungu amefanya ndani yetu na tunafanikisha tu yale ambayo mungu amefanya kupitia sisi.ikiwa ningejifunza haya mapema ingeondoa shinikizo hakuna haja kupoteza nguvu kushindana, kuhukumu kufikliria yote yalikuwa juu yangu.

Kwa huduma nyingi ambazo nimekutana nazo za viongozi wote wanaomaliza vizuri, mafanikio yao yanayokana yanategemea neema ya mungu. Paulo alisema laifanya kazi kwa bidii kuliko wote, lakini hata hivyo ilikuwa kwa sababu ya neema ya mungu. N I njia nzuri ya kushi tukigundua ni upendo wa mungu usio na masharti kutupatia kipaji/karama na kutuandaa kile achotuita kufanya.

Kuishi katika zawadi hivi na neema inamaanisha tunahitaji kumpa sifa kila wakati ili kutembea kwa unyenyekevu na mungu ambaye alituita kwa hali hii.

Kama ukweli wote nilitamani ningejua wakati nilianza, nina hitaji upendo katika ukweli huo leo ili kutimiza wito na huduma yangu.

## MUNGU HUTUMIA JUHUDI ZETU NDOGO / DUNI KWA NJIA ZA AJABU

### GAVIN CALVER - MKURENZI WA MISHENI MUUNGANO WA KINJILI/ EVANGELICAL ALLIANCE

Jambo moja ambalo natamani ningejua wkati nilianza kuhubiri injili ni kwamba kile ninachofikiria kuwa duni kiwango kutoshughulika au kusumbuka kitumia kwa hivyo kina thamni ndogo,kinaweza kutumiwa njia ya ajabu wakati umemoa mungu. Uzoefu umenifunza kupata faraja kwa maandiko hasa hadithi ya kulishwa kwa watu elfu tano katika Yohana 6,ikiwa utaongezea wanawake na watoto unagundua na watu kati ya elfu kumi na moja na elfu kumi na tano wenye njaa uwanjani wakati wa chakula cha mchana.

Andrea anamwendea Yesu na kusema” kijana huyu hapa ana mikate mitano na smaki wawil, lakini hii italisha watu wangapi?” (Yohana 6:9).

Andrea haelewi jinsi toleo hilo dogob litasaidia lakini licha ya wake wa ufahamu ya korohobado anajua vya kutosha kumletea yesu. Anakubali kwamba chakula cha mchana kilicho mbele yake hakiwezi tosha hata mtu mmoja mwanamume aliye na njaa. Lakini anafanya kazi na Yesu ambaye anafnaya maajabu kwa hivyo anaipeleka kwa mfalme, matokeo yake ni yesu analisha umati wote wa watu uwanjani hata chakula kinabaki. Andrea ameshangazia sawia na wengine lakini anaanza kugundua kwamba huyu Yesu anaweza kuchukua kile kinachoonekana kama juhudi ndogo kwetu na kuzitumia kwa njia ya kushangaza. Hii ni kweli kwa sisi wainjilisti leo. Anaweza kuchukua kidogo ambacho tunatoa na kufanya vitu vya ajabu. Rasilmali duni ambayo, vitu ambazo hatuwezi kuwaza kamwe. ukweli ulio wazi na rahisis ni kwamba Yesu akiwa upande wetu chochote cha weza kutokea.

Kwa sababu hii tunapofikiria hatuna chochote cha kumpa/kupeana tunadhani kwamba haukuna atakaye jibu, lakini ni lazima bado tulete madogo/ kile kidogo tuklicho nacho kwa yesu. Kama tu alivyochukua chakula cha mchana cha kijana na kulisha maelefu ya watu,anaweza kuchukua juhudi zetu ndogo za uinjilisti na kuzitumia kwa njia ya ajabu. Anaweza kubadilisha maisha hapo na hapo na kisha kupitia juhudi hizo ndogo. Ni muhimu

tuepuke kujitia lawama kwa kujilinganisha na wengine.. inaokekana kuna watu husema hadithi za kuongoza watukwa yesu kwenye gari la moshi,katika mbuga au mahali popote. Hadithi hizi zinafanya sisi wengine kujisikia kamwe hatuwezi kufikia viwango hivi. Wacha niwe wazi kuhusu kitu hatuwezi! Sisi ni ushuhuda ulio hai au ushuhuda unaoishi wa neema ya mungu, sio watu wanaokusanya hadithi za Holywood. Tunahitaji kusherehekea athari tunayofanya kila siku, sio kusherehekea wakati uiliowekwa katika mpango wa mungu. Sisi wote tunaweza kuleta kile kinachoenekana kama mchango mdogo na Yesu anaweza kutumia hii kubadilisha maisha ya wengi.Natamani ningegundua hii mapema kuendelea ndio ya maana zaidi, je! Na wewe pia utaendelea?

> Au katika maneno ya Mtume Paulo anavyosema:
>
> " ...ataendelea kushikilia kile ambacho Kristo alinishikilia nikisahau kilicho nyuma yangu na kujikaza kuelekea mbele, na songa mbele kuelekea lengo la kushinda tuzo ambayo mungu ameniita kwenda mbinguni katika Yesu Kristo"
>
> **WAFILIPO 3:M 12, 14**

## INUKA NA UENDELEE

**RACHEL JORDAN -WOLF - KANISA LA UINGEREZA**

Miaka ishirini na nane iliyopita nilimsikiza George Vermer akizungumza, akiwaita vijana kujitolea katika ulimwengu wa uinjilisti, nilijitolea kwa changamoto hio na miaka ishirini na nane baadaye bado nimejitolea. Kwa hivyo hii ni " jambo moja ambalo mtu aliniambia ambalo limenisaidia ambalo nashiriki na wewe"

Vermer anaandika katika kitabu chake" MAPINDUZI YA UPENDO

> "Ninakupa changamoto kuwa mkimbiaji wa mbio za masafa marefu za marathon kwa mungu katika kazi hii kubwa ya unjilisti wa ulimwengu. Unapoangushwa chini inuka tu na urudi kwenye mbio na uanze kukimbia, uposhindwa unapoanguka, inuka! Na utagundua siku moja miaka ishirini au thelathini kutoka sasa utakuwa bado unakimbia kama mimi, labda na uchovu, labda na jeraha lakini bado unaendelea kwa sababu ya Yesu Kristo, tuendelee pamoja kwa ajili ya ufalme wa mungu na uinjilisti wa ulimwengu"

Nina furaha sana kuhusu Advance 2020 itakuwa mika thelathini kama vile George Vermer alisema kwa hivyo inaokena sawa kurudia changamoto kwa kizazi kipya, mambo yatakuendea mrama yataharibika, safari hii itakuwa ngumu, lakini siri kubwa ni kuinuka! Na kuendela na wewe pia katika miaka thelathini baadaye utaweza kupitisha na kurudia changamoto na ujumbe huo huo/

## HUBIRI UJUMBE WA BIBLIA

**STEVE UPPAL - KIONGOZI MKUU KANISA LA MATAIFA YOTE**

Kwa miaka thelathini na moja nimepata heshima ya kuhuburi habari njema ya Yesu Kristo. Ikiwa ningeweza kurudi kwa ujana wangu na kutoa ushauri mmoja itakuwa kuhubiri ujumbe wa Biblia, ningejiambia kuwa nguvu halisi ipo katika neno la mungu linapotangazwa kwa ujasiri. Kwa hivyo jipe yafuatayo:

Soma Biblia kila siku na uwe thabiti katika nidhamu hiyona kiroho kuchukua neno la mungu, neno la mungu linalochukuliwa /somwa kwa udogo/ muda mdogo kila siku litaanza kuwezesha kubadilisha na kukuza. Kumbuka pia Biblia utakusoma -ukifunue vile ambavyo vinahitaji kubadilika ndani yako ili uweze kuwa kama Bwana.

Sikiliza mahubiri mazuri yawe moja kwa moja au podikasti, mahubiri yatakuwa ma mkate unaolisha roho yako na jinsi unavyofikiria na mtazamo wako wa ulimwengu. Baki mnyenyekevu na wakufundishika unaposikia neno.

Jifunze Biblia. Chukua vitabu, mada maneno na wahusika na uchunguze kwa kina. Kujifunza Biblia kutakupa kina zaidi na miziz yako itakita. Fanya kujifunza Biblia kuwa sehemu ya maisha yako. tathmini siku chache kwa wiki au / ama mara moja kwa wiki na uijenge katika mahadhi yako ya maisha.

Kariri mistari., vifungu,sura na vitabu vyote. Hili linaokena kuwa jambo gumu kidogo mwanzoni lakini unaweza kulifanya kwa uwezo wa roho

mtakatifu. Kuweza kunukuu Biblia wakati unapohubiri kunaongoza kiroho na nguvu katika/ kwa maneno yako tafuti na kitu kigine chochote.

Tafakari juu ya maandiko: wacha moyo wako na akili yako zitafune neno la mungu kwa siku nzima, iwe umesafiri au umelala kitandani, chukua andiko, fikiria na uulize roho takatifu ikupe ufunuo kupachika ukweli ndani yako kama mtu.

Omba kwa kutumia Biblia chukua Zaburi au saa/ maombi ya mtume na ujifunze kuzisali kwa Bwana, hakuna kitu chenye nguvu kama kuomba neno la mungu kwake. Unaomba kulingana na neno lake na hiyo utatupa imani kubwa katika maombi yako.

Nguvu ya kubadilisha maisha ipo katika neno la mungu kwa hivyo hubiri hiyo na sio hadithi na mawazo za kijanja, jiepushe na mitindo inayokuja na kupita, usipoteze nafasi yako ya kuhubiri kwa kushiriki maoni yako mwenyewe-shiriki neno la mungu na la milele na ni hilo pekee yake lina uwezo /nguvu ya kubadiilisha maisha

# USOMAJI ULIOPENDEKEZWA

**INJILI NA UINJILISTI**
Raphael Anzenberger - **Kugundua Tena Huduma Ya Unjilisti/ Rediscovering The Ministry Of The Evangelist**

Robert Coleman - **Mpango Mkuu Wa Unjilist**

Mark Denver - **Injili Na Uinjilisti Wa Kibinafsi/ The Gospel And Personal Evangelism**

Mark Greenwood - **"Ndio" Kubwa "Ndio" Ndogo Na " Labda" Yenye Afya**

Andy Hawthorne, Mimi Ndio Huyu - **Kujiunga Na Wito Wa Kusisimua Wa Kupenda Ulimwengu/ Here I Am, Joining God's Adventurous Call To Love The World**

Ben Jack - **Injili Ilio Rahisi/ The Simple Gospel**

R.T Kendall - **Ni Nini Kilichofanyikia Injili/ Whatever Happened To The Gospel?**

Will Metzger - **Sema Ukweli/ Tell The Truth**

J.I Parker - **Injili Na Uhuru Wa Mungu/ The Gospel And The Sovereignty Of God**

Luis Palau - **Kutoka Kwenye Jangwa? Out Of The Desert**

Rico Tice - **Unjilisti Wa Ukweli/ Honest Evangelism**

David Watson - **Ninaamini Katika Injili** (Sasa Kiko Nje Ya Kuchapishwa Lakini Nakala Za Mitumba Zinapatikana Kwa Bei Ya Chini Soko La Amazon/Amazon Workplace

Tom Wright - Habari Njema Tu/ **Simply Good News**

**KAZI**
David J.Bosch - **misheni zinazobadilisha/ transforming missions**

Peer Greer & Chris Horst - **kukengeuka misheni/ misssion drift**

Christopher J. Wright - **Misheni ya mungu/ the msiion of God**

**IMANI YA KIMSINGI YA KIKRISTO NA TEOLOJIA YA UTANGULIZI**
Oswald Chambers - **yote niwezayo kwa aliyebora zaidi/ my upmost for His highest**

Wayne: teolojia kimfumo - **utangulizi wa teolojia ya kiBiblia/stematic thelogy, an introdution to Biblical theology**

George Eldon Ladd - **teolojia ya Agano jipya (iliyorekebishwa)/ a theology of the New Tetament (revised)**

Allstair Mcgrath - **teolojia ya kikristo; utangulizi/ christian theology introduction**

J.I Packer - **Teolojia fupi,mwongozo wa historia ya imani ya Kikristo / a guide to Historic Christian beliefs**

J.I Packer - **kumjua Mungu/ knowing God**

John Scott - **Msingi Wa Ukristo/ basic Christianity**

**MSALABA NA UFUFUO**
Paul Beasley - **Murray Ujumbe Wa Ufufuo/ The Message of Resurrection of Jesus**

John Scott - **msalaba wa yesu/ the cross of Jesus**

Derek Tidball - **ujumbe wa msalaba/ (Biblia inazungumza Leo)/ the message of the cross (the bible speaks today)**

D.A Carson - **kashfa: Msalaba na ufufuo wa Yesu scandalous: The Cross And The Resurrection of Jesus**

**KUHUBIRI NA KUWASILIANA**
Bryan Chapell - **Mahubiri ambayo Yesu Yuko Kati/Christ centered preaching**

Zack Eswine - **kuhubiri kwa ulimwengu wa baada ya kila kitu/ preaching to a Post Everything World**

Carmine Gallo - **zungumza kama Ted - siri tisa za usemaji kutoka kwa akili kuu duniani/ talk**

**like Ted: The 9 public speaking secrets of world's top minds**

Tim Keller - **mahubiri,kuwasilisha imanika katika umri wa shaka/ preaching: communicating faith in the age of skepticism**

Dereck Tidball - **mhubiri jikinge kutokana na masanamu/ preacher keep yourself from idols**

## BIBLIA – THE BIBLE

Craig. L.Bloomberg - **Yesu na injili/ Jesus and the gospels**

Gordon D. Fee & na Douglas Stuart - **Jinsi ya kusoma Biblia na thamani yake/ how to read the Bible and all that is worth**

Gordon D Fee &Douglas Stuart - **jinsi kusoma Biblia kitabu kwa Kitabu/ how to read the bible book by book**

Mark.L. Strauss - **Picha Nne yesu mmoja/ four portraits one Jesus**

Peter J. Williams - **je! Tunaweza kuamini injili? / can we still Trust the gospels?**

Pata masomo ya biblia nzuri ikiwa hauna moja tayari (wingi wa tafsiri kuu za Biblia kama vile ESV, NIV, KJV, NRSV, NLT kila linatoleo moja la kujifunza na kamusi ya Biblia iliyo imara (Becker, Erdmans, Harper collins, kamusi mpya ya Biblia/ new Bible dictionary

## UTETEZI WA IMANI

Tim Keller - **Sababu Ya Mungu/ The Reason For God**

C.S .Lewis - **Ukristo Tu/ Mere Christianity**

Josh Mcdowell - **Ushahidi Mpya Unaohitaji Uamuzi/ The New Evidence That Demands A Verdict**

Allstair Mcgrath - **utetezi wa imani tu, jinsi ya kuwasadia wanaotafuta na walio na shaka wapate imani/ mere apologetics ,how to help saeekers and skeptics find faith**

Frank Turek - **kumuibia Mungu/ stealing from God**

J.Warner Wallace - **Ukristo kesi b aridi/ cold case Christianity**

Lee Strobe - **kesi ya Yesu/ The Case For Christ**

Christopher yuan - **[utakatifu wa hali Ngono na Injili Ya Yesu Kristo/ Holy sexuality and the Gospel**

## MAELEZO

Msingi/ ibada l - **mifululizo ya "ya kila mtu", "ni yako"**

Utangulizi - **Biblia inazungumza leo matumizi ya NIV**

Inayofuatilia - makamu Rais, Tyndale, wafafanuzi wa maelezo ya kiBiblia (iliyorudiliwa); uelewaji wa Biblia

Cha juu: Pillar(Agano ya zamani); Apollos (Agano jipya) maelezo mapya ya kitaifa; upedo mbili

## UONGOZI

Ken Blanchard na Phil Hodges - Ongoza kama yesu/ lead like Jesus

Robert greenleaf na Larry spears - nguvu ya kiongozi mtumishi/ the power of a servant leader.

Peter Scazerro, kiongozi aliye na afya ya kihisia moyo.

## RASLIMALI ZILIZO MTANDAONI

Reasonablefaith.org

Coldcasechristianity.com

Apologetic315.com

## RASLIMALI ZA DVD/USB

talkingjesus.org

Alpha.org

Dare2share.org

# MASWALI YA UWAJIBIKAJI

‘Ee mungu unichunguze uujue moyo wangu, unijaribu, uyajue mawazo yangu’ (ZABURI 139:23)

Mkubali kila mmoja (WARUMI 15:7) Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi (YAKOBO 5:16) Basi farajieni na kujengana kile mtu na mwenzake (1 WATHESOLANIKE 5:11)

## KIELEKEZI

✓ VIZURI/NJEMA
— SAWA
✗ MBOVU/VIBAYA

**‘Ishi kulingana na utambulisho uliopewa na mungu,ishi kwa urarimu na neema juu ya kila mmoja wenu jinsi mungu unavyoiishi juu yenu.’ (MATHAYO 5:48, MSG)**

| | |
|---|---|
| Je! Taswira yangu ya maisha ni safi kwa kiwango gani? | |
| Je! Taswira yangu ni safi kwa kiwango gani kulingana na niliojihusisha nayo? | |
| Je! Napenda kile ninachokifanya? | |
| Je! Ninahisi furaha ya mungu kwa kile ninacho kifanya? | |
| Je! Ashiki kwa kazi hii? | |
| Je! Nina fuatilia uhusiano wa karibu na yesu? | |
| Je! Ninatengeneza nafasi ya kutosha kwa maombi? | |
| Je! Nina tumia muda katika masomo ya kibiblia ya kibinafsi? | |
| Je! Biblia iiliishi ndani yangu leo? | |
| Je! Ninatafuta ushahidi kuhusu nguvu ya mungu katika maisha yangu na huduma yangu? | |
| Je! Yesu ni wa ukweli kwangu? | |
| Je! Mimi ni rahisi wakufundishika na uwajibikaji? | |
| Je! Unapatikana na una urahisi wakusogelewa? | |
| Je! Nasikiza vizuri? | |
| Je! ninaongoza na moyo wa mtumishi? | |
| Je! Nimejiweka wazi kwa wengiene? | |
| Je! Mimi ni wa kuaminika? | |
| Je!ninaweka ahadi zangu? | |
| Je! Nimeshikilia msimamo mzuri? | |
| Je! Nina kabiliana na presha vizuri (kutoka kwa watu,kazi na hali) | |
| Je! Afya yangu ikoaje? | |
| Je! Nina kula vizuri? | |
| Je! Nina lala,vizuri? | |
| Je! Ni nani kubali maawazo yangu kushinda sehemu potovu? | |
| Je! Ninawakumbuka wale walio wagonjwa, wanaoumia na walio na mahitaji? | |

| | |
|---|---|
| Je! Familia yangu wanafuraha? | |
| Je! Mahusiano yangu yako vipi? Je! Mahusiano na wale tunaohudumu pamoja, wenzangu, viongozo na wa jinsia tofauti yako sawa? Je! Jibu langu ni la afya aje kwa kuwa na njaa, kukasiririka, ukiwa hohehahe? | |
| Je! Ninajihusisha na mawazo machafu/ mapotovu? | |
| Je! Napumzika vya kutosha? | |
| Je! Ninatunza wakati vizuri? | |
| Je! Natumia muda wangu wa ziada kwa njia nzuri na yenye afya? | |
| Je! Naweka/dumisha maisha ya usawaziko kati ya kanisa, kazi, na maisha ya nyumbani? | |
| Je! Nina anzisha na kudumisha uhusiano na watu wasio wakristo? | |
| Je!nimejiweka wazi kwa vitu ambavyop vinavutia ngono? | |
| Je! N imeshindwa katika sehemu yoyote ya maisha: kuwa na wivu,mchafu{kushirki katika ngono)mkosoaji/ mpekuzi, una tabia za kuudhi, kutoaminika,kukasirika kwa upesi? | |
| Je!natunza fedha/ pesa zangu vizuri? | |
| Je! Na toa kwa ukarimu? | |
| Je! Nachagua kutokuwa na wivu kwa wengine? | |
| Je! Nachagua kutonung’unika au kulalamika? | |
| Je! Natembea katika uadilifu? | |
| Je! Nina mimi ni mtu mwamuzi na jasiri? | |
| Je! nipo tayari kujihatarisha? | |
| Je! n inaweka wa malengo na kuyafika? | |
| Je! Niko tayari kujitolea | |
| Je! Nina dumisha makali yangu? | |
| Je! Nina songa kwa roho mtakatifu? | |
| Je! Nazuia msamaha kwa mtu? | |
| Je!nafuatilia uhuru/ kujikomboa katika ngome na mifumo ya uharibifu? | |

**‘Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenywewe, sikiza sauti ya mungu kwa kila kitu amachop ufanya, kila unakoenda. Nini atakayekuelekeza, usidhani kuwa unajua kila kitu, mkimbilie mungu,toroka maovu.’ (MITHALI 3:5-7)**

# INJILI HAKUNA MPANGO WA “B”.

ADVANCEGROUPS.ORG

LUIS PALAU ASSOCIATION

the message